# MATUMIZI YA UTANZIA KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED

Na

Haji Khatibu Ali

Tasnifu Imetolewa kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi Jamii katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma

Chuo Kikuu cha Dodoma

October, 2015

# ITHIBATI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa ***'Matumizi ya Utanzia katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed'*** ikubaliwe kwa azma ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi Jamii katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

………………………………………

Dkt A.S Ponera

(Msimamizi)

Tarehe ……………………

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, **Haji Khatibu Ali,** ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi. Haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa minajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote.

Saini ya Mtafiti…………………….................

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

# SHUKRANI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu. Sina budi kumshukuru Allah (s.w) aliyeniumba na kunipa uhai ulioniwezesha kujifunza elimu mbalimbali ikiwemo taaluma hii ya Kiswahili. Aidha, mafanikio ya tasnifu hii yametokana na msaada pamoja na ushauri kutoka kwa watu kadhaa. Naomba kuwataja baadhi kwa mchango wao uliohitimisha upatikanaji wa tasnifu hii.

Kwanza, natoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu, Dkt. Athumani Salum Ponera, ambaye alijitolea kuniongoza, kunielekeza na kunisimamia kwa kunipa mawazo, fikra pamoja na ushauri wa kitaalamu ulionisaidia kunipa msukumo wa kuikamilisha tasnifu hii kwa kiwango cha kitaalamu. Pili, ninaishukuru SMZ iliyoniruhusu kufanya utafiti katika maeneo ya Unguja na Pemba.

Tatu, nawashukuru wahadhiri wangu kwa kuwa pamoja nao katika kipindi chote cha masomo. Miongoni mwao ni Prof. Joshua Samwel Madumulla, Dkt. Muhammed Seif Khatib, Dkt. Elias Manandi Songoyi, Dkt. Rafiki Yohana Sebonde na Dkt. Athumani Salum Ponera wote kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, kwa kunijenga vyema katika taaluma ya utafiti na Fasihi ya Kiswahili.

Nne, napenda kumshukuru mke wangu kipenzi, Yusra Sultan Mohamed, pamoja na wazazi wangu wawili walionilea ambao ni Halima Saadat Khamisi na Khatibu Ali Khatibu, pamoja na ndugu zangu wa karibu kwa kunipa msaada na kunistahamilia kwa kipindi chote tangu mwanzo wa masomo ya Uzamili hadi kukamilika kwa tasnifu hii.

## TABARUKU

**Kwa Mama Mzazi**

Wengi hawakuelewi mama,
nao hujifanya wapenzi kwako,
kumbe kinyume cha mambo,
hujifanya wakujali sana,
Wana nia zao mbaya kwako,
kwangu mimi tambua mama,
*Chua haiharibu wali.*

**Kwa Baba Mzazi**

Malezi yako matamu baba,
tamu kwenye mate na ulimi,
umechukua nafasi kwangu,
kwa moyo na akili,
mimi nakwambia baba,
*Sikio halizidi kichwa.*

# IKISIRI

Tasnifu hii, inahusu Matumizi ya Utanzia katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed. Riwaya zilizochuguzwa ni *Utengano*, *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru*. Dhana ya utanzia katika tasnifu hii ina maana ya maneno matendo au mazingira yanayozua kwa hadhira huzuni, jitimai, majonzi, masikitiko, majuto na maumivu ya mwili, roho au akili. Utanzia unajengwa na vipengele kama vile vifo, ajali, vifungo, mabalaa, ulemavu, vilio, maradhi, njaa na mateso. Yumkini, hakuna uchunguzi wa kutosha kuhusu matumizi ya utanzia katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Hali hii imesababisha tatizo katika kuzielewa kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili.

Utafiti ulifanyika maktabani na uwandani. Maktabani tuliyadurusu mapitio mbalimbali kama vile: Majarida, tasnifu, tahakiki, makala na vitabu. Uwandani tulitumia mbinu ya mahojiano, majadiliano na udodosi. Kwa namna fulani mbinu hizi zilitusaidia katika kukusanya data mbalimbali zinazohusiana na utafiti huu. Maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Kusini Unguja, Dodoma na Dares Salaam yalitumika katika ukusanyaji wa data. Utafiti ulitumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo ilitumika kwa kupata fikra binafsi za wasomaji kutokana na uelewa wao wa vitabu teule walivyovisoma. Uchambuzi wa data uliegemea katika maelezo kwa kuwa utafiti huu ni wa kitaamuli. Hivyo, haukujihusisha na mwegamo wa kitakwimu.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha utanzia ni mbinu ya kibunulizi inayofungamana na utanzu mkongwe wa tamthiliya za kitanzia ambazo ndani yake hutoa athari maalum kwa wasomaji.

## YALIYOMO

**ITHIBATI** ............................................ **i**

**IKIRARI NA HAKIMILIKI** ............................................ **ii**

**SHUKRANI** ............................................ **iii**

**TABARUKU** ............................................ **iv**

**IKISIRI** ............................................ **v**

**YALIYOMO** ............................................ **vi**

**VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA** ............................................ **ix**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ............................................ **1**

1.1 Ufafanuzi wa Dhana za Msingi ............................................ 1

1.1.1 Tanzia ............................................ 1

1.1.2 Tanzia – futuhi ............................................ 3

1.1.3 Utanzia ............................................ 4

1.1.3.1 Vijenzi vya Utanzia ............................................ 5

1.1.3.1.1 Mateso ............................................ 5

1.1.3.1.2 Ajali ............................................ 6

1.1.3.1.3 Maradhi ............................................ 6

1.1.3.1.4 Kifo ............................................ 6

1.1.3.1.5 Kifungo ............................................ 7

1.1.3.1.6 Ulemavu ............................................ 7

1.1.3.2 Matokeo ya Utanzia ............................................ 7

1.1.3.2.1 Huzuni ............................................ 7

1.1.3.2.2 Kilio ............................................ 8

1.1.3.2.3 Maumivu ............................................ 8

1.1.3.2.4 Msawajiko ............................................ 8

1.2 Histori Fupi ya Said Ahmed Mohamed ............................................ 9

1.3 Usuli wa Tatizo Ia Utafiti na Tamko la Utafiti ............................................ 14

1.3.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ............................................ 14

1.3.2 Tamko la Tatizo la Utafiti ............................................ 17

1.4 Malengo ya Utafiti ............................................ 18

1.4.1 Lengo la Jumla ............................................ 18

1.4.2 Malengo Mahsusi ............................................ 18

1.5 Maswali ya Utafiti ... 19
1.6 Manufaa ya Utafiti ... 19
1.7 Nadharia ya Utafiti ... 19
1.8 Mipaka ya Utafiti ... 22
1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ... 23

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO ... 24**
2.1 Utangulizi ... 24
2.2 Maandiko Kuhusu Utanzia Katika Kazi za Fasihi ... 24
2.3 Maandiko Kuhusu Utanzia Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed ... 31
2.4 Mapengo Yanayojitokeza ... 34
2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili ... 34

**SURA YA TATU: MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI ... 35**
3.1 Utangulizi ... 35
3.2 Mpango wa Utafiti ... 35
3.3 Eneo la Utafiti ... 35
3.4 Walengwa wa Utafiti ... 36
3.4.1 Jamii ya Watafitiwa ... 36
3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji Wake ... 37
3.5 Ukusanyaji wa Data ... 38
3.5.1 Mbinu na Zana za Kukusanyia Data ... 38
3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake ... 38
3.6 Uchambuzi na Uunganishaji wa Data ... 39
3.7 Vikwazo vya Utafiti ... 40
3.8 Muhtasari wa Sura ya Tatu ... 40

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI ... 42**
4.1 Utangulizi ... 42
4.2 Miktadha ya Maisha ya Said Ahmed Mohamed ... 42
4.2.1 Said Ahmed Mohamed na Mfumo wa Dini ... 42
4.2.2 Said Ahmed Mohamed na Lugha ya Kiswahili ... 44

4.2.3 Said Ahmed Mohamed na Taaluma ................................................................ 46
4.2.4 Said Ahmed Mohamed na Uandishi wa Zama Hizi ......................................... 48
4.2.5 Said Ahmed Mohamed na Mfumo wa Kisiasa ................................................ 49
4.2.6 Muhtasari ....................................................................................................... 51
4.3 Matukio ya Kitanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed ............... 51
4.3.1 Aina za Utanzia ............................................................................................... 51
4.3.1.1 Utanzia wa Kimwili ....................................................................................... 51
4.3.1.2 Utanzia wa Kiakili .......................................................................................... 52
4.3.1.3 Utanzia wa Kiroho .......................................................................................... 52
4.4 Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed ............................................................ 54
4.4.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Utengano* (1980) ..................................................... 54
4.4.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* ( 2002) ........................................ 56
4.4.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Kiza Katika Nuru* (1988) .......................................... 58
4.5 Matukio ya Kitanzia Yaliyotumika Katika Riwaya Teule .................................. 60
4.5.1 Matukio ya Kitanzia Katika Riwaya ya *Utengano* ........................................... 60
4.5.2 Matukio ya Kitanzia Katika Riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* ............................... 66
4.5.3 Matukio ya Kitanzia Katika Riwaya ya *Kiza Katika Nuru* ............................... 73
4.6 Athari za Matukio ya Kitanzia kwa Wasomaji ................................................... 78
4.6.1 Athari Chanya .................................................................................................. 78
4.6.2 Athari Hasi ....................................................................................................... 80
4.7 Muhtasari wa Sura ya Nne ................................................................................... 81

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .......... 83**
5.1 Utangulizi ............................................................................................................ 83
5.2 Muhtasari wa Tasnifu .......................................................................................... 83
5.3 Utoshelevu wa Nadharia Katika Utafiti .............................................................. 84
5.5 Maoni Kuhusu Utafiti .......................................................................................... 86
5.6 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo ............................................................................. 86
**MAREJELEO ........................................................................................................ 87**
**VIAMBATISHO ................................................................................................... 92**

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| BA | — *Bachelor of Art* |
| BAKIZA | — Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| BBC | — *British Broadcasting Cooperation* |
| Bw. | — Bwana |
| Dkt | — Daktari |
| DW | — *Deutshe Welle* |
| h.t | — haina tarehe |
| http | — *Hyper Text Transfer Protocal* |
| KK | — Kabla Kristo |
| k.h.j | — Keshatajwa hapo juu |
| Ltd | — *Limited* |
| MA | — *Master of Art* |
| Mh. | — Mheshimiwa |
| Mr. | —*Mister* |
| Ph D | — *Doctor of Philosophy* |
| Prof. | — Profesa |
| SAW | — *Swalla-llahu Alayhi Wasallam* |
| SMZ | — Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SUZA | — *State University of Zanzibar* |
| SW | — *Subuhana Wata'ala* |
| TAKILUKI | — Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni |
| TPDF | — *Tanzania People Defence Force* |
| TTC | —*Teacher Training College* |
| TUKI | — Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |

| | |
|---|---|
| UDOM | — *University of Dodoma* |
| UDSM | — *University of Dar es Salaam* |
| Uk. | — Ukurasa |
| www | — *World Wide Web* |
| ZBC | — *Zanzibar Broad-casting Cooperation* |
| ZU | — *Zanzibar University* |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Ufafanuzi wa Dhana za Msingi

Sehemu hii inaeleza maana, chimbuko, vijenzi na matokeo ya utanzia. Dhana ya utanzia imetumiwa kwa kuinasibisha na dhana ya msingi ya tanzia. Kwa hiyo ufafanuzi unaanza na dhana yenyewe ya tanzia.

### 1.1.1 Tanzia

Islam (2009: 157) anaifasili dhana hii kuwa ni tamthiliya ambayo ina tendo ambalo lina uwezo wa kuwaathiri watazamaji na kuwafanya waingiwe na huzuni au simanzi. Mulokozi (1996: 191) anaongezea kuwa tanzia ni drama juu ya mkasa unaomsibu mtu mashuhuri kutokana na matukio ambayo mara nyingine hana uwezo nayo na ambayo yanapata msukumo kutokana na udhaifu fulani alio nao, na huishia katika majonzi. Naye Simon (2014) akimnukuu Aristotle anadokeza tanzia kuwa ni mwigo au uigaji wa tendo lenye udhati, ukamilifu, waingiwe na huzuni au kihoro pamoja na kuwa na uwezo wa kuzitawala hisia za woga au huzuni katika mtakaso Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, yumkini tanzia inafungamana na matendo yanayoigizwa majukwaani. Hivyo, matendo ya wahusika ni yale yanayotoa athari ya huzuni, simanzi na woga kwa watazamaji.

Chimbuko la dhana ya tanzia inatokana na jamii ya Kiyunani. Kisawe chake kinatokana na lugha ya Kiingereza ambayo ni ‘*Tragedy*’. Neno hilo nalo linatokana na lugha ya Kiyunani *tragōidia*, au “*goat-song*,” lenye asili ya neno *tragos* (*goat*) na *aeidein* (*to sing*). Maneno haya yalimaanisha ni zawadi ya mbuzi wanayopewa washindi wa mwanzo katika uigizaji. Lengo la zawadi hiyo ni kupata ngozi ya mbuzi

kwa wale washindi wa tamthiliya, au kutolewa sadaka katika matambiko ya jamii za watu wa Uyunani ya kale. Tanzia ilianzia katika miviga ya kidini katika sherehe za kumhusu 'Dionisius'. Wachezaji na waigizaji walivalia na kuonekana kama mbuzi huku wakiimba nyimbo zilizohusu anguko la shujaa. Katika sherehe hizo, watu 100 hushiriki kwa kuimba na kucheza, wakiongozwa na mzungumzaji mkuu pamoja na msaidizi wake. Hawa ndio wanaobuni muundo wa tanzia na kufanya mazungumzo (*Dialogue*). Watu 100 walioshiriki huaminika ni waigizaji wa kitanzia, kwa sababu waigizaji 90 wakisaidiana na msemaji mkuu hupotea na kubakia watu 7 tu (Catwright, 2013 na *Encyclopedia Britanica*, 1911). Kwa maoni yetu, tunaamini upoteaji huo ndio unaozua masikitiko na majonzi kwa hadhira iliyopo. Kuanzia kipindi hicho, matukio kama hayo yalienea katika jamii mbalimbali barani Ulaya na duniani kwa jumla. Matukio hayo yote yaliambatana na huzuni zenye kufungamana na vilio. Baadaye, matukio hayo yaliingizwa katika kazi mbalimbali za fasihi andishi kama vile ushairi, tamthiliya na nathari.

Aristotle[1] katika andiko lake la *Poetics,* ameorodhesha sifa mahsusi zinazohusiana na utanzu mdogo wa tamthiliya ya tanzia. Katika uchunguzi wake alivitambua vipengele sita vyenye kuleta ukamilifu wa muundo wa tanzia. Vipengele hivyo, ni msuko, wahusika, dhamira, nyimbo, maonyesho na uteuzi wa maneno. (Butcher, 1961 na Preston, 2014)

Mtaalamu huyu aliwagawa watu katika hadhira kuu mbili. Ambazo ni hadhira ya watu wa nasaba bora (Wafalme, Mashujaa na Wasomi) na ile ya watu duni. Anapendekeza kuwa, kundi la kwanza ndilo lenye kazi ya fasihi ya kitanzia

[1] Ni mwanafalsafa wa Kiyunani aliyeishi Uyunani (Ugiriki ya Kale) kati ya mwaka 386 na 322 Kabla ya Kristo. (E. Hussein, 1983:194) Alizaliwa katika sehemu iitwayo Stagira, huko Kaskazini Mashariki mwa Aegean, mwaka wa 384 KYM. Alipokuwa na miaka 17 alikuwa tayari mwanafunzi wa Plato huko Athens. Mwaka 335 Aristotle alianzisha talimia yake Peripatetic School ambayo ilidumu hadi 323 KYM (Senkoro, 1987: 48)

inayowafaa huwa na akili za kuchambua masuala ya kimchangamano yanayoibuka humo. Kwa upande wa hadhira ya watu duni alipendekeza kuwa kazi ya fasihi inayowafaa ni ya vichekesho na komedia. Kwa kuwa akili zao hazikuhitaji kufikirishwa wala hazikuwa na uwezo wa kuchambua. Hivyo, husisimuliwa na kuchangamshwa kikomedia na vichekesho (Senkoro, 1987). Mawazo haya, licha ya kujifunga katika utanzu mdogo wa tanzia, tunaweza kuyachukulia kama njia faafu ya kutathimini mwelekeo wa tanzu nyingine za fasihi ambazo ni riwaya, ushairi, semi, hadithi na sanaa za maonyesho.

Mnamo karne ya 5 Kabla ya Kristo (KK), zilikuwapo kazi za mwanzo zilizoandikwa na Wayunani kuhusiana na tanzia. Baadhi ya wataalamu hao ni: Euripdes (480 - 406 KK), Sophocles (496 – 406 KK) na Aeschylus (525 – 456 KK). Wengine walioibuka baada ya ujio wa Yesu Kristo ni waandishi kama vile William Shakespeare [2](1564 - 1616) wa Uingereza na Jean Basptiste Poquelin Moliere wa Ufaransa. Shekespeare alitunga tamthiliya zipatazo 38 zilizojikita katika utunzi wa tanzia yenye asili za Kiyunani. Tamthiliya nne kati ya hizo 38 zilitafsiriwa na wataalmu mbalimbali, mathalani, Mwalimu Julias Nyerere alizitafsiri tamthiliya mbili za Shakespeare ambazo ni Julias Kaisari na Mabepari wa Venisi. Pia, SS Mushi alizitafsiri tamthiliya mbili za Shekespeare ambazo ni Makbeth na Tufani. (Mulokozi, 1996; Saluhaya na Suleiman, 2012).

### 1.1.2 Tanzia – futuhi

Kisawe cha tanzia – futuhi katika lugha ya Kiingereza ni *'Tragi comedy'*. Ni tamthiliya ambayo huonyesha mabadiliko ya aina fulani yanayogeuza mwelekeo wa matukio ya kitanzia na kuufanya kuwa tofauti au wa kufurahisha (Simon, 2014;

[2] Ni Mwingereza ambaye inasemekana alibatizwa 26 April 1564 na alifariki 23 April 1616. Alikuwa ni mshairi na mtunzi wa tamthiliya maarufu kati ya karne ya 16 na 17 (Mulokozi, 1996: 191)

Islam, 2009). Naye Wamitila (2003: 219) anatilia nguvu kwa kusema: "Hutumiwa kuelezea aina ya tanzia ambayo inahusisha mbinu za futuhi". Kimsingi neno hili hutumiwa kurejelea aina mojawapo ya aina ya tamthiliya au drama ambayo huwa na miishio ya furaha au ramsa. Hata hivyo, katika muundo wa kifasihi, neno futuhi hutumiwa kwa maana pana na ni sifa inayokiuka utanzu na kupatikana pia tanzu nyingine kama vile riwaya na hadithi fupi ambazo aghalabu huishia kwa furaha. Maelezo ya wataalamu hawa yanatuzidishia maarifa kuwa si mara zote tanzia kuanzia mwanzo hadi mwisho hutoa hisia za kuhuzunisha kwa hadhira yake. Hali hii inaweza isitokee mwanzoni mwa tamthiliya, bali inaweza kutoa furaha mwishoni kutokana na matumizi ya mbinu za kifutuhi kama kejeli. Hii ikiwa na maana kuwa tanzia na futuhi huwa na mwingiliano na huathiriana. Aghalabu, wahusika wake hutumia kejeli za kuchekesha hadhira. Ijapokuwa kuna shida fulani inayowakabili. Kwa jicho la kitaaluma, dhana hii ina umuhimu katika utafiti wetu. Kwani mshabaha wake ni kutoa uhusiano uliopo kati ya matukio ya kitanzia na yale ya kifutuhi katika drama moja. Jambo hili linashadidiwa na Senkoro (2011:71) anaposema kuwa matukio ya kitanzia hujitokeza katika fasihi simulizi na andishi ambayo husikitisha katika hali ya taharuki. Baadaye mtambaji hutumia mbinu ya ucheshi ili hadhira yake ipumue kidogo kwa kutabasamu.

### 1.1.3 Utanzia

Ponera (2014) anafafanua kuwa utanzia ni mbinu ya kibunulizi ambayo mtunzi hutunga kazi yake ya kifasihi na kuweka vipengele mbalimbali viwezavyo kuzua hali ya huzuni, masikitiko, jitimai na mateso kwa hadhira yake. Maelezo ya mtaalamu huyu yanafichua ukweli uliopo kwamba utanzia ni mbinu ya kibunulizi inayojikita katika kazi za kifasihi ambayo shabaha yake kuu ni kuihuzunisha jamii. Sifa kuu ya

mbinu hii ni kutumika katika utanzu wowote wa fasihi, licha ya kuchimbuka katika tanzia. Katika tasnifu hii, utanzia una maana ya maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye kuifanya hadhira ihuzunike. Tumeitofautisha dhana ya utanzia na tanzia kwa hoja kuwa: Tanzia hujiegemeza katika suala la utendaji, hususan matendo ya jukwaani. Upande wa utanzia ni mbinu inayojengwa kwa misingi ya kuibua majonzi, masikitiko, jitimai na huzuni.

#### 1.1.3.1 Vijenzi vya Utanzia

Vijenzi vya utanzia, kwa mujibu wa Ponera (2014) ni mateso, hali ya ugumu wa maisha, manyanyaso, ajali na vifungo. Vingine ni ulemavu wa viungo au mapungufu ya mifumo au michakato ya mwili kama vile ugumba au utasa. Vilevile, utanzia huweza kujengwa kupitia mabalaa makubwa kama vile njaa, mafuriko, kimbunga, pamoja na milipuko ya magonjwa. Tunaafikiana na mawazo ya mtaalamu huyu kuhusu vijenzi hivyo. Bado kuna tatizo la kuwapo kwa idadi mahsusi ya vijenzi hivyo. Hii inaonekana vijenzi viundavyo utanzia ni kadhaa. Imani hiyo, imetufanya tuviwekee mipaka. Utafiti huu umeviweka vijenzi hivyo katika maeneo yafuatayo:

##### 1.1.3.1.1 Mateso

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya 21* (2011), mateso ni mambo anayofanyiwa mtu ili kumtaabisha, au kumpa  madhila na tabu. Nao TUKI (1981) wanaongeza kwa kusema kuwa ni hali ya kumuadhibu mtu au mnyama au kwa maana nyingine ni madhila na maonevu. Kwa jumla, maelezo haya yanatujengea hoja ya kuwa yumkini utesaji wa namna yoyote huwa na dhamira ya kumwonea mtu mwingine ambapo humweka katika hali ya masikitiko na majonzi ya mwilini au akilini.

#### 1.1.3.1.2 Ajali

Istilahi hii inafafanuliwa na *Kamusi ya Kiswahili Fasaha* (2010) kuwa ni tukio la ghafla lisilotarajiwa ambalo husababisha madhara au hatari. Kwa upande wa *Kamusi ya Karne ya 21* inaona kuwa ni tukio linalodhuru na hutokea kwa bahati mbaya. Msingi wa maelezo haya ni kuwa ajali ina mkusanyiko wa mambo makuu mawili ambayo ni tukio lisilopangwa kwa makusudi na mwisho wake huibua madhara kwa mtu. Kwa namna hiyo, msingi mkuu wa ajali ambayo imetoa maafa hukwepesha furaha au kicheko kwa aliyefikwa na ajali hiyo.

#### 1.1.3.1.3 Maradhi

Njogu na wenzake (2011) wanaifasili dhana hii kuwa ni kitu kinachoathiri afya ya mtu au mnyama. Pia wanaongeza kuwa ni ugonjwa, ndwele au ukongo. Wakati ambapo Kiango na wenzake (2007) wanaifasili dhana hii kuwa ni hali ya kuwa na afya mbaya sana. Msingi mkubwa wa maradhi ni kuidhoofisha afya ya kiumbe hai. Aghalabu, maradhi yanapovishambulia viungo vya kiumbe humweka katika hali ya kukosa amani ya mwili na akili. Hivyo, katika kipindi chote cha maradhi mtu hupoteza furaha.

#### 1.1.3.1.4 Kifo

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981) inafasili kuwa ni uondokaji wa roho mwilini. Pia ni tukio la kufa au mwisho wa uhai. Kwa jumla, upo uhusiano kati ya mwili na roho ambapo mfungamano wao hukifanya kiumbe kiishi. Mwingiliano huo unapokatika ndipo husemwa mtu fulani amekufa. Athari ya kifo hicho huwaweka jamaa wa karibu kuwa na jitimai.

#### 1.1.3.1.5 Kifungo

Mohamed na Mohamed (1998) neno hili ni sawa na maneno kama vile gereza, jela na korokoro. Nao TUKI (1981) wanaeleza kuwa ni adhabu ya mtu kuwekwa mahabusu au rumande au ni kizuizini. Pamoja na maelezo haya, msingi wa maisha ya jela ni kumyima mfungwa uhuru wa maisha yake. Hivyo, maisha ya gerezani huzua majonzi kwa mfungwa mwenyewe au watu wake wa karibu.

#### 1.1.3.1.6 Ulemavu

Kiango na wenzake ( 2007) wanalifasili neno hili kuwa ni hali ya kiungo cha mwili kuwa na hitilafu fulani. Wanaendelea kusema kuwa ni hali ya kulemaa au hali ya kuwa kilema. Kutokana na mawazo ya jumla ya maelezo haya, ni wazi ulemavu ni sehemu ya mwili yenye kuonyesha kasoro fulani, ambapo kasoro hiyo inakwenda kinyume na maumbile ya kiumbe hai. Ulemavu unaweza kutokea mwilini au akilini ukisababishwa na maumbile ya asili (tangu kiumbe kinapozaliwa) au harakati za kimaisha kwa mfano ajali au mabadiliko ya mwili.

### 1.1.3.2 Matokeo ya Utanzia

#### 1.1.3.2.1 Huzuni

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya 21* (2011), huzuni ni hali ya kutokuwa na furaha, majonzi, simanzi, masikitiko, sononeko na jitimai. Pia, Bakhersa (1992) anafafanua kuwa huzuni ni majonzi, masikitiko na simanzi. Mohamed na Mohamed (1998) wanaeleza kuwa huzuni ni ghamu, majonzi, jitimai, masikitiko, simanzi, kibuhuti, mbawazi, buka, shakawa, sononeko, na msiba. Naye Kiango na wenzake (2007) wanaeleza kuwa ni hali ya kuwa na masikitiko au majonzi au hali ya kukosa furaha. Maelezo haya yanatupa hoja mbili. Mosi, huzuni ni mbinu inayotumiwa na wanafasihi kwa lengo la kuiweka hadhira katika hali ya kukosa furaha. Pili, kwa

jicho la kitaaluma maneno kama vile majonzi, simanzi, masikitiko na jitimai tunayachukulia kuwa ni maneno yenye maana moja na hayana tofauti yoyote.

#### 1.1.3.2.2 Kilio

Kilio, kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Fasaha* (2010) ni sauti inayoashiria maumivu, msiba, huzuni au kutoridhika na jambo. Fasili ya Mohamed na Mohamed (1998) inaongeza zaidi kwa kueleza kuwa ni ukelele, ukwenzi, siyahi, unyange, yowe na unyende. Maelezo haya yanatupa hoja ya jumla kuwa utokeaji wa kilio huenda sambamba na mtu anapohuzunika. Mathalani, katika matukio kama vile mazishi, majanga ya kimaumbile na mikosi mbalimbali. Hii ni hali ya kudhoofika kwa moyo na akili ya mwanadamu. Kwa hivyo, kilio huweza kutokea katika hali ya uwazi au usiri au kutegemeana na jinsi au umri wa mhusika.

#### 1.1.3.2.3 Maumivu

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2010) inafafanua kuwa ni hisia ya uchungu anayopata mtu kutokana na kuumia. Kiango (2007) anaongezea kuwa ni hali ya kusikia uchungu kwa sababu ya jeraha au ugonjwa. Fasili ya kwanza imetoa sababu ya maumivu ni kuumia na fasili ya pili ni jeraha au ugonjwa. Kutokana na fasili hizi inaonekana maumivu yanahusiana kwa namna moja au nyingine na hisia za uchungu azipatazo mtu baada ya kukabiliana na tatizo fulani. Katika tasnifu hii sababu ya maumivu tunaipeleka mbele zaidi kuwa ni jambo lolote linalompa mtu uchungu wa kiakili, kiroho au kimwili.

#### 1.1.3.2.4 Msawajiko

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981: 250), sawajika ni kubadilika hali na kuwa mbaya hasa kutokana na shida, njaa au ugonjwa. Kutokana na maelezo ya fasili hii,

aghalabu, mtu anapokumbana na moja kati ya matatizo yaliyoainishwa au zaidi ya matatizo hayo; hubadilika kisaikolojia au hata kimwili. Mathalani, mtu anapofiwa na mpendwa wake huweza kupata msawajiko wa akili na kumsababishia hadi kuzirai. Kwa jumla, suala la kufikwa na matatizo ni chanzo cha mtu kupatwa na msawajiko usiotarajiwa; ndio maana hata matukio ya kitanzia ni kiunzi muhimu kwetu katika kubainisha hatma ya utanzia.

## 1.2 Histori Fupi ya Said Ahmed Mohamed

Alizaliwa Pemba tarehe 12 Disemba 1947, hakupata malezi ya baba mzazi na mama mzazi kwa kuwa wazazi wake walitengana akiwa mdogo. Hali hii ilisababisha kulelewa na mama zake wakubwa ambao ni Bi-Jokha na Bi-Rukia. Mama wa Said Ahmed Mohamed anaitwa Fatma Said Suleiman. Wazazi wake wawili kila mmoja anatoka kisiwa chake. Kwa upande wa babaake ni mzaliwa wa Pemba. Na mamaake ni mzaliwa wa Unguja.

Said Ahmed Mohamed alifunga ndoa ya Kiislamu, na mwenza wake aitwae Bi Rahma. Walibahatika kupata watoto watatu ambao ni Najma[3], Mahir[4] na Fatma. Mtoto wake wa tatu (Fatma) alifariki dunia baada ya kuishi kwa siku ishirini tu. Hadi kumalizika kwa tasnifu hii watoto wake wawili bado wapo hai. Hao wawili wamefanikiwa kupata elimu ya shahada ya Awali.

Alianza elimu yake ya msingi katika shule ya Wete Boys iliyopo kisiwa cha Pemba. Baadaye, alihamia shule ya msingi ya Kiembesamaki iliyopo Unguja. Kisha

[3] Mtoto wangu huyu wa kike amenirithi katika uandishi. Lakini yeye huandika kwa lugha ya kiingereza, na si kwa lugha ya Kiswahili kama nilivyo mimi. Kwa sasa anafanya MA katika Media (Mazungumzo ya Prof Said Ahmed Mohamed na mtafitu yaliyofanyika Tarehe 05/03/2015 Mjini Zanzibar)

[4] Mtoto wangu huyu wa kiume anafanyakazi Uingereza. Ameoa mwaka 2014 (Mazungumzo ya Prof. Said Ahmed Mohamed na mtafiti yaliyofanyika Tarehe 05/03/2015 Mjini Zanzibar)

alihamishiwa katika shule ya watoto wenye vipaji maalumu iitwayo skuli ya Darajani. Kwa sasa shule hii ipo Zanzibar Mjini. Masomo yake ya sekondari yalianzia katika shule iliyoitwa ‘King George the VI’. Shule hii kwa sasa inajulikana kwa jina la Gulioni ipo katika maeneo ya Darajani. Wakati yanapotokea mapinduzi matukufu ya Zanzibar, mwaka 1964 alikuwa ni mwanafunzi wa kidato cha pili. Mwaka 1966 alimaliza rasmi masomo yake ya kidato cha nne. Hakuendelea kujiunga na masomo ya kidato cha tano na sita kwa kuwa Raisi wa kwanza wa Jamhuri ya watu wa Zanzibar Shekhe Aman Abeid Karume aliipiga marufuku elimu hiyo ya kidato cha tano na sita. Ndipo Said Ahmed Mohamed, akiwa na umri wa miaka 18, aliamua kusomea fani ya ualimu katika ngazi ya cheti. Mafunzo hayo aliyapata kwa muda wa miaka miwili, katika Chuo cha Ualimu Nkuruma. Alifaulu masomo ya Kiswahili, Kiingereza na Siasa. Baadaye, alijiunga kidato cha tano na sita *(A-level),* huku akiwa mwalimu katika shule ya Utaani. Katika elimu yake ya kidato cha tano na sita, aliamua kusoma masomo ya sayansi. Lakini kutokana na ukosefu wa vifaa vya kufanyia vitendo aliamua kusoma masomo ya sanaa.

Mnamo mwaka 1976, akiwa na umri wa miaka 29 alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa lengo la kusoma elimu ya Shahada ya Awali katika Ualimu. Akimakinia katika Isimu na Fasihi ya Kiswahili. Baada ya kufaulu vizuri, alirejea kwao Zanzibar, kuwa mwalimu mkuu wa shule ya sekondari ya Hamamni. Alidumu katika nafasi hiyo, kwa muda wa miaka mitatu. Mwaka 1981, alichaguliwa tena Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lengo la kujiunga na Chuo hicho, ni kusomea Shahada ya Uzamili katika Isimu. Mwaka 1985, akiwa na umri wa miaka 42, alijiunga Chuo Kikuu cha Karl Max Leipzing kilichopo Ujerumani kwa kusoma Shahada ya Uzamivu, yaani Udaktari katika Fasihi za Kiafrika katika Lugha za Kiafrika.

Mwaka 1968, aliajiriwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ajira hiyo, ilimpa nafasi ya kuwa mwalimu katika shule ya msingi ya Kizimbani; iliyopo huko Wete - Pemba. Baada ya kufundisha kwa muda wa wiki mbili, alitaka uhamisho wa kwenda shule ya Sekondari ya Utaani, huko alifundisha somo la Kiswahili. Pia masomo mengine kama vile ni Hesabu, Baiolojia na Kemia alidumu hapo kwa muda wa miaka kama sita. Mwaka 1974, alifundisha Chuo cha Ualimu cha Nkuruma, akiwa mwalimu wa sayansi (Hisabati, Fizikia, na Kemia) na masomo ya sanaa (Jiografia na Kiswahili). Mwaka 1985 aliteuliwa rasmi na Raisi wa Zanzibar wa wakati huo alikuwa Mh. Idrisa Abdul Wakili. Raisi alimpa kuwa Mkurugenzi wa TAKILUKI. Aliishikilia nafasi hiyo kwa muda wa miaka miwili.

Mwaka 1987, alikwenda Kenya kuomba kazi katika Chuo Kikuu cha Moi mjini Eldoret. Katika chuo hicho, alikuwa mwenyekiti wa kwanza wa Idara ya Kiswahili. Baadaye, mwaka 1989 alifundisha Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi, kwa muda wa mwaka mmoja na nusu. Mwaka 1990, aliitwa Japan katika Chuo Kikuu cha Osaka kwa lengo la kufundisha. Huko alikotunukiwa Uprofesa. Mwaka 1997 aliitwa kufundisha Kiswahili Ujerumani katika Chuo Kikuu cha Bayreuth. Tangu alipotunukiwa uprofesa hadi mwaka 2010 alipostaafu kufanya kazi ni kama miaka 13. Kwa sasa ameajiriwa[5] kuwa mhadhiri wa muda katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Baada ya kushauriwa na Raisi wa Zanzibar Mh Dkt Ali Mohamed Shein.

[5] Kwa sasa ajira yangu ipo SUZA. Nasomesha wanafunzi wa MA na PhD katika taaluma ya Kiswahili. Nimeamua kutoa msaada wangu SUZA, kwani Mh Dkt Shein ametuita wataalamu wa fani mbalimbali. Ili tuwasaidie vijana wa Zanzibar kielimu. Ndipo kama mimi Mzanzibar na nimestaafu hivi karibuni kutoka Ujerumani. Nimeamua kutoa msaada na kulitii agizo la mtukufu raisi (Mazngumzo kati ya Prof Said Ahmed Mohamed na mtafiti yaliyofanyika tarehe 05/03/2015Mjini Zanzibar)

Maisha ya uandishi ya Said Ahmed Mohamed yalianza tangu akiwa na umri wa miaka minane. Amerithi kipawa cha ubunifu na kiuandishi wa kazi za fasihi, kwa mama yake mkuu aliyeitwa Bi Nyakanga. Bibi huyu alikuwa mwenye uwezo wa kuimba nyimbo za unyago na kuwa mtunzi mzuri wa fasihi simulizi, hasa hadithi na mashairi. Alipata kipaji kupitia madrasa kwa kuimba na kughani kasda za kumsifu Mtume ( s.a.w). Mwaka 1960, akiwa darasa la sita alitunga shairi lake la mwanzo lililoitwa “Nimfunge Ndege Gani Hata Nipate Salama”. Hali hii ilimsababisha andike mashairi mengi na kuyapeleka Sauti ya Tanzania Zanzibar, kwa sasa inaitwa ZBC Redio. Vilevile, alipokuwa akisoma Chuo cha Ualimu cha Nkuruma kilichopo Beit el Ras Zanzibar aliandika hadithi yake ya mwanzo aliyoiita “*Ndoa ya Wahindi na Wahindi*”. Hadithi hii ilipata kusomwa na idhaa ya Kiswahili ya BBC. Halikadhalika, hadithi hii inapatikana katika kitabu chake cha *Sadiki Ukipenda* ameipa jina la *Mapenzi ya Ugunduzi*.

Said Ahmed Mohamed alipata hamasa kubwa ya kukiendeleza kipaji chake cha utunzi na uandishi. Kipaji chake kilichochewa na Mohamed Abdullah na kikundi cha Bw. Abubakar, ambao walikuwa wanampa ushauri zaidi wa kuandika. Vilevile, alipata hamasa kubwa zaidi baada ya kitendo chake kizuri cha kuanza kuandika mashairi na kuyapeleka idhaa ya Kiswahili ya BBC huko Londan. Pia, idhaa ya Kiswahili ya DW iliyopo mji wa Born Ujerumani. Idhaa hizi mbili zilianzisha mashindano ya kuandika hadithi fupi. Kupitia nafasi hii Said Ahmed alipata bahati ya kushinda, na ndipo kituo cha BBC kilimpa pongezi kubwa kwa kumtia hamasa na moyo wa kuzidi kuandika kazi za fasihi. Aliweza kupata wazo la kuandika kazi yake ya mwanzo ya riwaya ya *Asali Chungu* (1977). Hii ni baada ya kuzisoma na kuhamasishwa na riwaya ya *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1976). Riwaya hizi zilitungwa na Mohamed Suleiman Mohamed.

Said Ahmed Mohamed ni mtunzi mahiri wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili. Pamoja na vitabu vingine ambavyo si vya fasihi. Vitabu vyake tunaweza kuvigawa katika makundi yafuatayo:

a) Kazi za Riwaya:

i. *Asali Chungu* (1978), Shungwaya, Nairobi.

ii. *Utengano* (1980), Longhorn, Nairobi

iii. *Dunia Mti Mkavu* (1980), Longhorn, Nairobi

iv. *Kiza Katika Nuru* (1988), Longhorn, Nairobi

v. *Tata za Asumini* (1990), Longhorn,Nairobi.

vi. *Babu Alipofufuka* (2001), Jomo Kenyata Foundation, Nairobi

vii. *Dunia Yao* (2006), Oxford University Press, Nairobi.

vii. *Nyuso za Mwanamke* (2010), Longhorn, Nairobi

b) Kazi za Tamthiliya:

i. *Pungwa* (1988), Longhorn, Nairobi.

ii. *Kivuli Kinaishi* (1990), Oxford University Press, Nairobi

iii. *Amezidi* (1995), East Africa Educational Ltd, Nairobi

iv. *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000), Oxford University Press, Nairobi

vi. *Posa za Bi Kisiwa* (2007), Longhorn, Nairobi.

c) Kazi za Ushairi:

i. *Sikate Tamaa* (1980),Longhorn, Nairobi

ii. *Kina Cha Maisha* (1984), Longhorn, Nairobi.

iii. *Jicho La Ndani* (2002), Longhorn, Nairobi

iv. *Nilipoanza Kusema na Mashairi Mengine* (2011) Longhorn, Nairobi.

d) Kazi za Hadithi Fupi:

i. *Si Shetani si Wazimu*

ii. *Mfuko Mtupu*

iii. *Sadiki Ukipenda*

iv. *Harusi ya Buldoza*

v. *Damu Nyeusi*

vi. *Kiti cha Moyoni*

vii. *Hapa na Pale*

e) Kazi za Vitabu vya Watoto

i. *Simulizi za Kibobu*

ii. *Masikini Bibiangu*

iii. *Kigari Changu na Chake*

f) Kazi za Vitabu vya Taaluma

i. *Vito vya Hekima, Simo na Maneno ya Mshangao* (1973), Longhorn, Nairobi

ii. *Misemo, Milio na Tashbihi* (1977), Longhorn, Nairobi

iii. *Kamusi ya Visawe* (1998), Hi- Tech Typsetters, Nairobi

## 1.3 Usuli wa Tatizo Ia Utafiti na Tamko la Utafiti

### 1.3.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Utanzia ni mbinu ambayo inatumiwa na baadhi ya waandishi wa fasihi kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Licha ya mbinu hii kuna mbinu nyingine zinazotumiwa na wasanii, kama zifuatazo: taharuki, ufutuhi, matumizi ya taswira, uchawi, ushirikina na uhalisiamazingaombwe, mwingiliano-matini,

matumizi ya ndoto, usayansi na matumizi ya kejeli (Khamis, 2007; Ponera, 2010; Senkoro, 2011; Mhilu na Wenzake, 2008).

Riwaya ni kazi ya sanaa ya kubuni. Ni maandishi ya nathari (ujazo) yanayosimulia hadithi ambayo kwa kawaida ina uzito, upana na urefu wa kutosha. Riwaya huwa na wahusika mbalimbali wenye tabia za aina nyingi; ina migogoro mingi; mikubwa na midogo ndani yake ( Msokile, 1992; Enyclopedia Britanica 1960; Matteru, 1976). Kuwapo kwa urari na usambamba baina ya fani na maudhui katika riwaya hurahisisha uelewaji wa ujumbe ambao mtunzi anaukusudia kuufikisha kwa hadhira. Uchunguzi wa fani ya riwaya (au kazi yoyote ile) huhusisha vipengele kadhaa. Vipengele hivyo ni kama muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wahusika na mandhari (Senkoro, 1982; Wamitila, 2003:190).

Katika riwaya, fani na maudhui ni vipengele vikuu vinavyoukamilisha na kuupa uhai ili iweze kuwa na mvuto kwa wasomaji wake. Senkoro (1982) anavyonukuliwa na Madumulla (2009:120-121) akikazia kwa kusema: “Fani na maudhui ni sura mbili za sarafu moja; na si rahisi wala sahihi kuzitenga na kuzieleza katika upweke, moja bila ya kuhusishwa na nyingine...”

Fani na maudhui ni vitu vinavyokamilishana, kuwiana na kuathiriana. Haiwezekani kwa mwandishi kuziwasilisha dhamira zake bila kutegemea fani. Fani ni jumla ya mbinu, ufundi, mtindo, wa vipengele vingine vinavyotumika kuwasilisha maudhui (Mhilu na wenzake, 2008:2). Maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi, iwe tamthiliya, shairi, wimbo au riwaya (Njogu na Chimerah, 1999). Mwandishi wa kazi yoyote ya fasihi huwa haandiki kazi yake kutokea katika ombwe, bali huwa na fikra mgando kwa kusaidiwa na matumizi ya fani ili yaweze kuibua maudhui (Madumulla,

2009). Ili wazo lifike kwa hadhira yake kwa kiasi akitakacho, ni wajibu wa hadhira ya kazi hiyo kujitahidi katika kuisoma na kuihakiki. Uwezo wa kufanya hivyo husababisha walengwa wa kazi ya fasihi kupata thamani halisi ya kazi ya mtunzi kadri alivyoweza na kulenga. (Wamitila, 2002).

Kihistoria, utanzia ni mbinu ya kifasihi inayotokana na mzizi wa utanzu mkongwe wa kazi za kifasihi ulioanzia katika maigizo, tamthiliya, ushairi na riwaya. Mzizi wake umetokana na majaribio ya kidemokrasia kutoka Ugiriki ya kale kati ya mwaka 500 Kabla ya Kristo (KK) ( Mulokozi, 1999; Cartwright, 2013). Katika maendeleo ya fasihi, mbinu hii imekuwa ikitumiwa na watunzi mbalimbali katika utanzu wa riwaya. Kwa lengo la kuyaunda matukio yenye ujumbe mzito unaowasilishwa kwa lugha inayonawiri, ili izindue hofu na huruma. Pia, maigizo hayo yaripue hisia za ndani kutoka katika nafsi za hadhira (Wafula na Njogu, 2007).

Dhana ya utanzia kama mbinu ya kibunulizi ina mfungamano mkubwa na tanzia. Tanzia ni majonzi, huzuni na masikitiko (Mohamed na Mohamed, 1998). Kutokana na tafsiri hii, dhana hii imepiga hatua mbele zaidi ya kumaanisha kuwa ni kifo au msiba pekee; kwa sasa humaanisha hata zile hisia zenye kumsababishia mtu kupata huzuni, masikitiko na majonzi. Tanzia na utanzia huwafanya wasomaji waingiwe na huzuni (Wamitila, 2002) kwa lengo la kuyasawiri matukio ambayo yanaibua uoga na huruma katika akili za mtazamaji/ hadhira ili kuitakasa au kufua hisia hizi (za uoga na huruma) kwa kutanua na kurekebisha huruma zao.

Katika karne ya kumi na tisa, baadhi ya waandishi wa riwaya walianza kuitumia mbinu ya utanzia katika kazi zao. Ikiwa na lengo la kuonyesha hisia zao katika mapambano ya upatikanaji wa fedha; ambazo zilibadilisha utu na tabia za wanajamii katika mfumo wa kibepari ulioshamiri wakati huo ( Benito, 1888; Thomas, 1901;

William, 1884; Giovanni, 1888). Katika karne ya 20, mbinu ya matumizi ya utanzia ilianza kutumiwa na baadhi ya waandishi wa riwaya wa kizungu. Kwa mfano Fyodor Dostoyvsky, Thomas Hardy, Joseph Courad na William Faulkner. Kwa upande wa waandishi wa Fasihi ya Kiswahili, walianza kuitumia mbinu hii katika kazi zao kama tamthiliya, ushairi na riwaya. Miongoni mwao ni Said Ahmed Mohamed.

Wahakiki na watafiti kadhaa wameyashughulikia maandiko ya Said Ahmed Mohamed, kwa kuvichunguza vipengele mbalimbali vya fani na maudhui. Kipengele cha matumizi ya mbinu ya utanzia kimechunguzwa kwa kiasi kidogo na baadhi ya wahakiki. Hali hii bado inaacha tatizo kwa hadhira katika kuelewa dhana ya utanzia. Hivyoi, kuna haja kubwa ya kuyashughulikia maandiko ya Said Ahmed Mohamed, ili kuyaweka wazi matumizi ya utanzia kwa kubainisha miktadha, matukio ya kitanzia na athari wazipatazo wasomaji.

### 1.3.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Wapo watafiti na wachunguzi wengi waliomchunguza Said Ahmed Mohamed. kifani na kimaudhui. Mathalani, kwa upande wa kipengele cha maudhui; kuna wataalamu kama Khaemba, (1999), Swalehe (1997), Mbatia (1997), Wamitila (2002), Madumulla (2009), na Ligopola (2012). Na kwa upande kipengele cha fani wataalamu kama vile Wanjiru (2013), Walibora (2010), Magaju (2004), Shilla (2012), Senkoro (2007), na Traore (2008). Licha ya wahakiki na waandishi hawa kuyashughulikia maandiko ya Said Ahmed Mohamed, bado pana haja ya kuyashughulikia zaidi maandiko yake. Hii ni kwa sababu wahakiki na watafiti wengi hawajakishughulikia kwa kina kipengele cha utanzia kama moja ya mbinu ya kibunulizi. Wachache walioichunguza mbinu ya utanzia kwa kumhusisha mwandishi Said Ahmed Mohamed ni Mlacha (1987), Nocera (2005), na Traore (2008). Kazi

kubwa iliyofanywa na wahakiki hawa ni kutaja kwa uchache tu baadhi ya matukio ya kitanzia. Hali hii imeibua tatizo kubwa kwa wasomaji, kuacha maswali ambayo yanahitaji majibu. Mosi, miktadha gani iliyojitokeza zaidi katika riwaya za Said Ahmed Mohamed kuhusiana na matumizi ya mbinu ya utanzia? Pili, kuna matukio gani ya kitanzia? Tatu, athari gani inayoweza kupatikana kwa wasomaji, inapojitokeza mbinu ya utanzia katika riwaya za Said Ahmed Mohamed?

Hiyo, utafiti huu ulifanyika ili upige hatua mbele zaidi kwa kuuchunguza utanzia katika bunulizi za Said Ahmed Mohamed huku tukijielekeza katika kujibu mianya iliyodokezwa hapo juu.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

### 1.4.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza matumizi ya mbinu ya utanzia katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya utafiti huu ni kama ifuatavyo:

a) Kuchunguza miktadha mbalimbali iliyotumiwa na Said Ahmed Mohamed katika kuibua matukio ya kitanzia katika ya riwaya zake.

b) Kuchambua matukio ya kitanzia yaliyomo katika riwaya za Said Ahmed Mohamed.

c) Kutathmini athari za matukio ya kitanzia katika riwaya za Said Ahmed Mohamed kwa wasomaji.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

a) Ni miktadha ipi iliyotumiwa na Said Ahmed Mohamed katika kuibua matukio ya kitanzia katika riwaya zake?

b) Ni matukio gani ya kitanzia yanayojitokeza katika riwaya za Said Ahmed Mohamed?

c) Matukio ya kitanzia katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed yanatoa athari gani kwa wasomaji?

## 1.6 Manufaa ya Utafiti

Wasomaji wa tasnifu hii wanatarajiwa kupata manufaa yafuatayo: Mosi, itawasaidia wasomi, watunzi, wahakiki pamoja na wanafunzi katika kuifahamu dhana ya utanzia katika uga wa fasihi. Pili, itatoa maarifa mapya kwa kuielewa tofauti iliyopo baina ya tanzia na utanzia. Tatu, itawahamasisha walimu na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari hasa wa fasihi, na wapenzi wa riwaya katika kuzisoma kazi za Said Ahmed Mohamed. Nne, itawachocheo wasomi katika kukipigia mbizi kipengele cha utanzia katika tafiti zijazo. Tano, itatumika kama rejea kuu katika tafiti nyingine zinazohusiana na mada hii husika.

## 1.7 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Hivyo, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake ulijifunga kwa kuzingatia nguzo za nadharia hii husika.

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni nadharia iliyoibuka kati ya miaka ya 1960 na 1970, ambapo waasisi wake ni Stanley Fish (1980), Jane Tompkins (1980), Wolfang Iser (1974/1978). Wengine ni Robert Jauss (1982), Norman Holland na Roland

Barthes. Msingi wa nadharia umejigeza katika kuiangalia athari anayoipata msomaji baada ya kuzisoma kazi za fasihi, kama vile riwaya, tamthiliya au na ushairi. Kazi ya fasihi iliyokamilika hapa inazingatia kuwa ni ile iliyoandikwa. Mtunzi wa kazi anazingatiwa kuwa amekufa na kumuachia nafasi ya uhai msomaji. Nafasi hiyo huachwa kwa msomaji ili aweze kuihakiki kwa namna alivyoifahamu matini ya kazi husika kwa mielekeo yake binafsi.

Kwa muda mrefu nafasi ya wasomaji katika kazi ya fasihi imepuuzwa. Ndipo nadharia hii ikaibuliwa ili kuitetea nafasi pamoja na majukumu ya wasomaji katika kazi andishi hasa riwaya. Wamitila (2002) anafafanua kuwa mwelemeo mkubwa wa nadharia hii umekuwa katika utanzu wa riwaya. Hili linatokana na ukweli kuwa tukio au tendo la usomaji linadhihirika na kubainika waziwazi katika riwaya; kuliko ilivyo katika hadithi fupi, shairi na mbazi. Kwa kuwa nadharia hii inajikita zaidi kwa kuwarejelea wasomaji, wahakiki wa nadharia hii wamewagawa wasomaji wa aina tatu ambao ni msomaji mwashiriwa, msomaji andikwa, na msomaji mlengwa. Mwashiriwa ni msomaji ambaye anafahamu msingi wa kazi hiyo ambayo ni sawa na mwandishi. Msomaji andikwa ni msomaji ambaye ana sifa zinazotambulika waziwazi katika matini au kazi husika. Msomaji mlengwa ni msomaji ambaye anapatikana na sifa za ndani au hata za nje ya kazi fulani (Wamitila, 2002).

Abrahams (1993) anaona kuwa chimbuko la nadharia hii limetokana na mambo mawili. Mosi, ni uzukaji wa mitaala ya mawasiliano iliyotegemezwa kwenye jadi ya kijamii na ambayo imetambua tofauti katika upokezi wa vipindi vya vyombo vya mawasiliano. Pili, kuwapo kwa mgongano mkubwa kati ya wasomaji wasio wasomi na walio wasomi. Jambo la msingi katika nadharia hii ni kumpa nafasi kubwa msomaji wa matini ya kifasihi na kuiondoa nafasi hiyo kwa mtunzi. Hii ikiwa na

maana msomaji hupewa uhai *"born"* na mtunzi hufikiriwa kuwa amekufa *"dead"* Athari inayotazamiwa ni ile ya maana ya matini *"textual meaning"* kuliko maana inayotokana na makusudio ya mtunzi *"authorial intention"*.Yafuatayo ni mawazo ya msingi ya nadharia hii:

a) Kuwapo kwa uwiano kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki.

b) Kila kazi ya fasihi iwe na maana kufuatana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia.

c) Kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine.

d) Msomaji hutumia vigezo kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa au hayafai.

Akiizungumzia nadharia hii, Adena Rosmarin (1991), ananukuliwa na Wafula na Njogu (2007:86), akisema:

> Kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika. Mchongaji wa kinyago hiki kisichokuwa kamili hujaribu kukikamilisha. Vivyo hivyo, msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au huidhalilisha kazi hiyo kwa usomaji wa kiholela.

Wataalamu wa nadharia hii wanaona kuwa ipo haja kwa msomaji kufanya uradidi mwingi katika usomaji wa matini; ili kuweza kubaini maana iliyofichwa na mtunzi. Wafula na Njogu (2007:87) wanashadidia kuwa matini inayomfumbia msomaji mafumbo humshurutisha msomaji kurudia kusoma matini mara nyingi ili aielewe. Kutokana na misingi hii, matukio ya aina mbalimbali ndani ya kazi fulani ya fasihi yanaweza kueleweka au kutoa athari inayotofautiana kutokana na msomaji mmoja na mwingine. Kutegemeana na mguso aupatao msomaji. Mathalani, msomaji fulani huweza kupata athari chanya na mwingine kupata athari hasi. Hii inategemea na

tajriba za maisha. Hoja hii inayakinishwa na Margareth Atwood (1982) ambaye anasema:

> Usomaji ni fanyiko na unakubadilisha. Huwezi kuwa mtu yule yule aliyekuwa kabla na baada ya kuisoma kazi fulani ya kifasihi.

Kulingana na nadharia hii, uelewaji wa maana kwa msomaji/wasomaji unamsababisha awe na mwelekeo mpya ndani na nje. Jinsi ya kukabiliana na mazingira yake ya kijamii, kiutamaduni na hata kisiasa. Fasihi haina jibu moja bali hutegemea upokezi wa mwitiko wa msomaji mmoja na mwingine.

Hivyo, katika tasnifu hii, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ilitumika katika kuhusisha na malengo yetu ya utafiti. Mosi, mkabala huu ulitumika katika kuchochea ufahamu wa riwaya zetu teule na kupata maana za matini. Pili, kuichunguza miktadha mbalimbali ya maisha ya mtunzi na kuihusisha na tajriba za maisha ya kawaida. Hii ni kwa sababu mwandishi hakutokea katika ombwe la maisha, bali anatokana na kukulia katika maisha ya ndani ya jamii. Tatu, tuliitumia katika kuyachunguza matukio ya kitanzia pamoja na athari zake. Hii ni kwa kutumia fikra zetu binafsi na zile za watafitiwa ili kupata ubainifu yakinifu. Kwa kuruhusu mijadala na masailiano kutoka katika makundi mbalimbali. Hii ni kwa kuzingatia nafasi adhimu aliyopewa msomaji.

## 1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza  matumizi ya utanzia katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed. Umehusisha riwaya tatu ambazo ni *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980) *na Kiza Katika Nuru* (1988). Kazi nyingine za mwandishi huyu kama vile tamthiliya, hadithi fupi na ushairi hazikutumika kama msingi wa kukusanyia data ila zimetumiwa kama njia ya kutolea ithibati na mifano ya jumla. Sababu kuu ya kuteuliwa kwa riwaya hizi ni: Mosi, hizi ni riwaya za mwanzo

mwanzo katika utunzi wa mwandishi zilizoanza kutumia mbinu mpya za Kiafrika na kuachana na kanuni au misingi ya kigeni. Pili, ni riwaya zilizosheheni matukio lukuki ya kitanzia ikilinganisha na riwaya nyingine za mwandishi Said Ahmed Mohamed.

### 1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura imezungumzia uhusiano uliopo kati ya dhana mbili ambazo ni tanzia na utanzia. Imefafanua kuwa tanzia hujikita katika masuala ya utendaji na utanzia inachukuliwa kuwa ni miongoni mwa mbinu za kibunulizi. Pia, tumetoa ufafanuzi kuhusu vijenzi na matokeo ya utanzia. Pamoja na hayo, tumeieleza historia fupi ya Said Ahmed Mohamed ambaye ndiye mlengwa mkuu wa utafiti wetu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imeelezea mapitio mbalimbali ya maandiko yanayohusiana na mada yetu ya utafiti. Maandiko yetu tumeyagawa katika makundi mawili ambayo ni maandiko mbalimbali kuhusu utanzia katika kazi za fasihi, na maandiko yanayozungumzia utanzia katika kazi za Said Ahmed Mohamed.

## 2.2 Maandiko Kuhusu Utanzia Katika Kazi za Fasihi

Soileau (2006) anatoa ufafanuzi kuhusiana na tofauti iliyopo kati ya tanzia na utanzia. Kama anavyosema:

> *It is common to point out a distinction between the words "tragedy" and the "tragic". "Tragedy" in such a discussion usually refers to the literary form of a work, normally a drama but here a novel, which presents an interpretation of the meaning of human life or suffering and arouses a particular emotional response. "Tragic" refers to particular way of looking at the world...that tragic is a form in literature as a cultural trait that can be spread by diffusion throughout the literary world to the point that becomes a common and shared way of interpreting certain aspects of our existence*
>
> Kuna tofauti ya wazi kati ya neno "tanzia" na "utanzia". Tanzia ni kazi ya fasihi hasa katika tamthiliya na kwa sasa inajitokeza katika riwaya, ambayo inatoa maana halisi ya maisha ya mwanadamu au mateso (anguko) pamoja na kuibua hisia fulani. Wakati "utanzia" ni namna fulani ya kuitazamia dunia...kwamba utanzia ni mbinu ya kisanaa inayoonesha tabia ya kitamaduni inayoenea katika dunia ya fasihi inayojulikana na kuhusiana na taratibu za maisha ya jamii (Tafsiri yetu).

Mawazo ya mtaalamu huyu yametoa msaada mkubwa wa kupata uelewa wa kuwapo kwa utofauti kati ya dhana ya tanzia na utanzia. Tanzia kwa mujibu wa mtaalamu huyu ni aina ya tamthiliya inayohusu masuala ya mateso. Suala la mateso hutoa hisia za kuhuzunisha kwa msomaji wa tamthiliya. Kwa upande wa

utanzia, imetupa mwanga wa kubaini kuwa ni mbinu inayotumika katika kazi za kifasihi. Ndipo imetupa msukumo mkubwa kwetu, kuona haja ya kuchunguza udhahiri wa Said Ahmed Mohamed kutumia mbinu hii katika kazi zake.

*Enyclopedia Britanica* (1911:888) inazungumzia kuhusu dhana ya tanzia inavyotumika katika tanzu nyingine.

> *Tragedy is a branch of drama that treates in serious and dignified style the sarrowful or terrible events encountered or caused by heroic individual. By extension the term may be applied to other literary works such as the novel. Although the word tragedy is often used loosely to describe any sort of disaster or misfortune, it more precisely refers to a work of art the probes with high seriosness questions concerning the role of man in the universe.*
>
> Tanzia ni utanzu wa tamthiliya unaoshughulikia matukio yenye mtindo wa kuhuzunisha au kuogofya kwa kukabiliwa (adui, hatari, matatizo) au kusababishwa na ushujaa wa mtu. Kwa upanuzi zaidi, kipengele hiki hutumiwa katika kazi nyingine za fasihi kama riwaya. Ingawa tanzia mara nyingi hutumiwa kwa kuachwa (huru) kueleza namna fulani ya maafa (msiba) au taabu (balaa). Kwa usahihi zaidi inamaanisha ni kazi ya sanaa inayochunguza jambo kwa undani pamoja na masuala yenye uzito kuhusiana na nafasi (ya muigizaji) katika ulimwengu. (Tafsiri yetui; halikadhalika, msisitizo wa kwenye mabano ni wetu).

Dondoo hii inakusudia kuonyesha kuwa mtindo wa kutumia tanzia hujitokeza katika utanzu wa riwaya. Dondoo linakosoa mawazo yaliyopo kuwa mtindo wa mwandishi wa kutumia tanzia, hujitokeza katika tamthiliya pekee. Bali kamusi imeweka wazi kuhusu uwezekano wa kuutumia tanzia katika riwaya. Hii imetuchochea katika kuzizamia kazi za riwaya za Said Ahmed Mohamed kwa kuzilandanisha na tanzia. Vilevile, Kamusi imetumurikia kwa kubaini hoja ya kwamba, matukio yenye kuogopesha ni sehemu ya yale ya kuhuzunisha.

Ponera (2010), anamnukuu Wamitila (2002:76 - 77) ambaye anasema:

> Utanzu huu ni mwepesi ulinganishwapo na tanzia. Lengo la kimsingi la futuhi ni kuchangamsha na huishia kwa namna ya kufurahisha. Lazima tukumbuke kwamba kusema futuhi

> inafurahisha haina maana kuwa dhamira yake haina uzito. Futuhi huweza kuwa na sifa zinazotofautiana, jambo ambalo hutumiwa kama kigezo cha kuainisha aina mbalimbali. Lakini, vyovyote iwavyo, futuhi hujikwepesha na masuala ya kuhuzunisha au kushtua. Athari ya futuhi au kuchekesha hutokana na matendo, mienendo ya wahusika na hitilafu au ila za kuingiliana kwa kiusemi.

Nukuu hii imetupa mwanga wa mambo matatu. Mosi, tanzia ni kinyume cha futuhi. Pili, tanzia ni utanzu mkongwe ulinganishwapo na futuhi. Tatu, lengo la futuhi ni kujikwepesha na masuala ya kuhuzunisha au kushtua. Msingi wa maelezo haya si kuzungumzia tanzia na futuhi. Jambo linalotoa imani ni kuwapo kwa matumizi ya kutoa hisia za kufurahisha na kuhuzunisha au kushtua katika uandishi wa kazi za fasihi. Katika kufurahisha, mbinu itumiwayo huitwa ufutuhi na katika kuhuzunisha, mbinu itumiwayo huitwa utanzia. Katika maandiko ya Said Ahmed Mohamed kuna swali linalojitokeza. Je kuna utumiaji wowote wa kutoa hisia za kuhuzunisha au kushtua kwa wasomaji?

John (h.t) amegusia dhana ya ujumi katika utanzia. Anafafanua kuwa utanzia haujitokezi katika ujumi. Anaendelea kutoa sababu kuwa ujumi unajikita zaidi katika mambo yenye kuleta furaha katika taswira ya uzuri. Akaendelea kusema zaidi kuwa muziki ndio huleta ujumi kwa kuwa unafurahisha ndani yake mbele ya muhusika. Ufafanuzi huu wa John ulimuongezea mtafiti umuhimu wa kukichunguza zaidi utanzia

Ponera (2014) anatoa ufafanuzi mzuri kuhusu uhusiano wa ufutuhi na utanzia. Anabainisha kuwa dhana hizi zinatokana na kisawe chake ambacho ni utanzi- futuhi. Anaendelea kudokeza kuwa dhana hizi zina uhusiano wa ki-uwili; yaani hali ya majonzi au masikitiko huwa na uwezo wa kuzua hali ya furaha kwa wanaofuatilia tukio hilo la majonzi. Pia, hali ya furaha huweza kuzua hali ya majonzi au masikitiko kwa mhusika mwenyewe au kwa wanaofuatilia. Zaidi, anabainisha kuwa utanzia na

ufutuhi huweza kutokea hata nje ya mazingira ya kifasihi. Kazi hii imetupa mwanga kuhusu kuathiriana kwa dhana hizi mbili.

Macha (2013) ameonyesha uwapo wa matumizi ya vilio na vicheko katika fasihi. Andiko linasema:

> Hali kadhalika, katika tendi huwa kuna maswaibu mbalimbali huibua hisia kwa wahusika ambazo zaweza kuwa na furaha au huzuni na kupelekea vilio au vicheko. Vicheko huwa vinaweza kuashiria mambo mengi katika jamii kama vile, furaha, kebehi au kejeli, mzaha au dharau. Kwa upande wa vilio navyo vyaweza kuashiria furaha, huzuni au majonzi, matatizo au mkosi, maumivu, uchungu na hasira.

Wazo liliopo hapa ni kuwa kilio kina mahusiano makubwa na utumiaji wa mbinu ya utanzia. Ikiwa na maana kilio ni moja ya alama ya kuwapo hali ya kutoleta furaha na badala yake kinakuwa ni kidokezo cha huzuni. Dhana hii ya kilio imetoa njia ya kuona umuhimu wa iwapo Said Ahmed Mohamed katika riwaya zake ametumia vilio au la. Vilevile imetuzidishia hoja faafu ya kukiona kipengele cha utanzia kuwa kina uwanja mpana wa kujumuisha hali ya maumivu, uchungu au hasira aipatayo mhusika ndani ya kazi ya fasihi, au msomaji/msikilizaji wa kazi ya fasihi.

Holman (1972) katika Mulokozi (1996), anaenda mbali zaidi ya Tempels[6] kwa kuitaja nchi ya Misri kama mfano bora unaonyesha ukomavu wa sanaa za Waafrika kabla ya ujio wa wakoloni. Mchunguzi huyu anadai kuwa kumbukumbu za kwanza za maigizo ya kitamthiliya zinapatikana Misri. Huko Misri ndipo michezo ya miviga iliyohusu kufa na kufufuka kwa Mungu wa Wanamisri aliyeitwa Osiris; iliyokuwa ikiigizwa kila mwaka katika miaka ya 2500 KK. Uchambuzi wa mtaalamu huyu umetupa ushahidi wa kuwapo kwa maigizo yanayohusiana na kufa. Kwa kawaida

[6] 1954 alichunguza maisha ya wabantu na kuandika kitabu cha Bantu Philosophy. Anazungumzia sanaa ya Mwafrika. Mwanafilosofia huyu anazungumzia kuwapo kwa sanaa madhubuti ya Kiafrika hata kabla ya ujio wa utawala wa kikoloni kwa za Kiafrika

matukio yenye kufungamana na kufa huweza kutoa hisia fulani kwa hadhira iliyopo kwa kupata huzuni.

Suleiman na Saluhaya (2012) katika kitabu chao cha *Nadharia na Tahakiki ya Fasihi*, wanasema:

> Katika baadhi ya makabila, watani au wajukuu hupaswa kufanya maigizo yanayohusiana na maisha na matendo na tabia ya marehemu. Maigizo hayo huwa kama mchezo wa kuigizwa na husaidia kuwapunguzia wafiwa huzuni yao, mbali na kutoa mafunzo kwa watu waliopo msibani. Kwa mfano kama marehemu alikuwa na tabia mbaya, basi maigizo hayo huipiga vita tabia hiyo kwa njia ya kejeli au dhihaka.

Dondoo hii, inatoa mwanga wa kuwapo kwa uhusiano wa fasihi na matumizi ya utanzia katika mazingira ya msibani inayoambatana na huzuni. Mfano mzuri unaotolewa na wataalamu hawa ni maigizo yenye kusheheni kejeli na dhihaka kwa lengo la kupunguza makali ya huzuni katika misiba ya jamii. Hata hivyo, hoja hii imetoa nafasi ya kuviona kejeli na dhihaka kuwa ni sehemu ya kujenga huzuni

Mkubwa (2012) amezungumzia utani katika mazishi na matanga. Anabainisha kuna utani unaofanywa na jamii ya Wapemba kwa kuonyesha tabia zilizofanywa na marehemu msibani. Anaendelea kubainisha kuwa lengo lake ni kupunguza huzuni zilizopo kwa wafiwa. Haya ni maigizo yanayoambatana na utani. Aghalabu, maigizo huenda sambamba na utani ambazo huleta uchangamfu kwa hadhira, ili iwe ni njia ya kupunguza huzuni wakati wa mazishi. Ufaafu wa kazi hii ilituimarisha kupata wazo la kihusisha fasihi simulizi na hisia za kuhuzunisha.

Masebo na Nyangwine (2000) wamegusia uwapo wa dhana ya huzuni, furaha na kichekesho katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. Wanadokeza kuwa fanani hutumia mwili wake mzima katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira (Wasikilizaji au wasomaji). Pamoja na maelezo haya, tunaafikiana na fikra zao kuwa fasihi ina

dhamira ya kuhuzunisha na kuchekesha. Fikra za wataalamu hawa zinatufaa kwa sababu kazi yetu inahusu mambo yanayotoa hisia za kuhuzunisha.

Jieikob (2012) ametaja sifa zinazojitokeza katika masimulizi yanayotumia mbinu ya utanzia. Ameweza kutubainishia sifa kama vile: uwapo wa kejeli, kukosekana kwa utambuzi, kutokuwa na siri, kuhuzunisha, mateso ya mtu, kupoteza, kifo na maombolezi. Maoni haya, yametupa hoja ya kuzinasibisha riwaya za Said Ahmed Mohamed na matumizi ya utanzia yaliyomo yanakwenda sambamba na sifa za utanzia uliomo katika masimulizi.

Soileau (k.h.j) alifanya utafiti kuhusu *"Money and Tragedy In The Nineteenth-Century Novel"* Kupitia tasnifu yake amegusia matumizi ya utanzia kwa kuchunguza mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na nafasi ya pesa katika jamii ya mfumo wa ubepari. Anaendelea kutoa wazo kuwa Wafanyabiashara au watawala wanavyowasilisha utawala wao kama kusudio la kuanguka. Mambo ambayo hujidhihirisha katika riwaya husika au anguko la masimulizi yaliyojidhihirisha katika riwaya. Mtaalamu huyu amechunguza matumizi ya utanzia katika riwaya. Upungufu wake unajitokeza katika mambo mawili. Mosi, amejikita zaidi katika riwaya zilizoandikwa katika karne ya kumi na tisa. Pili, amezichagua riwaya zilizoandikwa na Wazungu pekee. Utafiti huu umedhamiria kumchunguza Said Ahmed Mohamed ambaye ni Mswahili na huandika kazi zake katika jamii za Waswahili. Tunamtumia yeye ili tuone ni kwa namna gani ameyamudu matumizi ya utanzia kutoka katika muktadha inayoendana na waswahili katika kazi zake.

Senkoro (2011:71) amegusia uwapo wa matukio ya kitanzia yenye kusikitisha. Anafafanua kuwa matukio ya kitanzia hujitokeza katika fasihi simulizi na andishi. Kwa maoni yake, anazungumzia mtambaji anapokuwa na hadhira yake, huyatumia

matukio ya kitanzia ambayo husikitisha katika hali ya taharuki. Baadaye, mtambaji hutumia mbinu ya ucheshi ili hadhira yake ipumue kidogo kwa kutabasamu. Hii ni baada ya kutumia matukio ya kutisha au maelezo marefumarefu yenye kuwachosha wasikilizaji. Mawazo yake yanajenga hoja kwamba huzuni na ucheshi, hujitokeza ndani ya kazi moja ya fasihi. Kimsingi mbinu hizi hutumiwa na mwandishi katika hali ya kupokezana. Muda fulani mwandishi anawahuzunisha wasomaji, na muda mwingine huwafanya wawe na furaha.

Mzandi (2011: 58- 59) katika utafiti wake amezungumzia utani unaofanyika katika maeneo ya msibani. Msiba huo hufanyiwa marehemu ambaye ni kijana, ambaye huwa sawa na mzee. Anaendelea kutoa maoni kuwa hali hii hutokea kwa sababu huzuni ni kubwa mno na unyonge uliopita mpaka. Vilevile, anatudokeza kuwa kuondokewa na kijana wa kiume au msichana huwa ni pigo kwao. Kwa maana kwamba kifo chake kimeipa ugumu familia. Mchunguzi huyu ametoa wazo la utumiaji wa utani, ni njia au mtindo unaofanywa na jamii katika sanaa za maonyesho ili kuzipunguza huzuni na hisia za unyonge walizozipata wanajamii. Licha ya maoni yake ametuacha katika kigugumizi. Hii ni kukosa kujua ni athari gani walizozipata jamii kutokana na tukio hilo la unyonge na kuhuzunisha. Ndio maana tasnifu hii inahitaji kuangazia ni athari gani zinazoweza kuzuka kwa wasomaji endapo panatokea matukio ya kuhuzunisha.

Bastide (1978) alifanya utafiti katika jamii ya Wanegro wa Waafrika. Aligundua wanayo matambiko yanayohusu vifo na maombezi kwa wafu. Anadai kuwa katika jamii hiyo, hufanya matambiko wakati wa mazishi kwa lengo la kuwaombea marehemu. Mazishi hayo hufanyika wakati amekufa mwanamke. Washiriki wake huwa ni wanawake tu, wanaume hawashiriki isipokuwa mkuu wa sherehe na mpiga

ngoma. Baada ya sherehe hizo maiti hupelekwa kanisani. Ufafanuzi huo unataja suala la vifo vinavyoambatana na maombezi ya wafu, yanayoongozwa na mpiga ngoma. Ngoma ni sehemu ya sanaa za maonyesho katika fasihi simulizi. Kwa jumla mawazo haya yamepalilia uyakinifu wa kuwapo kwa huzuni zinazopunguzwa kwa sherehe za kijadi ndani ya fasihi simulizi.

Wamitila (2003) katika kamusi yake ya *Istilahi na Nadharia* anadokeza kuhusu dhana ya Ufumbuzi wa Kitanzia. Anafafanua dhana hii hutumiwa kuelezea ufumbuzi ambao una tukio la kusikitisha, aghalabu kifo cha nguli au mhusika mkuu wa utungo unaohusika. Maelezo haya, ni mafupi sana ila yanatupa faida ya kuamini uwapo wa matukio ya kitanzia yanayosababisha hadhira isikitike ndani ya kazi za kifasihi.

## 2.3 Maandiko Kuhusu Utanzia Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed

Waandishi mbalimbali wamejitokeza kumsifia mwandishi Said Ahmed Mohamed kuwa ni bingwa wa kutumia mbinu mbalimbali za kibunulizi katika nathari zake. Mbinu hizo huweza kuibua maudhui katika kazi zake. Mathalani, Vuorela (1987), Senkoro (2007), King'ei (2002) na Mbatia (1997). Madai hayo yametufanya tuamini baada ya kuyapitia baadhi ya maandiko ya wahakiki na wachambuzi walivyoifafanua mbinu ya utanzia katika maandiko yao.

Wafula na Njogu (2007) wamegusia kuwapo kwa wahusika wa kitanzia katika kazi za Said Ahmed Mohammed. Wahusika hao walihusishwa moja kwa moja na sanaa tendaji inayodunisha au ubwege. Hoja yao imejikita katika kipengele cha ubwege. Wataalamu hawa wameifafanua dhana ya ubwege kwa maana ya wahusika waliodunishwa kwa kuutawala ulimwengu uliokinai maadili ya kidini na mantiki ya kisayansi. Katika kuwatolea mfano wahusika wa kitanzia, walijifunga katika kazi

mbili za tamthiliya. Tamthiliya hizo ni za Sammuel Beckett na tamthiliya ya *Amezidi* (1995). ya Said Ahmed Mohamed.

Nocera (2005) katika makala yake aliyoiita *"An Interpretation of Said Ahmed Mohamed's Novel Kiza Katika Nuru And Some Aspects Of Translation"* amegusia kuhusu tukio la kitanzia katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Katika makala yake, amelitaja tukio la kitanzia kwa kutudokezea:

> *The tragedy is that Kudura after having freed her soul inside, becomes a prisoner outside. She will eventually die through suicide in jail, where she is locked up for the murder of Bwan Juba.*
>
> Kuna tukio la kitanzia, pale Kudura aliposingiziwa kumuua Bwana Juba, kutokana na jambo hilo alifungwa. Jambo ambalo lilimfanya awe mpweke na kuamua kujinyonga. (Tafsiri yetu).

Nukuu hii imetoa msaada katika kuthibitisha kuwapo kwa matukio ya kitanzia ndani ya kazi za Said Ahmed Mohamed. Ijapokuwa mchunguzi ameishia katika kulitaja tukio husika bila ya kutupa ufafanuzi kuhusu athari inayoweza kuchipuka kwa wasomaji. Imani yetu tukio kama hili na mingine ambayo hayakutajwa yana athari zake kwa wasomaji. Hivyo azma yetu ni kuyazamia matukio ya kitanzia kwa lengo la kuibua athari zake kwa wasomaji.

Traore (2008) katika makala yake inayoitwa "*Family and Society In Said Ahmed Mohamed's Novels".* Mtaalamu huyu amegusia kuwapo kwa simulizi ya hadithi ya kuhuzunisha katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*. Anasema, riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* inafungamana na mwenendo wa kijamii kupitia simulizi ya kuhuzunisha kwa kifo cha Mama yake Fumu. Maoni haya, yanachochea kutupa masuala mengi ya namna gani mwandishi ameweza kuyaweka matukio yenye kuleta hisia za huzuni kwa kunasibisha na kifo au vifo vya wahusika wake.

Mlacha (1987) anatoa ufafanuzi katika kazi yake aliyoiita "*The Identification of Personality Differences in Kiswahili Prose"* amegusia kuwapo kwa utanzia katika hali ya kujiua na mauaji *(Suicide, Murder)* akizitaja baadhi ya riwaya kama vile *Utengano, Shida, Rosa Mistika* na *Nyota ya Rehema* zina matumizi ya mauaji. Mtaalamu ameitaja *Utengano* kuwa ni sehemu ya riwaya iliyosheheni matukio ya kitanzia. Kinachotoa mwanga kwetu kutokana na mawazo ya mtaalamu ni kutuchochea kuhusu dhana ya mauaji au kujiua ni kwa namna gani inavyoweza kuibua huzuni kwa msomaji.

Wamitila (2002) anaonesha suala la mgogoro katika riwaya ya Said Ahmed Mohamed ya *Kiza Katika Nuru*. Anasema pana mgogoro wa kiitikadi kati ya Mvita na Bwan'Juba. Mgogoro huu unaishia kwenye vifo vya wahusika hao wawili. Mgogoro huo unatoa hali fulani kwa msomaji ya kupata hisia za masikitiko kwa kifo cha Mvita. Kifo hicho kimesababishwa na udhalimu wa Bwan Juba. Hapa Wamitila amefungamanisha kwa pamoja kati ya vifo na dhana ya kupatikana kwa masikitiko baada ya kutokea vifo.

Ligopola (2012) amefanya uchambuzi katika riwaya ya *Utengano.* Katika uchambuzi wake amelifafanua tukio lenye kuhuzunisha ambalo Bwana Maksuudi alipompiga mkewe Bi Tamima kwa kutumia ukanda. Mtafiti huyu anataja huzuni kubwa aliyoipata Bi Tamima kwa kutomjua mwanae Maimuna alipokwenda. Jambo hili lilitokea baada ya kutoroka nyumbani kwao bila ya kutoa taarifa yoyote. Licha ya maelezo ya mchambuzi huyu kwa kulitaja tukio hili lenye kuhuzunisha. Hoja tunayotaka kuibulia hapa ni kujua athari anayoweza kuipata msomaji katika tukio kama hili.

## 2.4 Mapengo Yanayojitokeza

Pamoja na wataalamu mbalimbali kuchambua maandiko ya Said Ahmed Mohamed. Bado kazi zao hizo zimeacha mapengo kadhaa kuhusiana na dhana ya utanzia. Mapengo hayo ni: Mosi, hakuna andiko hata moja lililojikita katika kuchunguza na kuchambua matumizi ya utanzia kwa kuhusisha na miktadha mbalimbali katika maisha ya Said Ahmed Mohamed. Pili, baadhi ya wataalamu wameyataja tu matukio ya kitanzia kwa ujumla wake, bila kuonyesha athari kwa wasomaji. Kwa hivyo, utafiti huu umekusudia kuziba mapengo yaliyojitokeza.

## 2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura imeyatalii maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada hii husika. Lengo letu ni kutaka kufahamu ni mambo gani yamezungumzwa na waandishi hao na yapi hayakuzungumziwa. Kuyatalii kwetu mapitio kadhaa kumesaidia kubaini mapengo ambayo yamejitokeza. Hivyo, mtafiti ameweza kupata mapengo yanayohitaji kuzibwa.

# SURA YA TATU

# MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua mpango wa jumla wa utafiti. Mambo mengine yanayohusika ni eneo la utafiti, jamii ya watafitiwa, zana na mbinu za kukusanyia data, mchakato wa kukusanya data na uchambuzi wa data.

## 3.2 Mpango wa Utafiti

Katika kufanikisha matokeo ya utafiti huu,tulitumia mkabala wa maktabani na uwandani. Data za maktabani na uwandani zimekusanywa kutoka katika maandiko mbalimbali yanayomhusu Said Ahmed Mohamed. Pamoja na yale yanayohusu mada husika ya utanzia na taarifa zinazotokana na riwaya tatu zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed. Taarifa za uwandani zimekusanywa kwa kutumia njia ya mahojiano ya ana kwa ana, majadiliano ya makundi mbalimbali na dodoso zilizosambazwa kwa watu maalumu walioteuliwa. Mbinu ya kimaelezo ndio iliyotumika pekee. Imetumika kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa data mbalimbali zilizokusanywa, kuhakikiwa na kuchambuliwa kwa kina; ili kufanikisha malengo yetu ya utafiti. Kothari (2009:33-34) anavyoshadidia kuwa mkabala usiokuwa wa kiidadi unaleta na kuzalisha matokeo yasiyoonyesha idadi au kiasi na unalenga kutoa maelezo zaidi.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Kusini Unguja, Dar es Salaam na Dodoma. Maeneo ya mikoa miwili kutoka Zanzibar, yametusaidia katika kukusanya data za maktabani na uwandani. Mkoa wa Mjini Magharibi

umesaidia kupata data kupitia maktaba kuu ya Zanzibar, shule teule za sekondari zinazojumuisha waalimu na wanafunzi wa somo la Kiswahili, Taasisi za Kiswahili kama BAKIZA na TAKILUKI pamoja na Chuo Kikuu cha Abdul- Rahman al Sumait Memorial University. Mkoa wa Kusini Unguja umeteuliwa kwa sababu mnapatikana maktaba, wanafunzi na wataalamu lukuki wa somo la Kiswahili. Mkoa huu umetuwezesha kukitembelea Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo Kikuu cha Zanzibar. Kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma, imetusaidia kupata data za maktabani tu. Katika mikoa hiyo tuliweza kuitembelea maktaba kuu ya Taifa na maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vilevile maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma tuliweza kuzitalii tasnifu mbalimbali zinazohusiana na taaluma ya Fasihi ya jumla na Fasihi ya Kiswahili.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu wamegawanywa katika makundi mawili ambayo ni jamii ya watafitiwa na sampuli ya watafitiwa.

#### 3.4.1 Jamii ya Watafitiwa

Jamii ya watafitiwa ni jumla ya vitu vyote ambavyo mtafiti anaweza kuvitumia kwa ajili ya kupata taarifa za utafiti. Jamii iliyokusudiwa katika kupata taarifa za utafiti huu, ilijumuisha makundi muhimu yafuatayo:

a) Riwaya teule zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed.

b) Wataalamu wabobevu waliofanya utafiti, uchambuzi na kuzihakiki kazi mbalimbali za Said Ahmed Mohamed. Wataalamu hawa walisailiwa ili kutupa fikra za kitaaluma kuhusiana na mbinu ya kibunulizi ya utanzia pamoja na uandishi wa Said Ahmed Mohamed.

c) Wanafunzi mbalimbali wa somo la fasihi. Wanafunzi hawa tuliwahoji ili waweze kutupatia mawazo kuhusiana na matukio ya kitanzia na athari wazipatazo wasomaji.

d) Watu wa karibu wanaomfahamu mwandishi Said Ahmed Mohamed. Kundi hili linajumuisha ndugu, marafiki wanayoyafahamu maisha halisi ya mwandishi. Watu hawa tumewahoji ili kutupa taarifa sahihi ya maisha ya Said Ahmed Mohamed.

### 3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji Wake

Utafiti huu ulitumia sampuli[7] ambapo mtafiti alifanya uteuzi wa kiholela kulingana na vigezo na sifa faafu za wawakilishi wetu. Sampuli imetusaidia kwenda sambamba na malengo yetu ya utafiti. Mtafiti amezichagua sampuli zenye kujumuisha makundi yafuatayo:

a) Riwaya tatu zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed. Riwaya hizo ni *Kiza Katika Nuru* (1988), *Utengano* (1980) na *Dunia Mti Mkavu* (2002). Sababu kubwa ya kuziteua riwaya hizi, ni ile silka ya kuwa na matukio mingi ya kitanzia kuliko riwaya nyingine za Said Ahmed Mohamed.

b) Wanafunzi 25 wa kidato cha tano na sita. Wanafunzi wameteuliwa katika shule za sekondari za binafsi na serikali. Uteuzi wao umezingatia jinsi ya kike na kiume. Ambapo wanafunzi 13 walikuwa ni wanaume na wanafunzi 12 ni wanawake. Mbinu iliyotumika ni uteuzi wa bahati nasibu, ili kuwafanya washiriki kupata nafasi sawa ya ushiriki wao.

c) Wanafunzi 20 wa elimu ya juu katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Kundi hili lilijumuisha wanafunzi 10 kutoka SUZA,wanafunzi 5 kutoka ZU na

[7] Ni sehemu ya idadi ya watu au vitu ambavyo mtafiti anaitumia kukusanya taarifa au data zitakazosaidia kufanikisha malengo ya utafiti (Babbie 1992)

wanafunzi 5 kutoka SUMAIT University. Kategoria hii imezingatia jinsi na kiwango cha elimu.

d) Wataalamu 10 waliozihakiki kazi mbalimbali za Said Ahmed Mohamed. Kundi hili limeteuliwa kupitia sampuli lengwa[8] Mtafiti amechagua wawakilishi hao kwa lengo la kukidhi haja na makusudio ya utafiti.

e) Wakazi 5 wa maeneo ya Unguja Mjini. Kategoria hii iliteuliwa kupitia sampuli lengwa ambayo imetuwezesha kupata taarifa za historia na mwenendo mzima wa maisha ya Said Ahmed Mohamed.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inaelezea njia au mbinu[9] na zana mbalimbali za ukusanyaji wa data, na utaratibu kuhusu mchakato wa ukusanyaji wa data.

### 3.5.1 Mbinu na Zana za Kukusanyia Data

Mbinu zilizotumika kukusanyia data za utafiti huu ni udurusu wa kimaktaba, mahojiano, udodosaji na majadiliano ya makundi mbalimbali. Njia hizi zilisaidiwa na zana kama vile: mwongozo wa hojaji, mwongozo wa dodoso, mwongozo wa udurusu wa kimaktaba na mwongozo wa majadiliano. Zana nyingine ni kompyuta, kalamu na karatasi, simu ya mkononi na vijidaftari.

### 3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake

Maadili ya utafiti[10] yalizingatiwa katika utafiti huu. Mtafiti aliomba barua ya ruhusa ya kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Alipeleka barua ya ruhusa ya

---

[8] Ni sehemu ndogo ya jamii ya watafitiwa ambayo huchaguliwa na mtafiti itumike katika utafiti wake kwa sababu tu ya kuwa na sifa za kukidhi mahitaji ya utafiti (Ponera, 2010).

[9] Best na Kahn (1983) wanasema kila mbinu ya kukusanyia data ina ubora na changamoto zake. Njia moja wapo ya kupunguza changamoto na kuongeza ubora ni kutumia mbinu zaidi ya moja katika utafiti

[10] Ni misingi ambayo mtafiti anapaswa kuizingatia wakati wa kufanya utafiti (Kumary, 1999)

utafiti katika taasisi na watu binafsi na kupata ridhaa. Mtafiti alitunza taarifa za siri, kuficha majina kwa watoa taarifa. Data za maktabani zilikusanywa kwa kutumia udurusu wa kimaktaba na wovuti. Aliyadurusu majarida, vitabu, tasnifu, makala mbalimbali zinazohusiana na mada husika.

Data za uwandani zilikusanywa kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana na dodoso. Mwongozo wa hojaji ulitumika kwa kumuhoji Saidi Ahmed Mohamed na wabobevu wa taaluma ya fasihi pamoja na watu wa karibu wanaomfahamu Said Ahmed Mohamed. Dodoso ilitumika kwa ajili ya kuwadodosa wanafunzi wa vyuo vikuu na shule za sekondari. Mtafiti aliteua makundi maalum ya wanafunzi ili kudadisi kuhusiana na mada ya utanzia.

Zana kama vile kamera zilitumika ili kuzihifadhi taarifa zinazotolewa na wahojiwa pamoja na kupiga picha vyanzo vya taarifa zilizopatikana kuhusiana na mada husika. Vilevile, kalamu, madaftari na kompyuta zilitumiwa ili kutunza taarifa zilizotolewa na watafitiwa; pamoja na taarifa zilizopatikana kupitia udurusu wa maandiko mbalimbali ya vitabuni.

### 3.6 Uchambuzi na Uunganishaji wa Data

Uchambuzi wa data za utafiti huu umezingatia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Data zimechambuliwa na kupangwa kulingana na malengo yetu matatu ya utafiti. Kila lengo limeundwa katika sura ya nne ambapo kila lengo moja lina maudhui yanayolandana na mada husika. Pia, katika uchambuzi wa data mbinu ya ufafanuzi imetumiwa kwa sababu utafiti huu hauna mfungamano wa moja kwa moja na ufafanuzi wa kitakwimu. Hivyo, sehemu yote ya utafiti huu ni wa maelezo tu.

### 3.7 Vikwazo vya Utafiti

Licha ya kukamilika kwa utafiti huu, mtafiti kwa namna moja au nyingine aliweza kukabiliana na matatizo lukuki. Miongoni mwa matatizo hayo ni kama ifuatavyo: Kwanza, upungufu wa fedha. Asilimia kubwa ya utafiti ulihitaji fedha za kutosha. Upungufu huo umetokana na kutegemea chanzo kimoja tu ambacho ni mshahara wa mwisho wa mwezi. Mtafiti alikwazwa katika ukusanyaji wa data, uchapishaji wa tasnifu, gharama za nauli za kusafiri, malazi pamoja na vyakula. Hali hii ilisababisha kuchelewa kukamilika kwa tasnifu. Pili, watafitiwa wengi hasa wanafunzi wamekuwa na uduni wa kuvisoma vitabu vya Said Ahmed Mohamed. Wengi wao walikisoma kitabu kimoja tu cha *Kivuli Kinaishi*. Hii ni kwa sababu kinafanyiwa mtihani wa kidato cha tano na sita. Hivyo, wengi wao waliomba muda wa kutosha kwa lengo la kupata nafasi ya kuvisoma vitabu teule vya mwandishi. Tatu, baadhi ya watafitiwa hawakuwa na utayari wa kutoa ushirikiano kwa mtafiti. Hali hii ilisababisha kutumia jitihada zaidi za ushawishi wa kihekima na busara; ndipo watafitiwa wakawa na utayari wa kutoa taarifa. Nne, Urasimu katika taasisi mbalimbali za serekalini. Taasisi hizo kwa kiasi fulani zilikuwa na usumbufu katika mchakato mzima wa utafiti. Usumbufu ulianza tangu hatua ya kuomba vibali vya kuruhusiwa kufanya utafiti hadi ukusanyaji wa data. Wengi wa wahojiwa kupitia taasisi hizo walitupa shida ya kuonana nao baada ya kuwekeana miadi iliyo rasmi.

### 3.8 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura ilianza kuonyesha mpango wetu wa utafiti. Tuliitumia mikabala miwili ambayo ni ya maktabani na uwandani. Katika ufafanuzi wa data njia ya maelezo ilitumika. Pia, tumezibainisha mbinu na zana za utafiti pamoja na maeneo teule ambayo ni mkoa wa Mjini Magharibi, Kusini Unguja, Dar es Salaam na Dodoma. Mwisho,

tulihitimisha kwa kutaja baadhi za changamoto tulizokabiliana nazo katika mchakato mzima wa utafiti.

## SURA YA NNE

## UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti. Sura imegawanyika katika sehemu kuu tatu zinazolandana na maswali yetu ya utafiti. Sehemu ya kwanza inaeleza miktadha mbalimbali aliyokutana nayo Said Ahmed Mohamed katika maisha yake. Sehemu ya pili inafafanua matukio ya kitanzia yanavyojitokeza katika riwaya tatu teule za mwandishi. Sehemu ya tatu imechambua athari chanya na hasi wazipatazo wasomaji kutokana na matukio ya kitanzia.

### 4.2 Miktadha ya Maisha ya Said Ahmed Mohamed

Sehemu hii inahusu ubainishaji wa maisha ya mtunzi yanavyolandana na matumizi ya utanzia ndani ya kazi zake. Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) neno muktadha lina maana ya hali, wakati jambo linapofanyika au panapohusika. Kutokana na fasili hii, utafiti umeichukulia dhana ya muktadha katika mazingira mbalimbali aliyokulia mtunzi tukihusisha na utunzi wake.

#### 4.2.1 Said Ahmed Mohamed na Mfumo wa Dini

Kimsingi Said Ahmed Mohamed ni mfuasi wa dini ya Uislamu. Uislamu ni dini ambayo msingi wake ni Kurani Tukufu na inayoamini uwapo wa Mungu mmoja anayepaswa kuabudiwa kwa kuyatii maagizo yake na kuyaacha makatazo yake. Na inaamini kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) ni mjumbe wake wa mwisho (*Kamusi ya Karne ya 21*, 2011). Kama ilivyodokezwa katika historia yake fupi kwamba mwandishi alipata bahati ya kusoma madrasa. Elimu ya madrasa ilimweka katika werevu wa kumtambua Muumba wake pamoja na Mtume wake Muhammad (s.aw).

Msingi mkuu katika elimu hii ilimweka katika maadili mema na kujiepusha na kutenda matendo mabaya.

Said Ahmed Mohamed amezaliwa katika jamii ya watu wenye imani ya dini ya Kiislamu, na kukulia katika malezi ya Kiislamu katika eneo la Unguja Mjini, amabalo ndilo aliloishi tangu utotoni. Eneo hilo limetamalaki na desturi za dini ya Kiislamu. Alijikuta ameingiwa na imani hii taratibu tangu maisha yake ya utotoni hadi ukubwani. Suala la dini ni miongoni mwa hoja iliyomshughulisha katika kazi zake. Wazo kubwa alilojikita nalo ni pale ambapo watu kuichukulia dini kama sehemu ya kujifichia maovu. Analifafanua hili katika kazi yake ya *Kiza Katika Nuru*.

> Baada ya dakika za dua na nyuradi na dua, Shehe Juba aligeukia umma wa watu aliokuwa kwa muda wote huo ameupa mgongo. Uso wake ulikuwa mkavu, ingawa ulikuwa mbivu, umeiva na kuvimba. Uso huo haukuwa na hisia yoyote, hofu wala woga. Ile kovu au sijida usoni ilionekana nyeusi zaidi kwenye anga la kandili, taa pekee iliyokuwepo hapo. Mvita aliwaza ‘ Wanasema, laiti nyoyo za wanadamu zingeonekana, zingekutwa zimejaa fedheha. Ukweli ulioje! Bila shaka ndani ya nafsi yake Bwan Juba alijijua jinsi alivyo mchafu wa matendo. Damu yake imeshiba nguvu za watu wengine na tumbo, au matumbo yake, yamefura kwa kula visivyopasa kuliwa. Lakini yeye anajihakikishia kwamba hapana anayemjua zaidi ya wale wanaomjua au wanaopasa kumjua. . . ( uk 183-184).

Kupitia nukuu hii, Said Ahmed anaidhihirishia jamii namna ya viongozi wanavyoichukulia dini kama mtaji wa kuyatekeleza mabaya yaliyofichama moyoni mwao. Anaamini kuwa dini si nyenzo ya kuichukulia kama chombo cha kutendea madhambi kama wafanyavyo baadhi ya watu wanaojiita waislamu. Anatubainishia suala hili kwa kusema.

> Kazi zangu nyingi zikiwemo riwaya, mashairi, na tamhtiliya huwa nakipachika kipengele cha dini ili kuonyesha ukweli na namna ya watu waovu wanavyoichukilia dini hii adhimu[11]

[11] Mazungumzo binafsi kati ya mtafiti na Prof. Said Ahmed Mohamed yaliyofanyika tarehe 07/03/2015 mjini Zanzibar

Mawazo haya tunayalandanisha pamoja na yale yaliyomo katika shairi lake aliloliita *Simwabudu Mtu* lililomo katika bunulizi yake iitwayo *Jicho la Ndani*. Said Ahmed anathibitisha kwa kusema:

Tazameni ikhwani msijeje
Wan' osujudu insani niw'e teje?
Ni bora ya hayawani wa duni je?
Simwabudu mtu ( uk 42 )

Hapa anatuchorea taswira muhimu ya jinsi dini isivyohitaji kuchukuliwa katika mtazamo hasi pale ambapo waumini wanapofanya maovu. Ndipo anapomchukulia mtu mwenye kutamalakiwa na dini kuwa kama hayawani. Ama anawakejeli viongozi na wafuasi kwa mienendo yao inayopingana na mafundisho ya dini. Mathalani, katika kazi yake ya *Utengano* amelisawiri jambo hili kwa Bwana Maksuud ambaye alivaa joho la Uislamu kwa lengo la kuficha vitendo vyake viovu. Miongoni mwa vitendo hivyo ni kutembea na wanawake nje ya ndoa yake huku akisingizia anakwenda kwenye dhikri au kuwaombea dua wazee wake makaburini.

Kwa ujumla, katika maelezo na mifano hii inajenga ukweli wa Said Ahmed Mohamed kuwa ni mwandishi aliye na kipaji kikubwa cha kuitumia sanaa katika bunulizi zake ikiwemo utanzia katika kuihoji na kuihakiki jamii yake.

### 4.2.2 Said Ahmed Mohamed na Lugha ya Kiswahili

Historia ya Kiswahili imeanza takriban miaka 1000 iliyopita katika pwani ya Afrika Mashariki. Neno Swahili lina asili ya lugha ya Kiarabu *'Sahl'* umoja au '*Swahil'* wingi likiwa na maana ya upwa au pwani. Hii ikimaanisha Waswahili ni watu wenye utamaduni wao, katika eneo la pwani ya mwambao wa Afrika Mashariki. Maeneo haya yanajumuisha Unguja, Pemba, Lamu, Pate, Bagamoyo Kilwa, Somalia, Mombasa (Chiraghdin, 1977)

Lugha anayoitumia Said Ahmed Mohamed ni Kiswahili Sanifu, yaani ni lahaja ya Kiunguja Mjini. Wenyeji wa mwambao wanaamini Kiswahili safi ni kile cha lahaja hii. Said Ahmed ameipata athari kubwa katika lugha hii ambayo ilimfanya awe mahiri katika utunzi wa vitabu vyake mbalimbali. Lugha hii ndio aliyojifunza tangu akiwa mtoto. Ipo hoja inayoaminika kuwa asilimia kubwa ya maneno ya lugha ya Kiswahili inatokana na lugha ya Kiarabu. Upo uhusiano wa wazi kati ya Said Ahmed na utambuzi wa lugha ya Kiarabu. Uhusianao huo unaturejesha wakati alipokuwa madrasa ambapo alijifunza lugha ya Kiarabu kupitia Kurani tukufu, Hadithi za Mtume pamoja na maulidi ya barazanje zilifundishwa kwa lugha ya Kiarabu. Hii ikiwa na maana ni lugha yake ya kwanza kujifunza, kukulia, kufundishia na kufanyia kazi.

Nguzo muhimu ambayo Said Ahmed anaamini kuwa Kiswahili ndio nyenzo ya mawasiliano katika mazingira ya Waswahili. Anaona kuwa kutoitumia lugha hii ujumbe wake utakuwa haufiki kwa hadhira yake. Ndio maana upo uhusiano kati ya lugha yake na maudhui kama ilivyo lugha ni moja kati ya mbinu za kifani yenye kufikiksha ujumbe maalum.

Said Ahmed anaifahamu lugha hii kwa namna ambayo imejidhihirisha katika kazi zake mbalimbali za kibunulizi na zile ambazo si za kibunulizi. Kwa mfano yeye mwenyewe anatupa ithibati kwa kusema:

> Mimi ninajivunia zaidi kuitumia lugha yangu ya Kiswahili kuliko lugha za kigeni na ndio maana kazi zangu nyingi nimeziandika kwa lugha yangu ya Kiswahili ili niisawiri jamii yangu[12].

[12] Mazungumzo binafsi kati ya mtafiti na Prof. Said Ahmed Mohamed yaliyofanyika tarehe 05/03/2015

Hali kadhalika, tunaweza kumuona Said Ahmed Mohamed jinsi alivyojitahidi kuitumia lugha ya Kiswahili kupitia kazi zake mbalimbali. Humo, ametumia ustadi mkubwa katika matumizi ya lugha. Mathalani, ametumia tamathali za semi mbalimbali kama vile tash-biha, sitiari, tash-hisi na mubalagha. Vilevile, ametumia kejeli, methali, nahau, misemo na mafumbo kwa ufundi wa hali ya juu. Hali hiyo inaonyesha namna mtunzi alivyo na utayari wa kukienzi na kukitukuza Kiswahili. Yumkini, juhudi hizo zinatupa ithibati kuwa hali hii inampa nafasi mtunzi ya kuijadili hadhira yake kijamii, kisiasa na kiuchumi huku akiziteka hisia za wasomaji wake kwa kuingiza mbinu ya utanzia ili kufanikisha madhumunu hayo.

### 4.2.3 Said Ahmed Mohamed na Taaluma

Kielimu, Said Ahmed Mohamed alibahatika kusoma wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Wakati wa ukoloni ni kile kipindi cha utawala wa Waarabu uliokuwa chini ya Uingereza. Baada ya ukoloni ni kipindi cha baada ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Said Ahmed alikuwa na hamu na shauku ya kutafuta elimu tangu akiwa mtoto. Ukweli wa jambo hili umeonekana tangu akiwa madrasa ambapo huko alijifunza elimu ya dini yake ya Kiislamu ikiwemo lugha ya Kiarabu, sira, hadithi za Mtume Muhammad (s.a.w) na kughani kasida. Ithibati hii inapatikana kwa maneno yake mwenyewe kama asemavyo:

> Uwezo wangu wa kiutunzi unaanzia pale nilipokuwa madrasa. Kwani nilipata maarifa ya kusoma kasda za mtume kwa kughani baada ya kufundishwa na mwalimu wetu kwa wakati ule[13]

Alitambuliwa na hadhira kwa mara ya kwanza kupitia riwaya yake ya *Asali Chungu*. Riwaya hiyo aliitunga mwaka 1977 akiwa ni mwanafunzi wa mwaka wa kwanza

[13] Ni mazungumzo binafsi kati ya mtafiti na Prof. Said Ahmed Mohamed yaliyofanyika tarehe 20/04/2015 Mjini Zanzibar.

katika Shahada ya Isimu. Jambo hili lilisaidiwa na uzoefu kutokana na elimu yake na kuzisoma kazi za baadhi ya wandishi waliomtangulia.

Pia, Said Ahmed anaonekana katika kazi tatu nyingine ambazo ni *Utengano*, *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru.* Humo ametumia ujuzi mkubwa ikilinganishwa na kazi yake ya awali. Anaonekana zaidi katika vipengele mbalimbali vya kifani na maudhui. Hebu tukichukulie kipengele cha lugha hasa katika uwekaji wake wa maneno mapya na magumu. Mathalani, katika riwaya ya *Utengano* kuna maneno kama vile tadhrubu, ugoni, kibahaluli, mkareti na sneri. Kwa hakika, utumiaji wa maneno kama haya ni kuonyesha weledi mkubwa wa mwandishi inavyoshabihiana na upeo wake wa elimu.

Said Ahmed Mohamed anaonekana kuwa na msisitizo wa kuitaka jamii yake iwe karibu na kuipenda elimu. Msisitizo huo unajitokeza katika baadhi ya bunulizi zake kama ile ya *Kiza Katika Nuru*, *Utengano* na *Dunia Mti Mkavu*. Humo tunawaona baadhi ya wahusika wake wakiwa na hamu na shauku ya kutafuta elimu. Mfano mzuri ni ule wa mhusika wake Mvita ambaye alipata elimu ya ngazi ya juu katika nchi za ulaya iliyomsaidia kutoa mwangaza kwa jamii yake hata wakajikomboa kutokana na dimbwi la ujinga waliokuwa nao. Ujinga wao ni kutoyapinga yale matendo mabaya yaliyokuwa yakitekelezwa na viongozi wao. Ujio wa Mvita uliosaidiwa na elimu yake ilikuwa ni silaha kubwa ya kuikomboa jamii yake. Katika mazingira kama haya, tunamchukulia Said Ahmed kuwa anaitumia elimu yake aliyoipata tangu madrasa hadi elimu ngazi ya juu ( Shahada ya kwanza, pili na tatu) kwa lengo la kuimurika jamii yake katika masuala mbalimbali ya maisha iwe kiuchumi, kisiasa na hata kijamii.

Kwa maoni yetu, hili ndilo wazo kuu lililoitawala akili ya Said Ahmed Mohamed kuhusu elimu. Aliamini kuwa elimu ni nyenzo inayofaa kutumiwa katika mapambano yote katika maisha. Hivyo, alitaka kila mtu awe katika harakati za kuisaka elimu huku akisisitiza kuwa elimu bora ni ile inayomwezesha mtu kujikomboa yeye mwenyewe na jamii nzima.

### 4.2.4 Said Ahmed Mohamed na Uandishi wa Zama Hizi

Uandishi wa Said Ahmed ulianza katika miaka ya 1970 ulioambatana na misingi ya kiuandishi ya kidemokrasia na kimsaragambwe. Uandishi wa kidemokrasia ulijikita katika sifa lukuki ambazo ni kwenda sambamba na kustawi kwa misingi ya kilimbwende, uandishi ulikiuka misingi ya sanaa ya kikanuni, ujumi wake ulijikita zaidi katika mwelekeo wa upokezi wa kazi yenyewe na kuibuka kwa mlipuko wa mielekeo tofauti ya kiuandishi. Sifa bainifu katika uandishi wa kimsaragambwe ni pamoja na kuakisi uhalisia wa maisha ambao kwa wakati huu maisha hayakuwa katika namna nyoofu bali ni ya changamani hivyo waandisi nao walijikita katika kutunga kazi zao kiuchangamani. (Mwamzandi 2013; Khamis, 2003; Bertonice, 1989)

Ni wakati huu ndipo waandishi mbalimbali akiwemo Said Ahmed Mohamed walivyoanza kuingiza mbinu mpya katika fasihi. Miongoni mwa mbinu hizo ni kama vile mwingiliano matini, ufantasia, usayansi, uhalisia mazingaombwe (usihiri), ufutuhi na utanzia pamoja na ushughulikiaji wa matatizo ya kidunia. Mathalani, Said Ahmed aliibuka na bunulizi zilizobeba umazing’aombwe. Hizi ni kama vile riwaya ya *Babu Alipofufuka* na tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* inayomsawiri Bikirembwe anapotumia uchawi, kuwaloga wanaginingi na kuwafanya mazuzu kiasi cha kuamini rangi nyeupe ni nyeusi na nyeusi ni nyeupe.

Tasnifu hii inaamini kuwa, yumkini, hata matumizi ya utanzia ni sehemu tu ya matokeo yenye mwelekeo huu wa uandishi ambao Said Ahmed Mohamed aliugeukia katika kuimurika jamii yake

### 4.2.5 Said Ahmed Mohamed na Mfumo wa Kisiasa

Said Ahmed Mohamed alishuhudia siasa tangu kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni. Yaani kipindi cha Waarabu na Waingireza. Akiwa chini ya utawala wa kikoloni, aliyafahamu madhila na manyanyaso mbalimbali ya watawala hao dhidi ya Waafrika. Hapa alishuhudia jinsi Waafrika wazalendo walivyoonesha upinzani dhidi ya serikali za wakoloni. Kipindi hicho walikabiliwa na matatizo kadhaa ambayo kwa namna moja ama nyingine yaliyoondoa utu wao. Kuthibitsha hilo Said Ahmed tunamnukuu kama ifuatavyo:

> Wakati wa wakoloni nilikuwa ni mdogo sana. Ila kwa umri wangu kwa wakati huo, yapo baadhi ya matendo waliyowafanyia Waafrika nina kumbukumbu nayo. Hasa hasa wakati ule Waafrika walipoamua kufanya Mapinduzi ya Zanzibar.[14]

Pamoja na kujua huko, jambo la kuwepo kwa baadhi ya maudhui yanayowahusu wakoloni katika kazi zake, tunaamini Said Ahmed Mohamed aliipata athari za matendo ya watawala hao kama inavyoshuhudiwa katika baadhi ya bunulizi zake za mwanzo mwanzo, ikijumuishwa riwaya yake ya *Dunia Mti Mkavu*. Kupitia riwaya hiyo, wanasimuliwa kuhusu wakoloni wa Kiingereza wakati wa himaya ya Malikia na baadhi ya wahusika wa Kizungu kama vile Mr Barnes, Mr David na Mr Jacob ambao kwa namna moja ama nyingine walitumia nafasi zao kwa lengo la kuwakandamiza wanyonge.

[14] Mazungumzo binafsi kati ya mtafiti na Prof. Said Ahmed Mohamed yaliyofanyika tarehe 20/04/2015 Mjini Zanzibar.

Uandishi wa baada ya ukoloni ulikuwa katika namna mbili. Namna ya kwanza ni kuusifia utawala uliopo chini ya Mwafrika. Namna ya pili ni ule wa kuukosoa utawala wa Mwafrika kwa kuwa viongozi waliokabidhiwa dhamana na wananchi hawakuzitekeleza ipasavyo. Kwa kuwa baadhi ya viongozi hao walikuwa ni wasaliti, wala rushwa, wakandamizaji, wahujumu uchumi na uroho wa madaraka. Kwa hakika, Said Ahmed alijiegemeza zaidi katika kuuponda utawala wa Kiafrika. Kwani hakuiona tofauti kati ya watawala wa kikoloni na ule wa Mwafrika. Ndipo mwandishi alipoibuka na riwaya yake ya *Kiza Katika Nuru* ili kuakisi madhila ya viongozi wa Kiafrika dhidi ya wananchi wenzao. Said Ahmed anatueleza:

> Mradi wangu wa kuku unaendelea vyema. Hoteli zangu zinaendelea vyema. Wasokoa nazi shamba wananipa moyo. Ng'ombe wanatoa maziwa ya kutosha. Wakusanya kodi za nyumba zangu hawana matata. Gari zangu na teksi sawa. Kile kiwanda shirika na Jiwanji ingawa kidogo, lakini haijambo kinatia kitu. Nakwambia haya ili uone fedheha kuwa kwako tu ndio sipati kitu (uk 99).

Dondoo hii mwandishi anaonyesha namna ya viongozi wa Kiafrika wanavyokuwa na uchu wa kujilimbikia mali. Jambo ambalo linakiuka utaratibu au makubaliano baina ya viongozi na wanaoongozwa. Hata hivyo, mwandishi anaonyesha hisia zake kali za kuyachukia matendo mabaya yanayotekelezwa na viongozi wa Kiafrika ambao wanajaribu kuyaendeleza matendo yaliyokuwa yakifanywa na wakoloni.Said Ahmed Mohamed anaamini mategemeo ya wananchi juu ya viongozi wao ni kuyalinda maslahi yao baada ya kuyakosa kwa miaka mingi. Bila ya shaka, mambo kama hayo ndio yaliyomchochea Said Ahmed anapoitumia kalamu yake huku akizihusisha mbinu mbalimbali za kisanaa ikiwamo hii ya utanzia ili kuyaakisi matatizo halisi ya jamii yake katika hali ya kisiasa.

### 4.2.6 Muhtasari

Katika kipengele hiki tumejadili miktadha mbalimbali ambayo mtunzi Said Ahmed Mohamed aliipitia katika maisha yake. Mambo tuliyoyazamia hapa ni mfumo wake wa dini, lugha yake ya Kiswahili, taaluma yake, uandishi wake wa zama hizi na mfumo alioupitia au kuushuhudia kisiasa. Dhamira yetu ni kubaini namna ya mtunzi anavyohusisha maisha yake binafsi na utunzi wake wa kazi za kifasihi. Humo katika kazi zake za kifasihi tumegundua mbinu faafu kwake katika kuzifikisha hisia zake ni huku kuutumia utanzia.

## 4.3 Matukio ya Kitanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed

### 4.3.1 Aina za Utanzia

Pamoja na kudokezwa matokeo ya jumla ya utanzia. Soileau (2006) katika uchunguzi wake anabainisha athari ya utanzia huwa unaganda katika maumbile ya mwanadamu kwa hali mbili ambazo ni mwilini na akilini. Katika tasnifu hii, tunaamini na kuafiki kuwa hali hizi mbili zina uhusiano wa moja kwa moja na utokeaji wa matukio ya kitanzia katika kazi fasihi.

#### 4.3.1.1 Utanzia wa Kimwili

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Fasaha* (2010), mwili ni umbo lote la mnyama au binadamu kuanzia kichwani hadi miguuni. Kutokana na mawazo ya jumla ya ufafanuzi huu, aghalabu mwili wa mwanadamu umekusanya viungo mbalimbali vinavyoonekana kwa uwazi. Mathalani, kichwa, mikono, masikio, macho, tumbo na miguu. Hali ya utokeaji wa utanzia unaweza kwenda moja kwa moja kuvishambulia na kuvijeruhi viungo mbalimbali vya mwilini. Hivyo, imani yetu iliyojengeka ndani ya tasnifu hii ni kuwa mwili ni nyenzo ya msingi katika kukabiliwa na matatizo ya matukio ya kitanzia.

#### 4.3.1.2 Utanzia wa Kiakili

Akili, kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Fasaha* (2010), ni uwezo wa ubongo kufikiri kwa muda mfupi na kutoa jawabu au uamuzi sahihi. Naye Syambo (1992) anaona akili ni sehemu mojawapo inayotoa ufahamu na utambuzi wa mtu. Anaendelea kusema kipimo cha mtu hutambulikana kupitia akili. Kutokana na maelezo haya inaonekana akili ni nyenzo muhimu katika maisha ya uwerevu na utambuzi wa mwanadamu. Zaidi, akili inaweza kuharibiwa inapokumbwa na matukio ya kitanzia kwani kama tulivyoeleza huko nyuma utanzia hujumuisha matatizo yanayotokea katika harakati za maisha ya mtu.

#### 4.3.1.3 Utanzia wa Kiroho

Kwa mujibu wa TUKI (2004) roho ni kitu kisichoonekana ambacho hufikiriwa kuwa ni sehemu ya mwili wa kiumbe ambayo hukiwezesha kuwa na uhai. Wanaendelea kueleza kuwa roho ni hali ya kuwa na huruma na wema. Mawazo ya TUKI yana msingi muhimu kwetu hasa hasa tukiyachukulia maelezo yao ya pili ambayo yanaakisi hali ya kumjenga mtu kuwa na huruma na wema. Hali hizi mbili zinaungwa mkono na Wafula na Njogu (2007) pale waliposema ". . . mbinu hii imekuwa ikitumiwa na watunzi mbalimbali katika utanzu wa riwaya kwa lengo la kuyaunda matukio yenye ujumbe mzito yanayowasilishwa kwa lugha inayonawiri ili yazindue hofu na huruma. Kimsingi, utanzia wa kiroho una mfungamano wa moja kwa moja wa kumfanya mtu aweze kuwa na hisia za huruma na wema baada ya kukabiliwa na tukio la kitanzia.

Hivyo, kutokana na vijenzi na matokeo ya utanzia kama yalivyofafanuliwa huko nyuma pamoja na aina hizi tatu za utanzia, tasnifu hii imebaini kuwa kazi yenye matumizi ya utanzia huwa na sifa au tabia za msingi zifuatazo:

a) Huwa na mwendo wa pole. Hapa inahusiana zaidi na masimulizi ya mtunzi ambayo yanakwenda taratibu mno kiasi ambacho msomaji hupata umakini ndani ya kazi husika. Hii ni kinuyume na kazi za kifutuhi ambazo huwa na mwendo wa kasi sana.

b) Humfikirisha sana msomaji. Ni kutokana na matukio yake huwa ni ya kuhuzunisha yenye kuhusiana na jamii. Hivyo, msomaji anahusisha tukio la kitanzia na ama jambo lililomkuta au kulishuhudia ndani ya jamii yake.

c) Humfanya msomaji awe karibu na mhusika ambaye ni mhanga wa utanzia. Yaani, kazi zenye mwegamo wa matukio ya kitanzia huwapo mhusika mkuu anayejitolea mhanga kwa lengo la kuleta mabadiliko. Kwa hali hii msomaji hulazimika kuwa karibu naye kwa kuwa ndiye mwenye kuchukua wazo kuu la mtunzi.

d) Husisimua. Hoja hii inaakisi yale matukio ya kitanzia ambayo msingi wake ni kutoa huzuni inayompa athari ya moja kwa moja msomaji. Mathalani, kupandwa na jazba au kuwa na huruma.

e) Huhitaji umakini mkubwa katika kuzisana. Ubunaji wa kazi za kitanzia zinahitaji uwezo wa hali ya juu kwa mwandishi katika kuyatunga na kuyaunganisha na uhalisia uliopo ndani ya jamii. Ithibati ya jambo hili ni kuwa kazi za kitanzia ni chache mno zikilinganishwa na zile za kifutuhi.

### 4.4 Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed

Sehemu hii inaeleza muhtasari wa jumla kuhusu riwaya tatu teule za Said Ahmed Mohamed. Riwaya hizo zimetusaidia kutuonyesha mwelekeo wa kuyaibua na kuyatolea ufafanuzi matukio kadhaa ya kitanzia. Ufafanuzi kuhusu matukio hayo na mjadala wake umeelezwa katika sehemu inayofuata.

#### 4.4.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Utengano* (1980)

Riwaya ya *Utengano* inazungumzia maisha ya wakati wa ukoloni. Inaonyesha jinsi wananchi wazalendo walivyoshikamana na kushirikiana katika kufanya mageuzi ya kuwaondoa watawala dhalimu. Azma kubwa ya mageuzi hayo ilikuwa ni kujitawala wenyewe kwa matarajio na mustakbali mzuri wa maisha yao wenyewe bila kuingiliwa na wakoloni. Lakini matarajio hayo hayakupatikana.

Hadithi inasimulia hali iliyojitokeza kwa wazalendo walioshikilia hatamu za uongozi. Baada ya uhuru viongozi hao, walianza kuyafisidi malengo ya wananchi kwa kuyafanya mambo mbalimbali yaliyokataliwa na wananchi wakati wa ukoloni. Mathalani, viongozi kama Bwana Maksuudi ambaye Mkuu wa Wilaya na Bwana Zanga waliwasaliti wananchi kutokana na majukumu waliyokabidhiwa. Walianza ubadhirifu wa mali ya umma, waliendeleza dhuluma na unyanyasaji, ubinafsi, uroho wa madaraka, utumiaji wa magendo na rushwa. Mambo haya yaliwakera wananchi na kuamua kuwakataa waziwazi katika kampeni za uchaguzi.

Kitovu cha riwaya hii ni kuhusu familia ya Bwana Maksuudi ambaye alimuoa mke wa pili, Bi Tamima. Mke huyu alimuoa baada ya kumuacha mke wa awali, Mwanasururu ambaye alimnyanyasa na kumtesa hadi kumsababishia kifo. Maksuudi alibahatika kupata watoto wakubwa wawili, Mussa na Maimuna. Familia hii imebeba

dhana nzima ya “utengano” iliyosababishwa na tamaa na wivu uliokithiri kwa kuwatawisha Tamima na mwanawe Maimuna. Utawa uliokithiri ni miongoni mwa hoja iliyoibuliwa na mwandishi. Ameonyesha ni kwa jinsi gani baadhi ya wazazi katika miaka ya 80 walivyowakosesha watoto wao, hasa wa kike, uhuru wa kuamiliana na jamii katika hali mbalimbali. Mathalani, kukosa elimu ya mazingira katika jamii. Kwani Bwana Maksuudi hakuona haja ya kumruhusu mkewe pamoja na mtoto wake katika kuukabili ulimwengu uliowahitaji.

Riwaya inazungumzia hoja ya kisasi kilichoandaliwa na Bi Farashuu kutokana na kitendo cha Maksuudi kumdhulumu na kumtesa mwanawe Mwanasururu aliyekuwa mke wake wa kwanza. Matokeo ya kisasi hiki kilisababisha kuparaganyika kwa familia ya Bwana Maksuudi. Hali hii ilimfanya Mussa kumkimbia babaake, mamaake na ndugu yake Maimuna. Kisasi kilitekelezwa na Kazija pamoja na Biti Kocho, mtumishi wa ndani katika nyumba ya Maksuudi, Maimuna alitumbukia katika umalaya, unywaji wa pombe, wizi na kutoelewana na watu. Kwa upande wa Bi Tamima, hali hiyo ilimfanya apigwe na mumewe kwa kutumia bakora na ukanda na hatimaye kuachwa. Bwana Maksuudi ilimsababishia kukataliwa na wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi, kufungwa jela kwa muda wa miaka miwili, kulazwa hospitali baadaye kuzirai na kufariki dunia.

Hatimaye, Bwana Maksuudi alijitambua kuwa ndiye chanzo cha matatizo yote yaliyoikabili familia yake ya kitajiri. Kuungama kwa Maksuudi kulikubaliwa na Maimuna, licha ya kutoonana naye kwani tayari amefariki na kuzikwa. Mwisho, riwaya inahitimisha kwa kusimulia muafaka na utengamano wa familia ya Bwana Maksuudi ambapo Mussa, Bi Tamima na Maimuna wanakutana kwa pamoja baada

ya kutengana kwa miaka mingi na kuwa kitu kimoja. Huku Bi Farashuu akimsamehe na kuyasahau yote aliyofanyiwa na Bwana Maksuudi katika ulipizaji wake wa kisasi.

### 4.4.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* ( 2002)

Hii ni riwaya inayozungumzia madhila yaliyokuwa yakifanywa na wakoloni wa Kiingereza. Wakoloni hawa walikuwa chini ya himaya ya Malkia kwa wananchi wanyonge wanaojumuisha makuli, wachukuzi, wakulima, wafugaji na wafanyakazi wa viwandani. Nafasi za uongozi wa juu kwa wakati huo zilikuwa zimeshikiliwa na Waingereza. Kuthibitisha hilo, mwandishi anawataja wahusika kama vile Mr. Barnes ambaye ni Mkuu wa Bandari, Mr David ambaye ni *Commissioner of Police,* Mr. Jackob mkuu wa Kilimo na Hakimu Mzungu. Viongozi hawa walikuwa wakisaidiwa bega kwa bega na wazawa ndani ya jamii ya watawaliwa. Hawa ni kama vile, Inspekta Farouk, Makame, Fauz na Bwana Hamoud ambao walishiriki kwa namna moja au nyingine katika kuwakandamiza wananchi wenzao.

Kutokana na kukithiri kwa dhuluma, ukosefu wa haki, rushwa na usaliti, ndipo wananchi wakaamua kupanga mikakati ya kuwaondoa wakoloni ili wawe huru. Hii ni kutokana na maonevu yaliyokuwa yakitendwa dhidi yao. Katika kuitekeleza mikakati hiyo, walichukuwa hatua kuu tatu ambazo ni kugoma, kuandamana na kufanya mapinduzi. Kwa upande wa kugoma, wananchi, wakiwemo makuli, wachukuzi, wakulima, wafugaji, wafanyakazi viwandani na wazururaji mjini walishirikiana ili kuhakikisha panatokea mageuzi na mabadiliko ndani ya jamii. Baada ya kugoma kwa siku tano, wananchi wazalendo walioitisha mgomo walikamatwa, walifungwa na baadhi yao kuuliwa. Licha ya mambo hayo waliyofanyiwa, wananchi walifanikiwa kuwaondosha wakoloni pamoja na vibaraka vyao.

Jaribio la wananchi la kufikisha ujumbe wao kwa serikali ya kikoloni, kwamba wamechoka kunyanyaswa na kudhulumiwa, serikali ya kikoloni ilitumia hatua mbalimbali kuhakikisha mwamko wa wananchi dhidi ya kuigomea serikali yao unakomeshwa na kudhibitiwa mara moja. Kwa mfano walitumia njia ya kuua na kuwafunga viongozi wa juu wanaohamasisha kuleta mabadiliko. Vilevile, walitumia njia ya vyombo vya ulinzi na usalama kama Jeshi la polisi; kwa lengo la kuwadhibiti. Licha ya hatua zote hizo, hazikuweza kufanikiwa kutokana na nguvu ya umma.

Kiini cha riwaya hii ni matatizo inayoikabili familia ya Bwana Jaku kutokana na umaskini na unyonge. Hali hii iliweza kusababisha kumgawa mwanawe Kibwana Jaku kwa Bi Nafisa. Bwana Jaku alitumia nguvu bila kumshirikisha mkewe kwa hoja ya kutoweza kuwahudumia watoto pacha kwa wakati mmoja. Hadithi inaendelea kufafanua namna ambayo haki isipotendeka husababisha athari mbaya hata kwa ndugu wa damu. Said Ahmed Mohamed analipigia mfano suala hili kwa Kibwana Jaku kumsababishia babaake kufungwa jela bila kujua. Kibwana alilelewa katika familia ya kitajiri ya Mzee Hilali na mkewe Bi Nafisa (Bibi wa Minarani) tangu utotoni mwake. Hivyo, fikra zake zilijijenga kuwa wazee wanaomlea hivi sasa ndio wazazi wake wa damu. Kufungwa huko kwa Mzee Jaku katika kipindi cha miaka kumi na tano bila ya kosa lolote. Ulitokana na sheria kutojali haki kwa wanyonge. Mwandishi anatuambia hivi:

> Kesi ya Bwana Jaku ilikuwa ngumu, lakini kwa ubingwa na uhodari wake, Farouk alikusanya ushahidi wa kutosha dhidi yake. Akamtumbukiza hatiani akijua bwana huyo hana hatia. Na sasa alitafahari na kujisifu kwa namna alivyomtanza mshtakiwa. Sijui kwa nini jaji alimfunga miaka kumi na tano bwana yule; kesi yake ni kunyongwa tu; *it was quite clear. Oh, yes, quite clear. It was murder*. Kesi hiyo ndio ilimpandisha cheo. ‘Lakini bwana yule, siku ile alionyesha maajabu, nafikiri miaka kumi na mitano ilimtia kichaa, akawa anapiga kelele ovyo, ati alinambia mimi mwanawe: Kibwana unanifunga mwanangu, mimi sina hatia, mwanangu

> Kibwana... Kanipata wapi mwana kama mimi? Toka lini mimi mwanawe? Miaka imembobea hata hajui anasema nini (uk 76).

Baada ya kutumikia jela, Bwana Jaku alidhamiria kuitafuta familia yake kwa udi na uvumba, aliweza kukiri makosa aliyoitendea familia yake hasa kwa mkewe Bi Pole. Dhana hii ya majuto Said Ahmed Mohamed, ameweza kuitumia katika riwaya yake ya *Utengano* kama Bwana Maksuudi alivyojuta na kukiri makosa. Kusudio la Bwana Jaku ni kuitafuta na kuunganisha pamoja familia yake. Juhudi hiyo haikufua dafu kwa sababu wote walikuwa wameshafariki.

Mwandishi anahitimisha riwaya yake kwa kuyaonyesha majonzi yaliyomuandama Mzee Jaku na upweke uliotokana na vifo vya wanawe wanne. Kwa kifupi, riwaya inazungumzia mambo yafuatayo. Mosi, ni suala la ukoloni lililoingia katika nchi za Afrika. Pili, ni mapambano ya wananchi waliotawaliwa kwa miaka mingi dhidi ya wakoloni. Tatu, ni vibaraka wa wakoloni jinsi walivyoweza kuwasaidia katika kuwadhulumu wananchi wanyonge. Nne, ni jinsi ambavyo familia zinavyoweza kugawanyika katika mapambano ya kuleta haki ndani ya jamii.

#### 4.4.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Kiza Katika Nuru* (1988)

Riwaya inazungumzia maisha ya wananchi waliyopigania uhuru kutoka kwa mkoloni. Haionyeshi moja kwa moja wakati wa utawala wa kikoloni kama ilivyojitokeza katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*. Mwandishi ameonyesha jinsi wakoloni wa Kiingereza walivyoishi ndani ya koloni lao na matendo waliyokuwa wakiwafanyia wazawa. Ameeleza tu sehemu ya kumbukizi ya namna ya wananchi walivyopigana vita kwa lengo la kuwaondoa wakoloni. Kumbukizi zao zilihusu matarajio yao baada ya kuwaondoa wakoloni. Kazi hii imefafanua kwa uwazi matendo yaliyokuwa yakitekelezwa na viongozi wa juu. Viongozi ambao

walichaguliwa na wananchi kwa lengo la kuongoza kama wananchi walivyotaka. Viongozi waliyopewa dhamana mbalimbali walianza kuzikhini dhamana hizo kwani waliendeleza kufanya matendo mabaya kama ubadhirifu wa mali ya umma, ubinafsi, uroho wa madaraka, magendo, unyanyasaji pamoja na ukandamizaji, usaliti, dharau na kejeli na dhulma. Mwandishi amemtumia mhusika Bwan Juba kuiwakilisha hali hiyo.

Kutokana na kukithiri kwa matendo yasiyowaridhisha, wananchi walihamasika na kujitambua kuhakikisha viongozi hao wanaondoka madarakani. Mwandishi amemtumia Mvita, mtoto wa Bwan Juba, katika kukiondoa kiza kilichotanda kwa wananchi kwa kuanzisha mikakati kadhaa. Kwa mfano, alimpiga vita babaake mzazi kutokana na matendo mabaya anayoyafanya. Aliwazindua na kuwaunganisha wananchi. Said Ahmed anasema:

> Nililolitafuta na ambalo bado naendelea kulitafuta ni kujaribu kuutazama ukweli ninavyouona mimi na kutaka kuwaonyesha wengine jinsi n' navyouona mimi na kujadiliana nao na kukubiliana nao kama wao wanaona vingine na baadaye kutafuta njia moja ya kuishi bila ya mmoja kumuonea mwingine. Panapo kiza nuru lazima imulikwe. Panapo ujanja na hadaa, lazima ukungu ufunuliwe ili watu waweze kuona ukweli au kile kilichofichama (uk 202).

Mikakati iliyoanzishwa na Mvita imefanikiwa kwa wananchi kuwaelewa wabaya wao hata kama walivaa joho la kiucha Mungu. Kabla ya hapo, wananchi walikuwa katika kiza.cha kukosa kuujua ukweli dhidi ya viongozi wao. Ujio wa Mvita baada ya kupata elimu; ulikuja kulifaidisha taifa lake.

Katika kina cha hadithi hii, mwandishi ameonyesha namna ya familia inavyoweza kutofahamiana na kufanyiana uadui; hata kutoana roho pale haki na ukweli zinapotaka kuchukua nafasi. Said Ahmed Mohamed amelisawiri hili kwa Bwan Juba mwenye mke anayeitwa Kudura, na watoto wake wakubwa wawili; Mvita na Mbishi.

Hadithi inadhihirisha pande mbili zenye kukinzana ndani ya familia moja. Bwan Juba kwa upande wake anaendeleza maovu na kuwarubuni watu wasiuelewe ukweli wa mambo yanavyokwenda katika taifa lao. Huvaa joho la Ushekhe ili kuakisi wema. Upande wa Mvita, Kudura, na mdogo wake Mbishi walipata mwamko wa kupambana na Bwan Juba, ili kuimurika jamii iondokane na kiza kilichowafunika.

Mwisho hadithi inamalizia kuonyesha mkasa wa msiba uliojitokeza katika familia ya Bwan Juba. Kwanza, Mvita kuuliwa na Shazi kutokana na mpango uliosukwa na babaake mzazi. Pili, Bwan Juba kuuliwa na Kudura ili alipize kisasi cha kuuliwa mwanawe Mvita. Tatu, ni Kudura kujiua mwenyewe alipokuwa gerezani.

Baada ya ufafanuzi kuhusu muhtasari wa riwaya teule za Said Ahmed Mohamed. Sehemu inayofuata inahusu mjadala wa utokeaji wa matukio ya kitanzia katika riwaya hizo.

### 4.5 Matukio ya Kitanzia Yaliyotumika Katika Riwaya Teule

Sehemu hii inajadili utokeaji wa matukio ya kitanzia ambayo kwa namna moja au nyingine yameweza kutoa hisia za huzuni kwa wasomaji. Said Ahmed ameyateua matukio hayo ili afikishe dhamira zake kwa jamii.

#### 4.5.1 Matukio ya Kitanzia Katika Riwaya ya *Utengano*

Tukio la kwanza linajitokeza wakati mwandishi anapofafanua adhabu azipatazo Bi Tamima kutoka kwa mumewe Bwana Maksuudi. Mwandishi anasema:

> Maksuudi alimgeukia tena Tamima. “Wallahi nitakupiga leo, nikubakishe kope tu. Utasema husemi? Nitakula nyama mbichi mimiiiiiii”, Maksuudi alipiga kelele na kutikisa bakora yake hewani. Tamima huku akitetemeka, alirudi nyuma. Wote waliokuwepo walimeza pumzi moto. “Maimuna yu wapi naseeeemaaaa. Ilikuwaje? Alaa, ndiyo mambo yako haya? Nikiondoka mimi, wewe hutawala enn? Unamtorosha mwanangu na wewe mwenyewe

> unajiuza siyo? Yuko wapi Maimunaaaa?" Maksuudi ilimtoka bakora ambayo ilianguka juu ya kichwa cha Tamima. Tamima alipiga usiyahi mkubwa akaanguka chini. Muda ulipita. Maksuudi alihema kwa ghadhabu na Tamima aligaragara. Baadaye, Tamima alipopata upumzi, alitupa mkono pale alipopigwa bakora. Damu ilikuwa ikimchururika (uk 47).

Utanzia wa hapa ni wa kimwili ambao huweza kumjia msomaji anapoijenga picha ya jinsi Bi Tamima anavyopewa kipigo huku akiwa katika lepelepe la uzazi. Kitendo cha kupigwa kilichoambatana na mchururiko wa damu kinatoa taswira ya kimajonzi, hasa ikizingatiwa kuwa mwanamke anayepigwa amejifungua hivi karibuni, hata mwili wake haukurudi katika hali yake ya kawaida. Mtunzi ameuweka utanzia huu ili kuonyesha ni kwa jinsi gani wanaume wanavyowapa mateso wanawake kwa kujilinda na maovu yao. Ifahamike kuwa muda huu wa kutolewa adhabu hii, ni baada ya Bwana Maksuudi kurudi kwa mwanamke wake Kazija.

Tukio jingine la kipigo ambalo linaweza kumhuzunisha msomaji ni hili lifuatalo:

> Maksuudi alitupa bakora yake na sasa aliupapatua ukanda wake kiunoni. Aliuvuta na kuanza kumcharaza nao mkewe. Raap! Ukanda ulitua juu ya mwili wa Tamima. Mtumeeee, alisalia Tamima huku akiangukia meza iliyokuwa na buli na vikombe vya kahawa vya fedha. Hivyo akaenda navyo chini pamoja. Maksuudi aliendelea kumpiga Tamima kanda za mafumba. Tamima hakujua njia ya kujikinga. Maksuudi aliendelea kucharaza. Tamima zilimtoka mtume nyingi. Hakuwa na hila wala rai ya kujiokoa. Pale chini alibaki kusota kitangomalele na huku Maksuudi akimrapua kwa ukanda. Akamwandama ukumbi mzima. Vitu vya mapambo vikaanguka. Maksuudi aliendelea kumrapua Tamima; mara kipembe hiki mara kipembe kile na mara amvute mkono amlete katikati ya ukumbi. Ilikuwa hujma isiyokuwa na mwombezi, na Maksuudi alipiga kama mwandawazimu (uk 49).

Hapa utanzia unasababishwa na kitendo cha upigaji wa kutumia ukanda. Huyu ni mume anayepambana na mkewe. Katika tukio hili, huzuni inaingia katika hisi ya msomaji kwa kitendo cha kupigwa kichwani huku Bi Tamima akiangukiwa na meza yenye mkusanyiko wa buli, vikombe pamoja na vitu vya mapambo. Jambo hili

linaonekana linamkera sana mtunzi. Kwani amelikuza kwa kutumia mubalagha kwamba akamwandama ukumbi mzima. Hapa mwandishi anaonyesha namna ya mfumo dume unavyoendeleza unyanyasaji kwa wanawake. Anaamini kwamba mfumo dume uliopo katika jamii, huweza kumdhalilisha mwanamke kwa kuwapa adhabu zisizojali utu wa kibinadamu jambo ambalo wanaume hujihisi wapo juu ya sheria.

Adhabu nyingine inayohusiana na utumiaji wa ukanda ni tukio hili la Bwana Maksuudi dhidi ya Mwanasururu. Riwaya inasema:

> Kwenye meza kulikuwa na picha kubwa ya mwanawe, Mwanasururu. Huyu ameshatengana na ulimwengu, amekufa kabla zake. Na Maksuudi, ndiye aliyekuwa sababu ya kifo chake. Na ile mali ya mwanawe ambayo ilikuwa ikimwendesha yeye Mwanasururu na Farashuu mamaake, yote imefisidiwa na huyu Maksuudi. Farashuu alimuona tena mwanawe katika kivuli kisichokuwepo akimuhadithia matendo ya mumewe Maksuudi. Sasa macho yake yalianza kulengalenga machozi. Nyuma ya machozi haya kulikuwa na picha ya Mwanasururu katika mateso mbalimbali aliyokuwa akiteswa na Maksuudi. Anakumbuka alipomhadithia jinsi yeye Mwanasururu alipopigwa kanda mpaka akazirai. Chozi lilimtiririka Farashuu, akilifuta kwa kanga yake (uk 60).

Mateso ya kupigwa kwa Mwanasururu hadi kuzirai bila shaka, itamfanya msomaji ajiwe na maumivu ya kimwili. Jambo linaloshindiliwa na mwandishi hapa ni ule utekelezaji wa mateso huku yakienda sambamba na unyang’anyi wa mali. Tukio hili lilikuwa katika kumbukizi ya Bi Farashuu kwa mwanawe. Lakini katika ukumbukaji huo ulizua mtiririko wa machozi. Licha ya kusikitisha, tukio hili linatoa ujumbe mzito kwamba suala la kuwaadhibu wanawake bila ya sababu ya msingi ni jambo linaloweza kuhatarisha uhai wa mtu. Pamoja na hilo, Said Ahmed Mohamed anakemea udhalilishaji wa wanaume dhidi ya wanawake katika hali yayote ile.

Tukio lingine linalohusiana na adhabu ni lile la kupewa talaka kwa Bi Tamima. Mwandishi anafafanua tukio hili kwa kusema:

> "Hii talaka", Maksuudi alimtupia Tamima ile karatasi aliyokwisha iandika. Tamima alinyoosha mkono na kuiokota talaka yake. "Mwa . . .mwanangu je?" Tamima bado hajanyamaza kilio. "Mwana gani? Huyu mchanga? Maana wana wawili umewaharibu na kuwapoteza wewe. Sasa nikupe na huyu wa tatu siyo? Ukamuuwe siyo? Ehe kwanza utamlisha nini? Utamvisha nini? Nenda kamtafute Maimuna na yeye umwambie asirudi, nyumba hii aione paa," Maksuudi alipayukwa huku anarusha mikono kama mwendawazimu (uk 54).

Katika mazingira ya kutolewa kwa talaka hii utafiti umebaini kuwa utanzia waweza kutokea kwa sababu talaka iliyotolewa haikuwa na sababu ya msingi, kwa kuwa kosa halikuwa la mwanamke bali ni la mwanamume. Pamoja na haya, muda wa kupewa talaka na kufukuzwa katika makazi ya Bwana Maksuudi, umeambatana na ukiwa uliomkabili Tamima. Hii ni kutokana na kutojua uhakika wa kupata huduma za lazima. Jambo kubwa zaidi, Bi Tamima tayari ana kitoto kichanga kinachohitaji malezi na matunzo ya karibu zaidi kutoka kwa mama na baba.

Katika tukio lifuatalo, mwandishi ameubainisha utanzia kupitia mazingira ya ajali. Tukio limesawiriwa kwa mhusika Kabi. Mwandishi anasema:

> "Mimi nilizaliwa na miguu yangu miwili lakini nimepoteza mguu wangu wa pili kwa kumuokoa mamaangu. Mamaangu katika siku za mwisho wa umri wake alikuwa mwendawazimu. Na wazimu huo aliupata kwa ulevi mwingi alioushiriki siku zake za mwisho. Siku moja aliniita chumbani kwake, na mimi mdogo siku hizo, mtoto wa miaka kumi na tatu. Nilipofika chumbani, niliyojionea na lile ambalo alitaka nilifanye lilinipa hapo hapo nitoke mbio. Nyumba yetu iko kando kando na barabara. Niliufungua mlango wa nje kwa pupa. Kuchupa kizingiti tu, nataka kukata barabara, gari hilo limefika, pua na mdomo nami. Mtume! Mtume! Mtume! aaa wapi! Gari lilinipiga dafurau moja na kunirusha huko! Sikujijua tena" "A-a, maskini we, tena?" Maimuna alijaa huzuni. Hiyo ndiyo iliyokuwa sababu ya kukatwa mguu huu. Ulikuwa umevurugikavurugika (uk 163).

Haya ni masimulizi ya Kabi kwa Maimuna kwa njia ya majonzi. Anamueleza namna ya ajali ilivyompata hadi kupoteza mguu wake. Tukio hili tunalichukulia kuwa ni sehemu ya kumpa msomaji jitimai. Kwani mtunzi ametumia kiungo cha mwili wa binadamu katika kutengeneza utanzia. Kiungo kilichobainishwa na mtunzi ni mguu uliovurugika kutokana na kugongwa na gari jambo ambalo limempa Kabi ulemavu wa kudumu. Pia, ametaja sababu ya kuzuka kwa ajali hii ni pale mamaake Kabi kumlazimisha ashiriki katika uovu wa kulewa. Hata hvyo, Kabi alikataa. Hapa mtunzi kwa mara nyingine amelitumia tukio hili ili kuwasuta wazazi wenye tabia ya kuwalazimisha watoto wao kushiriki maovu.

Utanzia mwingine Said Ahmed Mohamed anausawiri kupitia. Tukio kubwa ni lile la Bwana Maksuudi kufariki dunia kama anavyotuambia:

> Mimi siponi Mussa, nakufa, na kifo changu kimesababishwa na ubaya wangu mwenyewe, na hasa uchungu wa Maimuna aliyekuwa kipenzi changu. N'nakufa Mussa, lakini mtafute Maimuna umhakikishie kwamba mimi nimempa radhi zangu, na yeye anisamehe sana. Mhakikishie kwamba sisi tulikuwa na mapenzi na ukweli naye. . . Baadaye baba alikata roho. Alikata roho huku akipunga mikono kama wewe daima ulimsimamia usoni pake. Na katika dakika yake ya mwisho, alitaka urudi, umwendee, akuvae na akupakate kama alivyokuwa akikupakata ulipokuwa mchanga. Lakini wapi, baba nd'o tumeshamzika, hamkuwahi tena kukutana (uk 175-176).

Huu ni umauti uliomkabili Bwana Maksuudi. Umauti ambao ulishikamana na wasia kwa mtoto wake Maimuna. Katika hali yake ya mwisho anajuta kwa matendo mabaya aliyokuwa akiyafanya dhidi ya familia yake. Utanzia wa Said Ahmed Mohamed hapa ni wa kiakili ambapo upo kwa namna alivyoweza kuonyesha kifo cha Bwana Maksuud kwa hali ya majonzi yaliyomwandama wakati wa kutoka roho. Kipindi hiki ndicho alichoungama kutokana na makosa yake. Kwa kawaida, mtu anapofariki dunia huchukuliwa ni kitendo cha majonzi na masikitiko. Hata iwe mtu

huyo aliyefariki ni mbaya au mwema. Bwana Maksuud aliyatenda mabaya mengi; licha ya mabaya yake, watu waliotendewa mabaya kama vile Bi Farashuu, Bi Tamima, Maimuna na Mussa walihuzunika sana baada ya kupata taarifa ya kifo cha Bwana Maksuudi. Hapa mtunzi anatufungulia hoja ya kuomba msamaha na kusamehe.

Tukio jingine la kifo limejitokeza kwa Mwanasururu mtoto wa Bi Farashuu. Mwandishi anasema hivi:

> Kwenye meza kulikuwa na picha kubwa ya mwanawe, Mwanasururu. Huyu ameshatengana na ulimwengu, amekufa kabla zake. Na Maksuudi, ndiye aliyekuwa sababu ya kifo chake. Na ile mali ya mwanawe ambayo ilikuwa ikimwendesha yeye Mwanasururu na Farashuu mamaake, yote imefisidiwa na huyu Maksuudi (uk 175).

Mwandishi anataja kwa kifupi namna ya mwanamke huyu alivyosababishiwa kifo na Bwana Maksuudi. Mateso ya Bwana Maksuudi yalitekelezwa kwa nyenzo ya kutumia ukanda. Namna hii ya kutoa mateso ambayo yamehatarisha uhai wa Mwanasururu yanatoa hisia za huzuni au unyonge kwa msomaji. Pia, athari ya huzuni imepatikana kwa mhusika Farashuu ambaye alihuzunika hadi kufikia hatua ya kutokwa na machozi.

Zaidi ya adhabu, ajali na vifo, mwandishi ametumia dhana ya kilio ili kuibua utanzia kwa hadhira yake. Nukuu ifuatayo inatoa taswira nzima ya kilio.

> Maimuna alibwagika chini. Alizidi kulia huku akinyamazishwa na kila aliyekuwepo hapo. Halafu alipokuwa akija juu uso wake ulitokeza kukabili kioo cha gari. Alijiangalia, akaliona lile kovu lake. Hakujua kama ataweza tena kuyasahau ya zamani. Hasa akiwa na kovu lile. Tena alimwangalia Mussa machoni mwake. Humo bado mlikuwa mkitiririka machozi. Uso wake ulikuwa wa huzuni na msiba. Akageuka na kumtazama Kabi mumewe, akamwona machozi njia mbili mbili. Ukweli na imani ya mkewe ilimweza Kabi. Maimuna alimgeukia mamaake. Uso wake Bi Tamima umeroa machozi; huruma na mapenzi katu hayakumpa kumwacha

> mwanawe aliye peke yake. Na alipokuja kumwangalia Farashuu, kifua chake kiliroa chapachapa. Kwake Farashuu kilikuwa kilio cha machozi ya mafuriko- alikuwa akimaliza kilio chake cha ghadhabu alichokuwa akililia miaka kwa miaka. Lakini hatimaye alinyamaza na kilio chake kilikatika moja kwa moja, na chozi lake, lile aliloliita, Chozi la mliwa, lilikauka moja kwa moja pia. Hakujua kama amefurahi au amezidi kuhuzunika. Hivi sasa alifumwa na kifo cha Maksuudi ambacho alikihisi amekisababisha yeye (uk 176).

Kila mmoja kati wahusika hao wamebebeshwa huzuni zinazoashiriwa kwa njia ya kulia au kutokwa na machozi. Kwa upande wake Maimuna analia hadi kuanguka chini huku akishindikizwa na vilio vya akina Mussa, Kabi, Bi Tamima, na Farashuu. Ametumia mtindo wa vilio vya wahusika tofauti ili kupata utanzia. Ambapo vilio hivi vimewaambukiza wasomaji na kujihisi kutokwa na machozi. Tukitaka kujua uzito wa jambo hili, ni vema, kwa kuzingatia msingi wa mkabala wa Mwitiko wa Msomaji, Hivyo, matukio haya ya kulia ni ithibati ya namna ambavyo mtunzi anavyoonyesha uwezo wake mkubwa wa kuwaathiri wasomaji.

### 4.5.2 Matukio ya Kitanzia Katika Riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*

Tukio la kitanzia limeibuka katika hali ya ugonjwa. Said Ahmed Mohamed amelijenga tukio lifuatalo:

> . . . Pandu aliinama, na kwa jicho la karibu aliona mdomo wa bibi huyu umeroa damu. Alishtuka kwa ugunduzi huo. Aliokota kitambaa. Akaifuata hiyo damu kutoka mdomoni – nyengine imetapakaa kifuani pake pote na nyengine imefanya baka kwenye shuka. Staghafiru anahema, pumzi za mjusi; kupuma na kupumua; haziwashi wala hazizimi moto. Pandu alinyoosha mikono yake inotetema, akamgeuza mzee wake. Alimlaza kichalichali, akamnyoosha miguu na mikono mbavuni. Alimwinua kichwa, akakitua na kukiweka sawa. Hima alifika kwenye kasha bovu ambalo lilitumika kama meza ya mganga. Hapo alichukua pamba na kurudi nayo kwa mgonjwa. Alimfuta damu midomoni na kifuani. Tena alipangusa ile iliyotapakaa kwenye shuka. Kisha alitupa pamba iliyotumika ndani ya kikapu kibovu kilichowekwa kupokea uchafu. Staghafiru aliendelea kutweta. Hatimaye Pandu alikaa ubavuni pa mgonjwa juu ya kitanda, akimwinua mkono Bi Staghafiru, akaukanda. "Kkon' kkon' kkon' kkon' . . . u-u-u-u-u,

> aaaaa . . .” alikohoa Staghafiru na kuugua, Safari hii kikohozi kifupi. Kisha alifurukuta; akavuta jicho lake angani, akatazama, kama vile dari ilimwonyesha maajabu ya siri. Tena aliteremsha jicho, akamtunga Pandu. Kimya kikazidi kumea. Nzi aling’ong’a na kuruka akimzunguka mgonjwa kichwani na hatimaye kutua kwenye paji lake. Pandu alimwinga. Kwa ghafla tumbo la mgonjwa lilipiga mpwago. Staghafiru alipaza sauti, akameza mate, akashusha pumzi. Pandu alikithiri huzuni. Kiumbe pekee aliyemjali na kumwaia mapenzi alikuwa katika ukomo wa safari ngumu (uk 65- 66).

Taswira ambayo mtunzi anatujengea katika tukio hili, ni ile ya Pandu na mlezi wake Bi Staghafiru. Bibi huyu alipata tabu wakati wote wa maradhi. Maradhi aliyoyapata ni T.B. Tukio hili linaibua huzuni katika hali ya kiroho wakati ambapo msomaji hujenga jumla ya tabu alizozipata wakati wote wa kuumwa kwake. Hivyo humjenga kuwa na hisia ya kumhurumia mgonjwa. Mtunzi anazibainisha tabu hizo kama vile ya ukohoaji wa shida, utokaji wa damu za mdomoni mara kwa mara, upumuaji wa shida na maradhi yaliyomweka kitandani kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo. Kwa jicho la kifasihi, Said Ahmed amezibainisha tabu hizi ili kuizindua jamii kuhusu umuhimu wa kuwatunza wazazi hasa katika kipindi cha matatizo. Pia, imulikwe picha ya hali halisi kuhusu ukosefu wa huduma za msingi katika jamii kama vile hospitali.

Matukio ya vifo yamechukua nafasi katika kujenga utanzia katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*. Tukio kubwa ni lile la wahusika Pandu, Fumu, Bakari, na Farouk. Hawa ni watoto wa familia moja ya Mzee Jaku. Kwa pamoja walikabiliwa na umauti wa kuuliwa. Vifo hivi vinaelezwa kama ifuatavyo:

> Mzee Jaku sasa alikuwa keshafika chini ya wale maiti, Mughma umemvaa; kijasho kinamkatika, malaika yamemsimama, moyo unamwenda mbio. Alitazama maiti ya Pandu, tena ya Fumu, halafu ya Bakari na mwisho ya Kibwana au kama ulimwengu ulivyozowea kumwita, Farouk. Wale wote ni wanawe. Kabisa hakuweza kupotewa na damu yake. Maiti ya Fumu ililala kichalichali ikitazama mbingu nyeusi na kukoga mvua iliyomwaika; ya Bakari imelala kifudifudi, kabisa imekataa kuipa uso dunia iliyomcheza

> toka kuzaliwa. Maiti ya Pandu imejipeta kwa unyonge kuilalamikia dunia iliyomdhulumu, na Kibwana, maiti yake iliuma ardhi na kuiomba msamaha kwa vile ilivyokuwa akiikanyaga kwa matakuro na dharau. Mzee Jaku aliinua uso, akamtazama masika, aliyekuwa katekwa kama simba mkali; tena aliangusha chini uso wake na kutazama maiti ya Kibwana, ah, zuio la nafsi yake lilipigwa kumbo na huzuni ya msiba iliyojaa tele sasa (uk 120).

Miongoni mwa hali zinazoweza kuzua utanzia kwa msomaji hapa ni hili tukio la kufa kwa pamoja watoto wanne wa familia moja. Ni wazi kuwa mtu ashuhudiaye tukio kama hilo litamstaajabisha na kumhuzunisha kwa sababu si jambo la kawaida kutokea katika jamii. Ithibati nyingine ni ile ya Mzee Jaku na mkewe Masika kupata huzuni kubwa na kubaki kulia baada ya kuziona maiti zilivyolala. Mathalan, maiti ya Fumu ililala kichalichali, maiti ya Bakari imelala kifudifudi, maiti ya Pandu imejipeta kwa unyonge, na maiti ya Kibwana iliuma ardhi na kuiomba msamaha. Huzuni au maumivu huweza kupatikana kwa msomaji kutokana na hali ya unyonge iliyomkabili Mzee Jaku na mkwewe kwa kumiminikwa na machozi na kutojua lipi wafanye. Ni katika wakati huuhuu ndipo tunashuhudia mtunzi, kupitia maisha yake binafsi amewahi kupatwa na msiba wa kufiwa na mtoto wake ambaye alikufa akiwa mdogo sana. Yumkini, kutokana na msiba huo, mtunzi anatupa tajriba ya tukio la kufa kwa mtoto na uzito wa huzuni aipatayo mzazi.

Tukio jingine ambalo mwandishi analisana kwa njia ya kifo linapatikana kupitia kifo cha Bi Tele. Mwandishi analibainisha tukio hili kwa kusema:

> Bila shaka amesikia kifo cha mkewe, na sasa miaka mingapi imepita. Kifo cha mkewe kimemtia huzuni na kumbukizi nyingi; hasa akijua yale aliyokuwa akimtendea. . . (uk 117).

Mwandishi anatujuza kuhusu Mzee Jaku mara alipopata taarifa ya kifo cha mkewe kilichotokea muda mrefu. Taarifa hiyo moja kwa moja ilimhuzunisha na kumweka katika hali ya ugumu ya kukumbuka yale matendo mabaya aliyokuwa akimfanyia

mkewe. Katika kumbukizi hii msomaji anaweza kuhuzunika kutokana kitendo cha mzee Jaku kutomjali mkewe katika huduma za lazima ambapo ndiyo sababu kuu ya kupoteza uhai wake.

Kifo kingine kilichotumiwa na mwandishi ni cha Bi Staghafiru. Tukio hili limebainishwa kama ifuatavyo:

> Jicho la Staghafiru lilipekuka hatimaye; kiini kilipotea na weupe ukastakimu. Alivuta koromo la nguvu na ghafla kichwa kilidenguka. Kinywa wazi. Pandu alipeleka mkono kwenye macho yake akayafumba, kisha kwenye midomo, nayo akaifumba. Akachukua kaniki ya pili na pamoja na ile ya mwanzo alimfunika mlezi wake gubigubi. Hatimaye, mauti yalipata fursa ya kusimama wima juu ya kiwiliwili cha mwanamke huyu – yalikuwa yakikenua, kicheko cha ushindi; yakibainisha athari ya vile vita vilivyomalizika, baina yake na uhai. Tena kwa kejeli yalitoa kidole na kuashiria kiwiliwili baridi cha Staghafiru, yakatangaza matokeo ya ushujaa, Mfu (uk 69).

Jambo linalotazamiwa kuzuka kwa huzuni hapa ni hali ya msomaji anavyoshuhudia namna ya Bi Staghafiru anavyokufa. Mwandishi anaeleza mambo yaliyomtokezea bibi huyu wakati wa kufa ni kugeuka kwa kiini cha macho, kugeuka kwa kichwa ghafla, kinywa kuwa wazi. Pamoja na hayo, mtunzi anaonyesha namna ya Pandu alivyochukua hatua baada ya kifo cha mlezi wake. Hatua zote hizi zinaripua hofu, woga na huruma kwa msomaji. Kama ilivyodokezwa huko nyuma kuwa pia utanzia hujumuisha hisia za woga, hofu na huruma.

Mtunzi ametumia matukio yenye utanzia katika hali ya kulia inayoambatana na machozi. Tukio linalojitokeza ni hili lifuatalo:

> “Niambie, kuna nini Kazija, kuna nini?” alishikilia kwa hisia. Sasa Fumu alionekana waziwazi kwamba kahusika na yote yaliyokuwa yakitokea. Hakuweza kungojea jingine. Lililobaki ni kusikiliza na kukishindikiza kilio cha Kazija, kainama vilevile na mkono upo pale pale begani. Hatimaye Kazija aliregeza kilio. Dakika za kujinyamaza zikapita, na kwa Fumu huu ulikuwa wakati mmoja wapo ambapo, alijiona kazuzuka, hana la kufanya, ila kubaki

> kutumbua macho na kubwaga vineno viwili vitatu vya kumnyamaza Kazija ili amfunulie siri ya kilio chake. Kasi ya kilio kilipungua, ikabaki kwikwi na machozi njia mbilimbili, na katikati ya kushusha pumzi Kazija alikuja juu: "Ame. . . ame. . . u. . . ameuzwa, ameuzwa." . . Kilio kilipanda juu tena (uk 20).

Hapa, kwa mara nyingine tunashuhudia matumizi ya viungo vya mwili wa binadamu katika kutengeneza utanzia. Jambo kuu katika kitushi hiki ni Masika kuozeshwa kwa nguvu na babaake ili aolewe na Fauz. Mtunzi analijengea hoja tukio hili kwa kuonyesha namna ya Masika anavyofungwa kamba za mikono na miguu. Jambo hili lilimliza Kazija. Wasomaji wameweza kuhuzunika kutokana na athari ya kilio cha Kazija. Hii ni ithibati ya jinsi mkabala wa Mwitiko wa Msomaji unavyoweza kuchukua nafasi kutokana na misingi ya tabia zake. Kilio chake ni cha kwikwi ambacho kinapanda na kushuka hali ambayo baadhi ya wasomaji wametoa maoni kuwa wamelia baada ya kukisoma kitushi hiki. Hapa, mwandishi anawasuta wazazi kuachana na tabia ya kuwaozesha watoto wao bila ya ridhaa zao. Ithibati ya jambo hili ni pale babaake Masika anaposema "Masika, sisi tu masikini. Mimi ni nokoa tu na mabwana hawa; huoni kwamba ndoa hii itatufungulia milango ya heri" (uk 21).

Utanzia mwingine wenye kufuatana na kilio umo katika tukio lifuatalo; ambapo mwandishi anasimulia:

> Bakari alipokuwa angali kitoto cha miaka mitano Alikumbuka siku ile aliporudi nyumbani na kilio, amepigwa na wenzake. Alikwenda moja kwa moja hadi kwa mamaake aliyekuwa kalala kwenye mayowe. Alimlilia, akamkumbatia, akamparamia, akamshtakia maonevu aliyokutishiwa nje; lakini mamaake hakufurukuta, hakuinuka wala hakufungua jicho; naye Bakari alipoona yule mtetezi wa haki zake, yule mwonelezi wa machungu yake, yule mkidhi wa haja zake hakujali, amempuuza moja kwa moja, alijitupa chini na kugaragara; akalia na kulia hata kifua chake kikaroa machozi, na hatimaye alipata usingizi na kulala. Baadaye, Bakari aliona kibanda chao kimejaa watu waliolia na kuomboleza; naye alijiunga nao akalia kwa uchungu kwa nini mamaake hakuinuka kumwitikia na kwa nini hakuinuka kuwafurusha wale watu walioleta udhia wa kilio kibandani mwao. Naye hakumuona tena mamaake mpaka leo mtu- mzima (uk 40).

Mhusika anayetwishwa kisa hiki ni Bakari. Mtunzi anakisimulia kilio cha Bakari kwa mtindo wa kutia chumvi na takriri. Ametaja kuwa akalia na kulia hata kifua chake kikaroa machozi. Shabaha iliyopo katika kitushi hiki ni kuonyesha namna kilio hicho kilivyotoa hisia kubwa ya huzuni kwa Bakari mbele ya mamaake. Huzuni ilimzukia kwa mambo mawili. Jambo la kwanza ni kule kupigwa na watoto wenzake. Jambo la pili ni kutopata mwitiko kwa mamaake kwani tayari ameshafariki. Kwa mujibu wa utafiti huu, pamoja na shabaha hizo Said Ahmed Mohamed anataka kuwafanya wasomaji wake waingiwe na jitimai moyoni mwao. Inatarajiwa kuwa msomaji anaweza kupata mwitiko kutokana na matendo ya mhusika aliyepo.

Utanzia mwingine katika mazingira ya kilio ni tukio la Mzee Jaku. Kama ilivyodokezwa huyu ni mzee mwenye watoto wanne. Mwandishi anasema:

> Mzee Jaku aliinua uso, akamtazama Masika, aliyekuwa katekwa kama simba mkali; tena aliangusha chini uso wake na kutazama maiti ya Kibwana, ah, zuio la nafsi yake lilipigwa kumbo na huzuni ya msiba iliyomjaa tela sasa, alianguka na kuitapakaa damu ya watoto wake iliyokuwa ikichanganyika kwenye mkondo wa maji. Alilia. ‘Masikini damu yangu . . . aaaa, masikini wanangu . . . hivi ndivyo ulivyonipokea ulimwengu? (uk 120 – 121).

Tukio hili linasawiri hali ilivyokuwa baada ya kufa kwa watoto wanne wa mzee Jaku. Hii ni baada ya kujuta makosa yake aliyoyatenda kwa familia yake. Hata hivyo alidhamiria kuwatafuta watoto wake. Dhamira hiyo ilikatishwa baada ya kuziona maiti za watoto hao. Katika tukio hili, utanzia unakamilishwa na tukio la kulia kwa mzee Jaku na Masika. Hivyo, mtunzi kupitia tukio hili, anaidokeza hadhira yake kuhusu umuhimu wa kujuta makosa na kuwa na mapenzi ya dhati kwa watoto. Yumkini, dhana ya majuto hapa inaturejesha katika maisha ya mtunzi na mfumo wake wa dini ya Kiislamu. Dini yake inamfunza umuhimu wa kujuta na kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu na kwa wanadamu ambao amewakosea.

Tukio jingine la kilio ni hili ambalo anapofariki Bi Staghafiru. Mwandishi anasimulia:

> Pandu hakujibu kitu, aliwatazama watu waliomzunguka machoni Mzee Siwa kwa muda, tena aliwatazama watu waliomzunguka, akatangaza: ‘Mama ame . . . amekufa, Bi Staghafiru.’ Aliangua kilio kikubwa (uk 71).

Mwandishi moja kwa moja amemtaja Pandu na mkasa wake wa kulia. Jambo lililomfanya Pandu kulia ni baada ya kufariki mlezi wake. Mwandishi ametia chumvi katika kukisimulia kilio hicho. Hilo limefanywa na msimulizi- mwandishi ili kuonyesha ukubwa wa huzuni ya Pandu. Kwa hiyo, hali ya kujiwa na huzuni kwa msomaji kutoka katika kilio cha Pandu ni yale mazingira ya kulia ambayo imeletwa kwa njia ya kiutendaji.

Tukio lifuatalo linamhusisha Fauz akimtesa mfanyakazi wake. Mfanyakazi huyo ni Fumu. Mwandishi anatufafanulia kwa kusema:

> Fauz alikunja uso na kupandisha nyusi, akakweza bunduki juu na kuelekeza mdomo kwenye paa la kibanda cha Fumu. Hapo alivuta sefu. Bunduki ilialika kwa mshindo mkubwa na kutawanya marisau kwenye paa la makuti. Hapo hapo Roket, aliachiwa na kutomezwa, alitimka huku akibweka kwa ghadhabu na kutumbukia kibandani mwa Fumu. Mlikuwa na mtafaruku kibandani mwa Fumu. Utukutu ulimwisha. Muda si muda, alianza kupiga kelele za uombezi, “Nani? Nani? We, unataka nini? Kuna nini?” Ni maswala yaliyomwenda midomoni mbiombio. “Jibwaaa! Toka, toka, wacha, niwacheee!” lakini Roket aliendelea na kazi aliyoamrishwa. “Wu, wu, wu”, alibweka huku akimparamia Fumu na kuzidi kumrarulia mararu yake. Ndani hamkua na salama na pale Fumu alipoupata upenyu, alipenyuka – nje, na kelele zake, huku Roket ananing’inia kwenye mkia wa raru la shati lake (uk 6).

Hapa inasawiriwa hali ya kutumia mateso dhidi ya wengine. Mtunzi ameonyesha jinsi ya Fauz anavyojichukulia sheria mikononi mwake kwa kumuadhibu Fumu. Ametumia bunduki na mbwa katika kuyatekeleza mateso hayo. Msomaji.anaweza kujiwa na utanzia wa kiakili baada ya kuona hasara anayoipata Fumu. Hasara

iliyopatikana ni ile ya kubomolewa kwa kibanda chake anachotegemea kimalazi. Jambo lingine ni lile la kutafunwa na mbwa ambapo alisababisha kupata jeraha la mwili pamoja na kuchanwa kwa shati lake. Kwa mara nyingine mwandishi anakemea kuhusu ukandamizaji na unyanyasaji dhidi ya watu wanyonge.

Mazingira mengine ya utanzia katika mateso na adhabu ni tukio la Fumu kuchomewa konde yake. Mwandishi anafafanua:

> "Kaka Fumu, kaka Fumu" . . . maneno ya Kitwana yalimtoka mtawalia, akasita. "Konde yako imeunguzwa moto", aliendelea, "imechomwa; imetiwa moto, hivi sasa watu wanamaliza kuizima, nimetumwa nije nikuite." Kitwana alikuwa bado anahema. "Enn, wamechoma . . . enn, wameichoma!" alinguruma Fumu (uk 91).

Katika tukio hili msomaji anahuzunika kwa mambo yafuatayo: Fumu ni mnyonge, na tegemeo lake la maisha linategemea konde iliyochomwa. Mwandishi anaonyesha namna Fumu alivyotumia juhudi na maarifa ili konde yake istawi vizuri. Kwa mfano alifanya hatua ya ulimaji, upaliliaji, umwagilaji maji kwa matarajio ya kupata mavuno kwa ajili ya chakula. Hivyo, tasnifu hii inaamini kalamu ya Said Ahmed imetumika ili kuvitahayarisha vitendo vya unyanyasaji dhidi ya watu wanyonge. Hali hii inakwenda sambamba na mfumo wa kisiasa alioukuta Said Ahmed Mohamed wakati wa ukoloni ambao uliwapora mali wanyonge hasa ardhi, na kuwaacha katika hali ya umaskini.

### 4.5.3 Matukio ya Kitanzia Katika Riwaya ya *Kiza Katika Nuru*

*Kiza Katika Nuru* ni riwaya ambayo kwa kiasi fulani imeyatumia matukio kadhaa ya kitanzia ambayo yamejitokeza kama ifuatavyo:

Tukio lifuatalo linaakisi kilio kinachoambatana na machozi

> Katika taathira ya utendi, uso wa mamaake ulipopwaya na macho yalipoanguka kwa huzuni na mboni zake nyeupe zilizopagaa zinapolengalenga machozi, mapafu ya Mbishi yalisunyaa kumziba

> pumzi. Sauti ya mama ake ilipoburutika kuonyesha kuvumilia kwake shehena ya maonevu, moyo wa Mbishi uligutuka na kupiga beni na pale macho ya mamaake yalipowiva na kupukutisha machozi, Mbishi alijiona hawezi, hawezi tena kustahamili. Alibanduka kwa hasira zilizokamatana na huzuni kwenda kichochoroni kujibanza na ukuta, kuyaachia huria machozi yake yatiririke ukomo wa kutitirika, kujibisha kilio cha mamaake na kulani kitendo cha kumtia mamaake msumari wa moto juu ya kidonda chake kibichi (uk 34).

Licha ya kijichomoza kwa kilio katika tukio hili, vilevile mwandishi anapenyeza tabia ya watoto kuwaudhi wazazi wao. Anamwonesha Mbishi jinsi ya utukutu wake wa kuchora ukuta wa nyumba yao jambo ambalo huwa anakatazwa mara kwa mara na mamaake. Hali hiyo inamkera Kudura na kumfanya apatwe na unyonge kwa kutumia kilio kutokana na makero na utundu wa mwanawe. Unyonge aupatao Kudura unaweza kupenya katika akili za wasomaji na kujikuta katika hisia ya unyonge. Hatimaye, kuweza kumfanya awe na huzuni.

Vilevile, kuna tukio jingine la kilio. Mwandishi anasema:

> Akalia, akalia kwa muda mrefu huku akiuacha uso wake ukoge milizamu ya machozi yaliyompukutika njia mbilimbili. Kamasi nyembamba zilimkatika, akawa anazifuta kwa mkono wake bila ya kujali. Ilikuwa kama Mbishi kenda kuchimba chemchem mpya ndani ya macho ya mamaake. Machozi hayakuwa na kizuizi. Kudura alilia kwa shaki, kwikwi na kekefu (uk 55).

Tendo la kulia ni la Kudura na Mbishi. Kudura analia kutokana na vitendo anavyofanyiwa na mwanawe Mbishi. Mwandishi anavitaja miongoni mwa vituko hivyo ni kile cha kumtapikia Kudura. Mbishi alilia kutokana na kujuta kwa yale aliyomfanyia mamaake wakati akiwa katika hali ya kilevi. Hatimaye, wote walipatwa na majonzi. Pamoja na kuwajenga wahusika wake katika hali ya kulia, utafiti unaona kwamba upo uwezekano wa msomaji kulia kutokana na taathira iliyojengwa kwa wahusika. Kwani kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ina mtazamo wa kuwa usomaji ni fanyiko linaloweza kumbadilisha msomaji na kuwa

tofauti baada ya kuisoma kazi ya fasihi. Hivyo, tunaamini kwamba msomaji anaweza kulia kama alivyolia Kudura.

Aidha, sehemu nyingine inayohusiana na kilio ni pale ambapo Salma alipoiona maiti ya mumewe, ambaye aliuliwa kwa kupigwa kitu kizito kichwani mwake. Mwandishi analigusia jambo hili kwa kusema:

> Salma kwa muda alikuwa kama aliyepigiliwa misumari. Alikodoa macho yake yote, akainua mikono juu pamoja na kandili yake, akapiga usiyahi mkali na kujitupa kwenye kiwiliwili baridi cha Mvita. Akalia, akalia, akalia kwa kugugumka huku kila mara akipiga usiyahi . . . alfajiri ilikwisha ingia (uk 247).

Mwandishi hapa anachora tendo la mauaji linavyozua majonzi. Ameyafunga majonzi kwa mhusika Salma ambaye ndiye aliyeiona maiti ya mumewe. Hili ni tukio la kitanzia kwa sababu ni wazi kuwa Salma alikumbwa na hali ya fadhaa alipobaini mumewe ameuliwa kwa kupigwa kitu kizito kichwani. Bila shaka hali ya kuzua kilio kwa Salma ni kuashiria kuwa amekumbwa na majonzi ya wazi. Hali hii pia huweza kupenya katika hisia za msomaji na kujikuta kama ni yeye ndiye aliyefanyiwa tendo hilo la kuuliwa mtu mwingine.

Upo utanzia ulioambatana na mazingira ya vifo. Said Ahmed analifafanua tukio lifuatalo:

> Mvita alikuwa akiwaza kwa nini wale jamaa aliokuwa akiwangojea hawajafika mpaka sasa wanamuacha yeye na mtoto wake nzigunzigu wanaojiangamiza wenyewe na wengine wanaomtambaa yeye. Lakini wakati huu ndipo Mvita alipohisi pigo kubwa la kichwa- nyota nyingi na vimulimuli na halafu kiza cha moja kwa moja (uk 247).

Mvita ni kijana aliyejitolea katika kupambana na viongozi wasaliti akiwemo baba ake. Katika juhudi zake hizo, zilisitishwa kwa kuuliwa na wapinzani wake. Mauaji haya yalipangwa na babaake mzazi Bwan Juba. Mtekelezaji wa mauaji ni Shazia na

wenzake wanne. Miongoni mwa hali zinazoweza kuzua utanzia kwa msomaji hapa ni hali ya kuona namna ya mtu anavyouliwa. Mauaji yalitokea kwa kupigwa kitu kizito juu ya kichwa. Hata hivyo, kutokana na mauaji haya mtu anahuzunika na kusikitika kwa sababu kijana aliyeuliwa ni tumainio la jamii nzima. Ikumbukwe kuwa katika mfumo wa kisiasa, Said Ahmed Mohamed amebahatika kuushuhudia utawala wa kikoloni pamoja na utawala baada ya kuondoshwa kwa mkoloni. Hivyo anatumia uzoefu huo alioushuhudia kwa kukijenga kitushi hiki ili kuwaumbua viongozi wasaliti wanaojaribu kupanga mikakati ya kuzima juhudi za watu wazalendo wenye dhamira ya kuikomboa jamii yao.

Tukio jingine linalohusiana na kifo ni pale mwandishi anavyoudokeza mkasa ufuatao:

> Taarifa rasmi tuliyopata sasa hivi kutoka gerezani kwa mshtakiwa Kudura Abdullah aliyekuwa kawekwa rumande huko gerezani hadi hukumu yake itakapotoka, amejiua jana usiku (uk 258).
> .

Mazingira ya kutokea kwa kifo hiki ni ya kujinyonga. Kudura alihisi haki na usawa havipatikani kutokana na utawala uliopo, ndipo alipochukuwa maamuzi ya kujiua. Tendo la kujinyonga linaweza kutokana na kupoteza kwa uhai wa kudura ambaye ni mhusika aliyejitolea katika kupigania haki kwa wanyonge dhidi ya wakandamizaji. Hali kadhalika, kitendo cha kujiua kwake kimesababisha watu wake wa karibu na jamii kwa ujumla kuhuzunika kwa kumkosa mpiganiaji wao.

Licha ya utanzia huo, Said Ahmed Mohamed ametumia mazingira mengine ya upigaji. Mazingira haya yanamuhusu Bwan Juba na Kudura. Mwandishi anasema:

> Mama ameachwa na baba na amepigwa na kutolewa nyumbani kwa rakadha na damu zinamchururika (uk 156).

Huu ni utanzia wa kimwili. Kipigo ni jambo linalotia machungu kwa mtu. Hali ya mwanamume kuchukua maamuzi ya kupiga hadi kutoa madhara ya mwilini ni tendo

linapotokea huweza kuamsha huzuni kwa wanaoshuhudia. Kwa mfano, msomaji anapojenga taswira ya jinsi Bwan Juba alivyompiga mkewe na kumfukuza ndani ya nyumba yake huku akiacha majeraha huweza kutoa majonzi ya wazi. Hapa, mtunzi bado anaendelea kutoa kilio chake kwa mfumo dume. Anaona kuwa kuendelea kuwepo kwa mfumo huu huyaviza maendeleo ya wanawake.

Ufuatao ni utanzia unaohusika katika mazingira ya gerezani ambao unamuhusu Salma. Tukio lenyewe ni hili:

> Taathira ya mambo ilikuwa kubwa kwa Salma katika kijichumba kidogo cha gereza. Kuta nne zilizokwenda juu zilimfanya ajione kama mnyama mkali aliyetiwa katika tundu madhubuti kwa usalama wa watu wa nje au alikuwa kama ndege mdogo kwenye tundu kubwa, aliyefungwa kwa maslahi ya mtu mmoja kucheza na kustareheshwa naye. Salma aliemewa na mambo mengi kwanza kisa na sababu iliyomfanya yeye awepo hapo dakika hii hakuijua; pili, na pengine kubwa zaidi, mauaji ya Mvita. . . Nani aliyemuua Mvita? Tatu ni ukweli kwamba Mvita ndio ameshaondoka wakati ambapo kila mtu alimhitaji, na yeye Salma alimuhitaji zaidi! Kila mtu alimuhitaji Mvita, hata lile buje la mtu liliomo tumboni mwake Salma! Nne ni kujua hatma yake Salma: atatoka humo gerezani au hatoki? (uk 259).

Hili ni tukio linaloweza kutoa hisia za huzuni. Saidi Ahmed Mohamed anawasuta wakoloni kwa namna walivyokuwa wakiwaonea wanyonge kwa kuwaweka gerezani. Lengo la wakoloni ni kupunguza kasi ya watu waliyopata mwamko dhidi ya serikali yao. Katika tukio la Salma kuwekwa rumande kutokana na kesi ya kusingiziwa kwamba amemuua mumewe Mvita. Ukweli wa jambo hili ni Bwan Juba ndiye aliyepanga mkakati wa kumuua mwanawe. Katika usanaji wa tukio hili linatoa hisia za huzuni, kwa sababu mwanamke aliyefungwa ni mjamzito. Hali kadhalika, amewekwa gerezani bila ya kosa lolote. Mwisho chumba alichowekwa ni kidogo sana hali inayoonyesha unyanyasaji wa wazi. Yumkini, mtunzi anaturejesha nyuma katika utawala wa kikoloni ambao uliwaziba vinywa wananchi waliotaka mabadiliko

ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa kuwaweka gerezani ili kuizuia mwamko watakaoupata wananchi wanyonge.

### 4.6 Athari za Matukio ya Kitanzia kwa Wasomaji

Sehemu hii inaeleza kuhusu athari za utumiaji wa matukio ya kitanzia katika kazi za kifasihi kwa wasomaji. Athari hizo tumezigawa katika makundi mawili ambayo ni athari chanya na hasi.

#### 4.6.1 Athari Chanya

Mosi, imesaidia kukuza tafakuri kwa wasomaji. Msomaji licha ya kuisoma kazi ya fasihi hukabiliwa na mawazo lukuki yanayotembea kichwani mwake. Kwa msingi huo, msomaji huweza kuzitoa nje fikra zake wakati asomapo kazi ya fasihi andishi. Utokeaji wa utanzia humsababisha msomaji kuzigandisha fikra na mawazo yake pamoja na kuwa mzingatiaji wa tukio liliopo. Mara nyingi msomaji hupenda kulireja rejea tukio kutokana na majonzi aliyoyahisi. Hii hatimaye, humfanya msomaji kutolisahau kwa mara moja tukio lililomhuzunisha. Mathalani, katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru,* tukio la kuuliwa kwa Mvita ambalo tumekwisha dokeza huko nyuma limeonekana kukumbukwa sana na sehemu kubwa ya watafitiwa. Msomaji anapoendelea kulisoma tukio hilo humjia fikra za kujiuliza maswali kwa nini akafanyiwa jambo lile? Ni jambo lipi lilofanya aonewe? Maswali kama haya huweza kukaa katika kumbukumbu za msomaji.

Pili, imetumika kama nyenzo ya kufikishia ujumbe maalum. Lengo kuu la mwandishi katika kazi yoyote ya fasihi ni kutoa ujumbe fulani kwa hadhira yake. Ujumbe huo huweza kuwa wa kuelimisha, kuonya, kuadilisha, kukosoa na kuonyesha matatizo mbalimbali yaliyomo ndani ya jamii. Mtunzi hufanya uteuzi

wake wa kuchagua mbinu faafu za kibunilizi ili kuzifikisha hisia zake kwa wasomaji. Utumiaji wa utanzia huwa ni kichocheo cha mwandishi katika kuyafikisha makusudio yake. Mathalani, Katika riwaya ya *Utengano,* Said Ahmed Mohamed amelitumia tukio la kitanzia la kupigwa kwa Bi Tamima. Kutokana na kosa la kujifungua bila ya ruhusa ya mumewe. Kipigo hicho kilimsababisha kupata maumivu makali pamoja na kupewa talaka. Kulingana na utafiti uliofanyika tukio hili limebeba: Mosi, unyanyasaji wa mwanamke. Pili, ukosefu wa mapenzi ya dhati na huruma. Tatu, mwanamke ni kiumbe kisichoweza kutoa maamuzi mbele ya mwanamume.

Tatu, imetumika kujenga ujumi wa kisanaa. Fasihi ni kitu cha kiujumi. Ujumi ni uzuri wa kisanaa au ni hali ya kutumia ufundi na ustadi kwa lengo la kuwavutia wasomaji (Langer, 1977). Tukiyachukulia mawazo ya Langer kuwa ujumi hujikita zaidi na fani ya fasihi, tunaona kuwa fani hiyo ina vipengele vya muundo, mtindo, mandhari, wahusika, na matumizi ya lugha pamoja na mbinu mbalimbali za kibunililzi. Imeonekana wazi jinsi Said Ahmed Mohamed alivyoyasawiri masuala mazito kwa kutumia matukio ya kitanzia kama yalivyodokezwa huko nyuma ambayo yanaonyesha ukomavu na ustadi mkubwa aliokuwa nao katika usanaji.

Nne, kujenga upekee wa mtunzi. Inaposomwa kazi fulani ya fasihi inawezekana kumwona mtunzi wa kazi hiyo akitofautiana na mtunzi mwingine. Jambo moja linaweza kuongelewa na wasanii wawili tofauti lakini namna linavyowasilishwa likatofautiana, na hii ni kulingana na upekee wao wa kimtindo. Senkoro (1982) anashadidia kwa kusema kuwa mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia ambayo hutokeza au huonyesha nafsi na labda upekee wa mtungaji wa kazi hiyo. Anaongezea kuwa mtindo hubainishwa kwa vipengele vitatu; ambavyo

ni mbinu za kibunilizi, uteuzi wa maneno na uhusika na wahusika. Mwandishi Said Ahmed Mohamed katika uteuzi wake wa matukio ya kitanzia ameyaunda kwa muundo wa kipekee. Mathalani, matukio ya kitanzia yanayohusiana na vifo. Aghalabu, yanaishia kwa kutaja tukio hilo tu bila kulipeleka katika taratibu za kimazishi. Kama ilivyojitokeza katika tukio la Mvita kuuliwa (*Kiza Katika Nuru*), tukio la kufa kwa Bwana Maksuudi (*Utengano*) na tukio la kufa kwa watoto wanne wa Bwana Jaku (*Dunia Mti Mkavu*) Matukio yote haya yanaishia katika kusimulia vifo vyao tu, bali mtunzi hakuonyesha namna ya kufanyiwa mazishi. Kutoonyeshwa kwa taratibu za mazishi ni mtindo wa mtunzi.

Tano, kuihuzunisha hadhira. Msanii mahiri katika kazi za fasihi andishi ni yule anaeziteka hisia za wasomaji wake. Utumiaji wa mbinu za kibunulizi ni sehemu mojawapo ya kufikia lengo la kuziteka nafsi na hisia za wasomaji. Kupitia hali za kuwaliwaza, kuwahuzunisha, kuwasikitisha, kuwanyongesha na kuwafanya wawe na huruma. Hali hizi huchimbuka kutokana na ustadi mzuri wa kuyajenga matukio ya kitanzia katika miktadha mbalimbali. Utafiti umegundua kuwa Said Ahmed Mohamed, katika ujengaji wake wa utanzia amesababisha baadhi ya hadhira kuhuzunika kwa kutokwa na machozi au kuyasikitikia matukio hayo. Yumkini, msomaji anapotokwa na machozi au kuwa na masikitiko, huweza kuchukuliwa kuwa lengo la mwandishi limefanikiwa.

### 4.6.2 Athari Hasi

Mosi, inachangia katika kutoa maamuzi mabaya. Kutokana na matukio ya kitanzia, msomaji huweza kupandwa na jazba na kutoa suluhisho ambalo linaweza kuleta madhara juu yake. Pia, huweza kuwashajihisha wasomaji kutekeleza matukio kama walivyoyasoma. Mathalani, tukio la kujiua kwa Kudura pamoja na lile la Bwana

Maksuud la kumpiga mkewe kwa kutumia ukanda. Hali kama hizi zaweza kutekelezwa na wasomaji baada ya kumaliza usomaji wa kazi ya fasihi. Hoja hii imetiliwa nguvu na mhimili mmojawapo wa nadharia ya utafiti huu unaosema kuwa kazi ya fasihi iwe na maana kufuatana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia. Kwa hiyo, uchukuliaji wa msomaji unaweza kuwa na manufaa kwake au kwa kuleta maafa.

Pili, kumkatisha tamaa msomaji. Usomaji wa kazi za fasihi unahitaji ujasiri na moyo ili faida ya kusoma ipatikane. Matumizi ya utanzia yanaweza kumtoa msomaji katika uendeleaji wa kukisoma kitabu. Hii ni kutokana matukio yote ya kitanzia huwa na lengo la kumhuzunisha msomaji. Hata kuweza kumkatisha mara moja na usomaji wake. Mathalani, msomaji anaweza kulia baada ya kukumbana na tukio la kuhuzunisha au ahusishapo na matukio halisi aliyowahi kukumbana nayo katika maisha yake. Hatimaye, ikamfanya asimamishe zoezi la kusoma kitabu.

## 4.7 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imeeleza kwa kifupi kuhusu mawazo ya jumla ya riwaya zetu teule; ambazo zimetusaidia kupata uelewa kwa yale yaliyokusudiwa na mwandishi. Vile vile, tulieleza miktadha mbalimbali iliyomsukuma mwandishi ili kuihusisha na utokeaji wa utanzia katika kazi zake. Miktadha hiyo ni wa kidini, lugha, kitaaluma, kiuandishi na kisiasa. Humo tulimmurika mtunzi kwa hatua zake za kimaisha aliyoyapitia ambayo yanakwenda sambamba na uteuzi wake wa kutumia utanzia katika kazi zake za kifasihi.

Pia, tulieleza utokeaji wa matukio ya kitanzia ambapo tulibaini utanzia uliomo katika bunulizi teule za Said Ahmed Mohamed umejitokeza katika maeneo mbalimbali

yakiwemo ya adhabu, mateso, kipigo, ajali, vifo, vilio, maradhi, na ufungwa. Mwisho, tumefanya mjadala kuhusu athari za matukio ya kitanzia. Athari hizo tumezigawa katika makundi makuu mawili ambayo ni athari chanya na athari hasi. Kwa upande wa athari chanya ni kukuza tafakuri kwa wasomaji, nyenzo ya kufikisha ujumbe maalum, kujenga ujumi wa kisanaa, kujenga upekee wa mtunzi, na kuihuzunisha jamii. Upande wa athari hasi ni kuchangia kutoa maamuzi mabaya, na kukatishwa tamaa kwa msomaji.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho la utafiti. Imegawika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza inaeleza muhtasari wa tasnifu. Sehemu ya pili inaeleza utoshelevu wa nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa data. Sehemu ya tatu inafafanua mchango mpya wa utafiti. Sehemu ya nne inatoa maoni ya utafiti. Sehemu ya tano inataja mapendekezo kwa tafiti zijazo.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti ulilenga kuchunguza mbinu ya utanzia. Katika kuichunguza mbinu hii, mtafiti aliyapigia mbizi matukio mbalimbali ya kitanzia katika riwaya teule tatu za Said Ahmed Mohamed ambazo ni *Utengano*, *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru*. Utafiti umegawika katika sura tano. Kila sura imefafanua vipengele maalum vya utafiti.

Sura ya Kwanza inaeleza usuli wa tatizo la utafiti. Vilevile, imeeleza historia ya mwandishi tangu kuzaliwa kwake hadi uandishi wake. Pia, inaeleza mambo kama vile manufaa ya utafiti na nadharia teule ya utafiti. Mwisho, sura hiyo imemalizia kueleza mipaka ya utafiti. Sura ya pili imechambua mapitio ya maandiko mbalimbali ya vitabu. Ikijumuisha majarida, mitandao ya wovuti, makala za waandishi pamoja na tasnifu za wataalamu mbalimbali. Maandiko hayo yaligawanywa sehemu mbili; yale yanayozungumzia utanzia katika kazi za fasihi pamoja na yale yanayozungumzia utanzia katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Kwa kiasi kikubwa, mapitio hayo yametusaidia kupata faida ya kuieleza kwa kina mada husika ya utafiti na kubaini mapengo ya utafiti. Sura ya tatu ilibainisha mbinu na vifaa

mbalimbali vilivyotumika katika utafiti. Tulivipitia vipengele kama vile mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti (jamii ya watafitiwa na sampuli ya watafitiwa), mbinu na zana za kukusanyia data pamoja na vikwazo vya utafiti.

Sura ya nne imejadili matokeo ya utafiti. Hapa imechambuliwa miktadha mbalimbali ya maisha ya mtunzi ambayo imemsukuma katika kuutumia utanzia. Miktadha hiyo ni kama vile wa mfumo wa dini, lugha ya Kiswahili, taaluma, uandishi wa zama hizi na mfumo wa kisiasa. Pia, tumebainisha aina za utanzia ambazo ni utanzia wa kimwili na kiakili. Aidha, tumetoa ufafanuzi wa kina kuhusu matukio mbalimbali ya kitanzia miongoni mwao ni adhabu, mateso, kipigo, vifo, vilio na ufungwa. Mwisho tumehitimisha mjadala kwa kufafanua athari wazipatazo wasomaji kutokana na matukio ya kitanzia. Humo zilibainika athari kama vile kukuza tafakuri kwa wasomaji, nyenzo ya kufikisha ujumbe maalum, kujenga ujumi wa kisanaa, kujenga upekee wa mtunzi, kuihuzunisha jamii, inachangia katika kutoa maamuzi mabaya na kukatisha tamaa kwa msomaji. Sura ya tano ni hitimisho la tasnifu nzima ya utafiti. Hapa panahusika vipengele kama vile muhtasari wa jumla kuhusu utafiti wetu, utoshelevu wa nadharia ya utafiti, mambo mapya tuliyoyagundua, maoni ya utafiti pamoja na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

## 5.3 Utoshelevu wa Nadharia Katika Utafiti

Nadharia iliyotumika katika kuchambua data za tasnifu hii ni Mwitiko wa Msomaji. Nadharia ilisaidia kupata maana za matini kwa kuyagundua matukio mbalimbali ya kitanzia pamoja na athari zake. Hii ni kutokana na suala la msingi kuwa nadharia hii inampa uhuru msomaji wa kutoa mawazo yake kulingana na mielekeo yake binafsi. Kwa ujumla, upokezi wa watafitiwa umetupa ithibati ya kuwa matokeo ya utafiti huu umekidhi kiwango kulingana na malengo yetu.

## 5.4 Mchango Mpya wa Utafiti

Mambo mapya yaliyoibuliwa tasnifuni ni haya yafuatayo: Jambo la kwanza ni dhana ya utanzia. Tunaona kwamba dhana hii imetokana na dhana ya msingi ya tanzia inayohusishwa na utanzu mkongwe wa tamthiliya. Inaonekana wazi kuwa utanzia ni dhana jumuifu yenye kujengwa na mambo maalum (mateso, ajali, maradhi, kifo, kifungo, na ulemavu) ambapo ujenzi huo huweza kutoa matokeo ya huzuni au kilio au hata maumivu.

Jambo la pili ni athari za utanzia kwa wasomaji. Kama tulivyodokeza lengo kuu la utanzia ni kuihuzunisha jamii. Licha ya kuwapo kwa lengo hilo, tumegundua kuwa matukio ya kitanzia katika kazi za fasihi huwa na faida na hasara zake. Zikiwemo kukuza tafakuri kwa msomaji, nyenzo ya kufikishia ujumbe maalum, kujenga ujumi wa kisanaa, kujenga upekee wa mtunzi, kuihuzunisha hadhira, inachangia katika kutoa maamuzi mabaya, na hukatisha tamaa kwa msomaji.

Jambo la tatu tuliloligundua linahusu sababu zilizomsukuma Said Ahmed Mohamed atumie mbinu ya utanzia. Sababu hizo ni kuwepo kwa dini ambapo ndani yake ameyashuhudia matendo mazuri na mabaya yanayotekelezwa na waumini wake. Si hilo tu bali pia, lugha yake ya Kiswahili ambayo ilimuezesha kupangilia maneno kwa njia ya kuhuzunisha. Pia, mapitio yake ya kielimu ambayo yalimwezesha kujifunza taaluma mbalimbali ikiwamo ya fasihi. Vilevile, kuwepo kwa uandishi wa zama hizi ambao kwa namna moja ama nyingine uandishi huo ulijaribu kuikeng'euka mikatale ya kikanuni. Humo ameweza kutumia mitindo mipya kama ule wa uhalisia mazingaombwe na ushirikina. Mwisho, ni mifumo ya kisiasa aliyokutana nayo ambayo ni mfumo wa siasa za kikoloni na baada ya ukoloni ambapo alivijenga vitushi vyake ili ayasawiri maudhui yake kulingana na mifumo hiyo.

## 5.5 Maoni Kuhusu Utafiti

Kutokana na utafiti uliofanyika kuna maswala mbalimbali ambayo yalionwa na kupaswa kutolewa maoni; ambapo jambo kubwa zaidi ni kupooza kwa taarifa za Said Ahmed Mohamed miongoni mwa Watanzania. Kwa hiyo, ni vema kuwe na azma ya kumtangaza Said Ahmed Mohamed. Taasisi za elimu kama vile vyuo na shule zinapaswa kumtangaza nguli huyu hapa nchini Tanzania na duniani kwa ujumla. Kwa kuwa ipo dhana iliyojengeka kuwa utaifa wa mwandishi huyu ni Kenya hali ambayo si kweli. Hii imetokana na jamii ya Watanzania kutompa thamani na heshima. Hivyo, juhudi zifanyike katika kutoa machapisho mbalimbali yanayomhusu yeye kielimu, kifamilia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

## 5.6 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo

Utafiti huu ulihusu "Matumizi ya Utanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed". Licha ya ugunduzi wa mambo mapya yaliyojitokeza ndani yake. Kiutafiti, bado kuna maeneo muhimu yanayohitaji kuchunguzwa zaidi ambayo kwa namna moja ama nyingine hatukuyashughulikia kutokana na kubinywa na malengo ya utafiti wetu. Hivyo, tunapendekeza maeneo yafuatayo yafanyiwe utafiti zaidi:

a) Utafiti kuhusu utanzia unaweza kufanywa kwa mtunzi mwingine. Kama vile Shafi Adam Shafi, Faraji Katalambula, Muhamed Suleiman Abdullah, Shaaban Robert, Euphrase Kezilahabi na wengineo. Ama kwa kuwalinganisha na kuwalinganua watunzi hao.

b) Utafiti ufanyike katika matumizi ya utanzia kwa kuzihusisha tanzu nyingine za fasihi. Tanzu hizo zinaweza kuwa ushairi, tamthiliya, hadithi, semi na sanaa za maonyesho.

## MAREJELEO


Abrahams, M.H. (1993), *A Glossary of Literary Terms.* 6th Edition, Harcourt and Brace, NewYork.

Atwood, M. ( 1982), *Second Words: Selected Critical Prose*,Toronto Anansi.

Babbie, E. (1992), *The Practice of Social Research (6th Edition),* Wadswarth Publishers, Belmount.

Bakhresa, S.K. (1992), *Kamusi ya Maana na Matumizi,* Oxford University, Dar es Salaam.

BAKIZA. (2010), *Kamusi ya Kiswahili Fasaha,* Oxford University Press, Nairobi.

Bastide, R. (1978), *The African Religious of Brazili,* The John's Hospkins University Press, Baltmore London.

Bertoncini, E. (1989), *Outline of Swahili Literature* (*Prose, Finction and Drama*), E. J. Brill, Leiden.

Borg, W. (1989), *Educational Research: An Introduction,* Longman, London.

Charles, C. (1995), *Introduction of Educational Research, Second Edition,* Longman, New York.

Chiraghdin, S. (1977), *Historia ya Kiswahili,* Oxford University Press, Nairobi

Encyclopedia Britanica, Inc (1911), Volum II, Chicago.

Enon, C.J (1998), *Educational Research Statistics and Measurement,* Makerere University, Kampala.

Gibbe, A.G (1980), *Shaaban Robert Mshairi,* Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Gombers, H.M.A. (1970), *Literature and Criticism,* London Chatto and Windus Publishers.

Hamad, H.A. (2007), "Lugha ya Kificho Katika Kazi za Said Ahmed Mohamed", Tasnifu ndogo ya Kukamilisha Mafunzo ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Haijachapishwa).

Haule F.C na Feslas T.K. (2011), *Nadharia ya Ukalimani Sekondari na Vyuo,* Peramiho Printing Press, Songea.

Islam, I.K na Wenzake. (2009), *Dhibiti PTE Kiswahili*, Oxford University Press, East Afrika Ltd.

Jieikobu. (2012), "What are Some Characteristics of Tragedy in Literature", Iliyosomwa 05/102014 katika http//www.answers.yahoo.com

John, P. (h.t) “Music and Tragic Affirmation”, Iliyosomwa 07/09/2014 katika http//www.protevi.com/john

Kamunde, M.E. (1983), “Kilio cha Wanyonge Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed”, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Khaemba, S.S. (1999), “Ulinganisho wa Maudhui ya Mapinduzi Katika *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru”*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kiango J.G na Wenzake (2007) *Kamusi ya Shule za Msingi*, Oxford University Press, Nairobi.

King’ei, K. (2004), “Fantansy and Realism in the Modern Kiswahili Novel: A Critical Look at *Babu Alipofufuka* Said Ahmed Mohamed” Katika *Kiswahili*. Juz. 67 TUKI. Dar es Salaam.

Kombo, D.K na Tromp, D.L.A (2006), *Proposal and Thesis Writing: An Introduction,* Panlines Publications Africa, Nairobi.

Kothari, C.R. (2004), *Research Methodology: Methods and Techniques (2$^{nd}$ Edt),* New Age International Publishers Ltd, New Delhi.

Kumary, R. (1999), *Research Methodology Step Guided for Beginner,* New Delh.

Langer, S.K. (1977), *Feeling and Form*, Longman.

Ligopola, M. (2012), “Nafasi ya Mwanamke Katika Nathari Teule za Said Ahmed Mohamed: Je, Ni Kumkweza Au Kumbeza”, Tasnifu ya Kukamilisha Shahada ya Uzamili katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Longhorn (2009), *Kamusi Kamili ya Kiswahili,* Longhorn Publishers, Nairobi.

Longman (1978), *Dictionary of Contemporary English*, Cayfosa Quebecor, Bercelona.

Macha, N.E. (2013) “Matumizi ya Vilio na Vicheko”, Iliyosomwa 21/07/2014 katika http//www.tunuzakiswahili.blogspot.com.

Madumulla, J.S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi,* Mture Educational Publishers Ltd, Dar es Salaam.

Magaju J. (2004), “Uhalisiajabu kati ya Riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) ya SA Mohamed na *Bina-Adamu* (2002) ya K.W. Wamitila”, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, (Haijachapishwa).

Matteru, M.L. (1976), *Fani ya Hadithi: Riwaya,* Kioo cha Lugha.

Mdee J.S na Wenzake (2011) *Kamusi ya Karne ya 21*, Longhorn Publishers, Nairobi.

Mhilu, G. na Wenzake (2008), *Tahakiki Vitabu Teule vya Fasihi Kidato cha 3 na 4 Nadharia, Uhakiki na Maswali,* Nyambari Nyangwine Publishers.

Mkubwa, C.M. (2000), "Dhima za Utani Katika Mazishi na Matanga ya Wapemba na Athari Zake kwa Jamii", Ripoti ndogo ya Utafiti Iliyowasilishwa kwa Masharti ya Kutunukiwa Shahada ya Sanaa (Ualimu), Chuo Kikuu Cha Waislamu Morogoro.

Mlacha, S.A.K. (1987), "*The Identification of Personality Differences in Kiswahili Prose," Swahili Forum*, Toleo la 54, uk 78.

Mligo, E.S. (2012) *Jifunze Utafiti, Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti Yenye Mantiki,* Dar es Salaam.

Mogere, O.G. (2003), "Uhakiki wa Riwaya za Ahmed Mohamed Katika Misingi ya Kifeministi", Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mohamed, S.A .(2010), *Nyuso za Mwanamke,* Longhorn Publishers, Nairobi.

_______________ (1978), *Asali Chungu,* Shungwaya Publishers, Nairobi.

_______________ (1990), *Tata za Asumini,* Longhorn Publishers, Nairobi.

_______________ (2001), *Babu Alipofufuka,* Jomo Kenyata Foundation, Nairobi.

_______________ (2002), *Dunia Mti Mkavu,* Longhorn Publishers, Nairobi, Kenya.

_______________ (1988), *Kiza Katika Nuru,* Longhorn Publishers, Nairobi.

_______________ (2006), *Dunia Yao,* Oxford University Press, Nairobi.

Mohamed, M.A na Mohamed S.A. (1998), *Kamusi ya Visawe,* Hi- Tech Typesetters, Nairobi.

Moore, T.S. (1920), *Tragic Mother,* London.

Msokile, M. (1992), *Misingi ya Hadithi Fupi,* Dar es salaam University Press, Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1983), "Utafiti wa Fasihi Simulizi" Katika *Fasihi,* Uk 1- 25, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi ya Kiswahili.

Mulokozi, M.M. (1996), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili,* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Mushengyezi, A. (2003), *Twentieth Century Literary Theory,* Makerere University, Kampala.

Mzandi, B.M. (2011), "Nafasi ya Utani wa Msibani na Harusini Katika Kabila la Wadigo" Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Njogu, K na Chimerah (1999), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Njogu, K na Wafula, R.M. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Sai Industries Limited, Nairobi.

Nocera, P. (2005) "An Interpretation of Said Ahmed Mohamed's Novel *Kiza Katika Nuru* And Some Aspects of Translation". *Swahili Forum.* Toleo la 12, uk 74.

Nshubemuki, L. (2004), *Misingi na Maarifa ya Utafiti*, Dar es salaam University, Dar es Salaam.

Ntarangwi, M. (2004), *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Augustana College, Rock Island, IL 61201.

Ponera, A.S. (2010), "Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana yake, Sababu za kutumiwa, na Athari zake kwa Wasomaji," Tasnifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Ponera, A.S. (2014), "Ufutuhi Katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi," Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Preston, B. (2014), "Jinsi Mandhari Yanavyoendeleza Maudhui Katika Tamthiliya ya Ebrahim Hussein ya *Mashetan*i", Tasnifu ndogo ya shahada ya Kwanza ya Usanaa na Ualimu, Chuo Kikuu cha Makerere (Haijachapishwa).

Said, A.A. (2007), "Nafasi ya Mwanamke Katika Hadithi Fupi za Mwandishi Said Ahmed Mohamed Ukilinganisha na jamii ya Kizanzibar", Tasnifu ndogo ya Kukamilisha Mafunzo ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Haijachapishwa).

Salim, S.A. (2008), "Fasihi ya Waswahili wa Zanzibar Katika Kazi za Said Ahmed Mohamed," Tasnifu ndogo ya Kukamilisha Mafunzo ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Haijachapishwa).

Saluhaya, M.C na Suleiman M.A. (2012), *Nadharia na Tahakiki ya Fasihi*, STC Publishers, Dar es Salaam.

Senkoro, F.E.M.K. (1987), *Fasihi na Jamii*, Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

________________ (2011), *Fasihi*, Kauttu Limited. Dar es Salaam.

Shilla, A.M. (2012), "Athari za Uhalisia Mazingaombwe Kwa Msomaji Katika Kuzielewa Kazi za Fasihi za Said Ahmed Mohamed", Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Simon, K.L. (2014) "Ishara Katika Kaptula la Karl Marx na Kijiba cha Moyo" Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Soileau, C. (2006) "Money and Tragedy In The Nineteenth- Century Novel" Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi Linganishi, Chuo Kikuu cha Louisiana (Haijachapishwa).

Songoyi, E.M na Masele E.J (2013), *Prose and Poetry: A Teaching Manual*, Heritage Tanzania Education Limited, Dodoma.

Soni, V. (2013), "Theory of Tragedy", Iliyosomwa 10/07/2014 katika http//www.northwestern.edu/class.com

Syambo, B. Na Mazrui, A. (1992), *Uchambuzi wa Fasihi*, EAEP, Nairobi.

Tempeles, P. (1954), *Bantu Philosophy*, Presence Africanize, Paris.

Traore, F.A (2008), " Family and Society In Said Ahmed Mohamed's Novels". *Swahili Forum.* Toleo la 15, uk 64- 65.

TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University Press, Dar es Salaam

Walibora, K. (2010), "Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum*". *Swahili Forum.*Toleo la 17, uk 143-157.

Walter, B (1998), *The Origin of German Tragic Drama*, Verso, London.


Wamitila, K.W. (2003), *Kamusi ya Fasihi ya Istilahi na Nadharia*, Focus Publications Ltd, Nairobi Kenya.

_______________ (2003), *Kichocheo Cha Fasihi Simulizi na Andishi*, Focus Publication, Nairobi Kenya.

Wanjiru J.W (2013), "Uhalisia na Uhalisiajabu Katika Riwaya Mpya *Babu Alipofufuka* (Said Ahmed Mohamed na Watu wa Gehenna (Tomali)", Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

## VIAMBATISHO

### A. Barua Mbalimbali za Kuruhusiwa Kufanya Utafiti



**THE UNIVERSITY OF DODOMA**
DEPUTY VICE CHANCELLOR ACADEMIC, RESEARCH & CONSULTANCY
OFFICE OF GRADUATE STUDIES

P.O. BOX 263
DODOMA, TANZANIA
TEL: +255 23 23002 FAX: +255 23 23000 EMAIL: ahmed_ame@yahoo.com

REF/UDOM/GS/2014/478

Monday, 22 December 2014

**To Whom It May Concern:**

**RE: INTRODUCING MR. HAJI KHATIBU ALI**

The above named student is enrolled at the University of Dodoma for the degree of Master of Arts in Kiswahili Literature with registration number HD/UDOM/527/T.2013

An essential requirement of the study programme is that each candidate is required to submit a dissertation report on a project undertaken within industry and supervised by a member of the University's academic staff. Where possible this project should relate to a practical situation in an organisation or firm selected by the candidate. Students are expected to use their own initiative to identify a possible project and negotiate access with a local firm or organization. The title of study is **"MATUMIZI YA UTANZIA KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED".**

The work may take the form of a survey, ethnography, case studies, etc. Where the report may contain confidential information and its publication could be harmful to the organization, confidentiality is assured by the University. Such reports will be seen only by the Supervisor and Examiner for examination purposes.

I would be grateful if you would provide the student with this opportunity to further his studies while at the same time gaining some useful input for your own organization through the results of the project report.

Sincerely,

Prof. A. M. Ame
**Director of Graduate Studies**

Barua ya uthibitisho wa kuruhusiwa kufanya utafiti (Ofisi ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dodoma, Desemba 22, 2014)

**REVOLUTIONARY GOVERNMENT OF ZANZIBAR**

SECRETARY
ZANZIBAR RESEARCH COMMITTEE
P. O Box 239
Tel: 2230806
FAX: 2233788



**RESEARCH/FILMING PERMIT**
**(This Permit is only Applicable in Zanzibar for a duration specified)**

**SECTION**

| | |
|---|---|
| **Name:** | **HAJI KHATIBU ALI** |
| **Date and Place of Birth** | 25/06/83 |
| **Nationality:** | **TANZANIAN** |
| **Passport Number:** | - |
| **Date and Place of Issue** | **10/02/2015 ZANZIBAR** |
| **Date of arrival in Zanzibar** | - |
| **Duration of stay:** | - |
| **Research Tittles:** | **"MATUMZI YA UTANZIA KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED ."** |
| **Full address of Sponsor:** | **P.O. BOX 3866 - ZANZIBAR** |

This is to endorse that I have received and duly considered applicant's request I am satisfied with the descriptions outlined above.

| | |
|---|---|
| **Name of the authorizing officer:** | **MAWANAISHA A. KHAMIS** |
| **Signature and seal:** | |
| **Institution:** | Office of Chief Government Statistician |
| **Address:** | P. O Box 2321<br>Zanzibar. |
| **Date:** | **10/02/2015** |

Ni utambulisho wa mtafiti wenye lengo la kuruhusiwa kufanya utafiti katika nchi ya Zanzibar. (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar. Febuari 02, 2015)

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

P. O. Box 239
Vuga Street
Zanzibar-Tanzania

Tel. 024 22 30808
Fax. 024 22 30808
E-mail : ps_2vpo@zanzibar.go.tz

---

**OMPR/M.95/C.6/VOL.XIII/** 47 **11/02/2015**

**KATIBU MKUU,**
**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI,**
**ZANZIBAR.**

**KUH: RUHUSA YA KUFANYA UTAFITI**

Kwa heshima, tunaomba uhusike na mada tulioitaja hapo juu.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imemruhusu **Ndugu Haji Khatibu Ali,** Mtafiti kutoka Chuo kikuu cha Dodoma, kufanya utafiti katika mada inayohusiana na "**Matunzi ya Utanzia katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed**". Hivyo tunaomba mtafiti asaidiwe kufanya utafiti wake. Utafiti huo unaanzia 10/02/2015 hadi 30/10/2015.

Tunaambatanisha na kivuli cha kibali cha kufanyia utafiti.

Ahsante,

Wako Mtiifu.

Abdallah

**ASHRAF MOHAMMED ABDALLA**
**/KATIBU MKUU,**
**OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,**
**ZANZIBAR.**

**NAKALA:**
**ND. HAJI KHATIBU ALI**
**ZANZIBAR.**

---

*Kwa mawasiliano ya moja kwa moja:*
*Waziri 024 22 33100; Katibu Mkuu 024 22 30808; Naibu Katibu Mkuu 024 22 31825*

Ni utambulisho wa mtafiti wa kuruhusiwa kufanya utafiti Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar. Febuari 11, 2015)

## B. Miongozo ya Hojaji, Dodoso, Udurusu wa Maktabani na Majadiliano

### B.1 Mwongozo wa Hojaji kwa Mwandishi Said Ahmed Mohamed

**Maelezo**

Huu ni utafiti unahusu ***Matumizi ya Utanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed.*** Tunaomba ushiriki wako ili kupata taarifa sahihi kuhusu utafiti wetu.

a) Nini maana ya Utanzia katika muktadha wa fasihi?

b) Kwa kuwa kila mtu ana historia yake ya maisha. Unaweza kueleza kwa kifupi historia yako ya maisha ikijumuisha uzawa wako, elimu yako, familia yako, kazi zako na uandishi wako?

c) Ikiwa wewe ni mwandishi mahiri, kwa nini unapenda kuandika zaidi katika utanzu wa riwaya kuliko utanzu wa tamthiliya na ushairi?

d) Kwa maoni yako, kwanini watunzi wa fasihi ukiwemo wewe binafsi mnatumia mbinu ya utanzia katika kazi zenu?

e) Kila kitu kina faida na hasara zake. Je unafikiri kuna faida au hasara gani ya matumizi wa utanzia katika riwaya?

f) Wewe ni mwandishi ambaye unatunga riwaya zako kwa kuiangalia jamii yako. Tunaomba utudokeze kuhusu shughuli zako za kijamii, kisiasa, kiuchumi zinavyolandana na uandishi wako hasa katika utumizi wa matukio yenye kuhuzunisha?.

**Ahsante**

**B.2 Mwongozo wa Hojaji kwa Wataalamu na Wahakiki wa Kazi za Fasihi**

**Maelezo:** Tunafanya utafiti kuhusu ***Matumizi ya Utanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed.*** Kwa heshima na taadhima tunaomba ushiriki wako katika kujibu maswali yetu ili kufanikisha lengo la utafiti.

a) Nini maana ya tanzia?

b) Utanzia una maana gani?

c) Kila kitu duniani kina historia na chimbuko lake. Kwa ufahamu wako, ni ipi historia na chimbuko la utanzia katika fasihi?

d) Kila mwandishi ana upekee wake katika utunzi wa kazi ya fasihi. Unadhani Said Ahmed Mohamed ana upekee gani katika maandiko yake ya riwaya?

e) Kwa ufahamu wako utanzia unajengwa kwa mambo gani?

f) Wanataaluma wengi wamezoea kuunasibisha utanzia na tamthiliya. Je una maoni gani kuhusiana na dhana hii?

g) Unafamu nini kuhusiana na mwandishi Said Ahmed Mohamed na matumizi ya utanzia katika riwaya zake?

h) Unadhani kuna maeneo au matukio yoyote yenye kusababisha msomaji apatwe na hisia za huzuni, simanzi, majonzi na masikitiko katika moja ya riwaya ya *Kiza Katika Nuru, Utengano* na *Dunia Mti Mkavu?*

i) Kutokana na kuwapo kwa tukio/matukio ya kuhuzunisha, ni athari gani anayoipata msomaji?

j) Kwa nini waandishi akiwemo Said Ahmed Mohamed hutumia mbinu ya utanzia katika riwaya?

**B.3 Mwongozo wa Hojaji kwa watu wa Karibu Wanaomfahamu Said Ahmed Mohamed**

**Maelezo:** Tunafanya utafiti kuhusu ***Matumizi ya Utanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed.*** Kwa heshima na taadhima, tunaomba ushiriki wako katika kujibu maswali yetu ili kufanikisha lengo letu la utafiti.

a) Unamfahamu vipi Said Ahmed Mohamed?

b) Said Ahmed Mohamed ana asili gani ya uzawa wake?

c) Je unaweza kueleza historia fupi ya Said Ahmed kwa upande wa mamaake?

d) Unamfahamu vipi Said Ahmed Mohamed kwa upande wa babaake?

e) Said Ahmed ana sifa gani katika kuamiliana na watu?

f) Kwa sasa Said Ahmed Mohamed anaonekana ni mtu maarufu sana ndani na nje ya nchi. Kwa maoni yako mambo gani yaliyomsababisha awe maarufu?

g) Katika taaluma ya uandishi, unavutika naye katika eneo gani?

**Ahsante Sana**

**B.4 Mwongozo wa Dodoso kwa Wanafunzi wa Somo la Kiswahili**

Jina la Mtafiti: Haji Khatibu Ali

Mahali pa Utafiti……………………….

Tarehe ya Utafiti………………………

Ndugu mshiriki, utafiti huu unahusu mada ya ***Matumizi ya Utanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed.*** Lengo letu ni kupata taarifa kuhusu miktadha mbalimbali iliyomsukuma mwandishi kutumia mbinu ya utanzia. Pamoja na taarifa zenye kuhusu dhima na athari za kutumia matukio ya kitanzia katika riwaya zake teule. Tafadhali tunaomba ushiriki wako kwani una mchango mkubwa katika ukamilifu wa kupata data.

**Sehemu ya Kwanza**

Tafadhali tunaomba uweke alama ya vema mbele ya kijichumba

**1 Kiwango cha elimu**

Kidato cha tatu ☐ Kidato cha nne ☐ Kidato cha tano ☐

Kidato cha sita ☐ Stashahada ☐ Shahada ☐

2 Riwaya gani kati ya zifuatazo ulizowahi kuzisoma, kuzihakiki au kuhadithiwa

*Asali Chungu* ☐ *Tata za Asumini* ☐ *Utengano* ☐

*Babu Alipofufuka* ☐ *Dunia Mti Mkavu* ☐ *Nyuso za Mwanamke* ☐

*Dunia Yao* ☐ *Kiza Katika Nuru* ☐

**Sehemu ya Pili**

Katika sehemu hii itahusu maelezo mafupi

1 Umejifunza nini katika riwaya ulioichagua hapo juu?

…………………………………………………………………………………….....

..…………………..............................................................................................

……………………………………………………………………………………...

…………………….............................................................................................

2 Taja tukio au matukio yaliyokuhuzunisha katika riwaya uliyoisoma/ kuihakiki/ kuhadithiwa?

a) ………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

b) ………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

c) ………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

3 Taja athari ulizozipata baada ya kulisoma tukio hilo la kuhuzunisha?

1) ………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

2) ………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

3) ………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

4 Unadhani matukio yenye kuhuzunisha yana kazi (nafasi) gani katika fasihi?

a) ………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

b) ………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………
………………………………………...................................................

c) ……………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………
………………………………………....................................................

**Ahsante Sana**

**B.5. Mwongozo wa Udurusu wa Kimaktaba**

| Vyanzo vya Kudurusiwa | Kipengele Kinachodurusiwa | Lengo la Udurusu |
|---|---|---|
| • Tasnifu<br>• Tahakiki<br>• Majarida<br>• Makala<br>• Wavuti<br>• Vitabu<br>• Riwaya za mwandishi<br>• Ripoti mbalimbali | ❖ Dhana ya Utanzia<br>❖ Dhana ya Tanzia<br>❖ Vijenzi vya Utanzia<br>❖ Matokeo ya Utanzia<br>❖ Dhana ya kifo<br>❖ Dhana ya huzuni<br>❖ Dhana ya riwaya<br>❖ Dhana ya ubunulizi<br>❖ Maisha ya mwandishi<br>❖ Mahusiano ya utanzia na uandishi wa Said Ahmed Mohamed | Kupata taarifa kuhusiana na chimbuko, historia na maendeleo ya utanzia katika fasihi.<br>Kupata ufahamu wa mambo yanayoijenga utanzia na sifa zake.<br>Kupata uelewa kuhusiana na miktadha mbalimbali ya matumizi ya utanzia katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed.<br>Mambo yanayoibua utanzia |

**B.6 Mwongozo wa Majadiliano ya Wanafunzi**

**Maelezo:** Ndugu wanafunzi, utafiti wetu unahusu ***Matumizi ya Utanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed.*** Tafadhalini tunaomba ushirikiano wanu katika kujibu maswali yetu ili kufanikisha lengo la utafiti huu.

1) Tuseme mtu anaposema tanzia katika maisha yetu ya kawaida, anakusudia nini?

2) Kutokana na maana mliyoitoa, tanzia na utanzia zina maana gani katika fasihi?

3) Je mnadhani kuna tofauti gani kati ya tanzia na utanzia?

4) Kwa mawazo yenu ili uitwe utanzia una sifa gani?

5) Nadhani kati yenu hapa ameshawahi kukumbwa na msiba wa kufiwa, mlipata athari gani kwa kila mmoja wenu?

6) Kuna mwandishi wa Zanzibar anayeitwa Said Ahmed Mohamed, kwa uzoefu wenu wa maisha mnamjua kama mtunzi mahiri wa Zanzibar?


7) Kuna kazi yoyote ya mwandishi huyu mliyowahi kuisoma au kuzisoma?

8) Kuna matukio au tukio lolote lililokufanyeni mjihisi kuhuzunika?

9) Kuwepo kwa matukio yenye kuhuzunisha kuna faida au hasara gani kwa msomaji?

10) Kuna malengo gani iwapo mtunzi ameliweka tukio la kuhuzunisha katika kazi yake ya riwaya?

**C. Picha Zinazohusiana na Utafiti**



Mtafiti (kulia) akifanya mahojiano na Prof. Said Ahmed Mohamed (kushoto) katika ofisi za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) mtaa wa Vuga, Wilaya ya Mjini ( Utafiti, Machi 05, 2015).



Mtafiti (Aliyesimama) akifanya majadiliano na wanafunzi wa kidato cha nne, katika skuli ya sekondari Mwanakwerekwe “C” iliyopo Wilaya ya Magharibi Unguja (Utafiti, Januari 06, 2015)




Mtafiti akifanya majadiliano na wanafunzi wa kidato cha tano wa shule ya sekondari ya Nyuki (TPDF) High School (Utafiti, Januari10, 2015)



Mtafiti (aliyesimama katikati) na Mwalimu Khamisi Mwinjuma Simba (aliyesimama kulia) pamoja na wanafunzi wa kidato cha sita, wa shule ya sekondari ya wasichana ya Benmbela. Iliyopo Wilaya ya Mjini Zanzibar. Wakifanya mjadala kuhusu athari za matumizi ya utanzia ( Utafiti, Machi 01, 2015)